Aprili 26 2019

Osvaldo Gratacós, Makamu Rais wa CAO
Mshauri/Mpokea Malalamishi
International Finance Corporation
2121 Pennsylavania Avenue, NW
Washington, DC 204333, USA
Baruapepe: CAO@worldbankgroup.org

**KUH: Malalamishi kuhusu uwekezaji wa International Finance Corporation katika Kenya Commercial Bank na Co-Operative Bank of Kenya**

Kwa Bw, Gratacós,

Malalamishi haya yanawasilishwa na Save Lamu na Kwasasi Mvunjeni Farmers Self-Help Group (wanaojulikana pia kama Kwasasi Farmers Self-Help Group), kutoka Kaunti ya Lamu, Kenya.[1] Save Lamu ni shirika la jumla la kijamii lenye makundi mengine 40 ya Lamu Kenya. Kwasasi Mvunjeni Farmers Self-Help Group ni mkusanyiko wa wakulima waliofurushwa bila fidia kutokana na miundombinu inayohusishwa na kiwanda cha makaa cha megawati 1,050, kinachokusudiwa kujengwa Lamu. Kwa pamoja, tunapinga mradi huu. Tuna hofu kubwa kwamba mradi huu wa kiwanda cha makaa utahatarisha afya, riziki, chakula, mazingira na turathi zenye thamani za kitamaduni.[2] Kaunti ya Lamu ina Lamu Old Town, mji uliotambuliwa na UNESCO kama turathi ya kimataifa[3] pamoja na misitu muhimu ya mikoko. Wakulima wetu wanafurushwa kutoka ardhi yao na wanapoteza mapato na chakula bila mpango imara wa fidia. Viwanda viwili muhimu sana katika eneo la Lamu vya utalii na uvuvi viko hatarini kutokana na uharibifu wa ghafla wa sifa maalumu na uzalishaji utokanao na mazingira ya baharini. Jamii asilia zinawekwa pembeni zaidi na zinapoteza rasilmali muhimu za kimaumbile na kitamaduni walizozisimamia kwa uendelevu kizazi baada ya kizazi. Hofu zetu kuhusu hatari hizi zimeongezwa na ukosefu wa mashauriano yenye kina pamoja na ushirikishaji wa wanajamii katika uandaaji wa mradi.

---

[1] Malalamishi haya yamewasilishwa kwa msaada wa Accountability Counsel and Natural Justice. Tafadhali tazama Nyongeza 1 kwa maelezo zaidi kuhusu Save Lamu, Kwasasi Mvunjeni Farmers Self-Help Group, wawakilishi wao na namna ya kuwasiliana nao. Mkataba wa uwakilishi umeambatwa katika Nyongeza 2.

[2] Hofu hizi pia zimetajwa na asasi za kimataifa kama vile United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO). Tazama UNESCO, *Report of the World Heritage Centre/ICOMOS/ICCROM Advisory Mission To Nairobi Concerning Lamu Old Town, Kenya* (Apr. 2018), uk. 20 na sehemu 3.4.2 https://whc.unesco.org/document/167872 ["UNESCO Report (2018)"] UNESCO, *Report on the Reactive Monitoring Mission to Lamu Old Town Kenya* (Feb. 2015), uk. 20, http://whc.unesco.org/document/135436.

[3] Mwaka wa 2011, UNESCO ilitambua Lamu Old Town kama Turathi ya Dunia Yenye Thamani Kuu Kimataifa. Lamu Old Town imehifadhi sifa zake za jadi nabado ni kikao muhimu cha elimu ya Uislamu na utamaduni wa Waswahili Afrika Mashariki. Kwa taarifa zaidi, UNESCO "Lamu Old Town" https://whc.unesco.org/en/list/1055/.

Tunaamini kwamba International Finance Corporation (IFC) inachangia katika mradi huu hatarishi kupitia mashirika mawili ya fedha: Cooperation Bank of Kenya na Kenya Commercial Bank. Mashirika haya yametoa mchango wa fedha kwa kampuni zinazohusika katika ujenzi wa kiwanda cha makaa. Fauka ya hayo, IFC ina historia ya uhusiano na asasi zingine zinazohusishwa na kiwanda cha makaa. Utaratibu huu wa uwekezaji unatutia hofu kuwa uwekezaji wa sasa wa Co-Operative Bank of Kenya na Kenya Commercial Bank sio - na hautakuwa – wa pekee katika kiwanda cha makaa cha Lamu na athari zake kwa jamii yetu. Ujengaji wa mradi unaonekana dhahiri licha ya ukiukaji wa wazi wa mpango wa uendelevu wa IFC (*IFC Sustainability Framework*). Tuna hofu kuwa ukiukaji huu utaongezeka kadri mradi unavyotekelezwa.

Pamoja na hofu zingine:

- Tathmini ya athari za kimazingira na kijamii kufikia sasa zimepuuza vipengele muhimu vya mradi. Vipengele hivi ni pamoja na: Kuchimba makaa na usafiri pamoja na mtambo wa makaa wa kilomita 15 unaokusudiwa; kibali cha kuchimba ekari 2,000 za mawe ya chokaa na shughuli zingine za uchimbaji barabara ya takribani kilomita 9 ili kufikia eneo la mradi; uhamishaji wa mamia ya wakulima , wavuvi na watumiaji wengine wa ardhi kutokana na miundombinu ya mradi na mabadiliko makubwa yaliyoripotiwa ya teknolojia ya kiwanda cha makaa;

- Watu walioathiriwa hawakutambuliwa au kushauriwa wakati wa kupanga mradi, pamoja na uandaaji na uzinduzi wa tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii ya Julai 2016 (*July 2016 Environmental and Social Impact Study- ESIA*). Jamii zingine zilizoathirika pamoja na jamii asilia na zile zilizoathiriwa na uchimbaji wa mawe ya chokaa katika eneo la Witu, hazikushauriwa kamwe. Wengine walipewa taarifa za juujuu ambazo hazikukamilika na za upande mmoja. Mashirika ya Umma kama vile Save Lamu, yametishwa wakati yakijaribu kuhudhuria au kupanga mikutano yao kuhusu mradi;

- Mamia ya wakulima, wafugaji na watumizi wengine wa ardhi pamoja na jamii asilia na zilizohatarini, wote wanatarajia kuhamishwa kutoka eneo la mradi, na muindombinu mbalimbali ya mradi, licha ya kwamba hakuna mpango wa makazi mapya uliotolewa hadharani kikamilifu kwa mashauriano na umma. Japo kuna muhtasari wa Mpango wa Makazi Mapya, haufikiwi kwa njia rahisi na hauna taarifa za kina ili mtu aweze kuelewa athari za kuhamishwa na zitakavyopunguzwa makali yake na vile fidia itakavyotolewa. Muhtasari huu unaonekana pia kukadiria visivyo kiwango cha uhamishaji hasa miongoni mwa wavuvi ambao hawataweza kufikia maeneo yenye samaki wengi. Hakuna mpango wa Watu Asilia; hakuna Ridhaa Huru, ya Awali na Yenye Taarifa; na hakuna fidia inayofaa kitamaduni inayotolewa kwa jamii asilia zilizoathirika.

- Athari za uchafuzi wa hewa na uanuwai wa viumbe hazijathaminiwa ipasavyo wala kuzuiliwa vyema. Utoaji na urejeshaji wa maji kutoka Kisiwa cha Manda ni hatari kubwa kwa uanuwai kwa sababu ya uchafuzi wa hewa yenye joto. Uchimbaji na uharibifu mwingine wakati wa kujenga na kufanya kazi utaharibu mikoko, mwani na mazingira ya miamba tumbawe. Uchafuzi wa hewa pamoja na mvua ya asidi ni hatari

kwa jamii zetu na mazingira yetu pamoja na majengo ya Lamu Old Town yasiyokuwa na nguvu.

- Hatari za mradi huu kwa turathi za kitamaduni hazijazingatiwa vyema. Mji wa Lamu Old Town, ambao uko kilomita 20 tu kutoka kwenye eneo la mradi ni Turathi ya Kimataifa yenye thamani kubwa. Visiwa jirani pia vina mabaki ya akiolojia (elimu kale) yanayorudi nyuma kihistoria hadi Karne ya 14. Kama ilivyothibitishwa na UNESCO, turathi hizi za kitamaduni zinahatarishwa na kiwanda cha makaa kutokana na uchafuzi wa hewa, ongezeko la watu na maendeleo yasiyodhibitiwa pamoja na kupotea kwa riziki za kitamaduni;

- Hakuna juhudi za dhati zilizofanywa kuhusu vyanzo vya nishati visivyokuwa chafuzi au maeneo tofauti ya kutekeleza mradi huu. Tathmini mbadala zinazopatikana katika Athari za Mazingira na Jamii (ESIA) ya Julai 2016 zinatokana na maoni potovu na mantiki isiyofaa kuhusu vyanzo bora na vinavyowezekana vya nishati.

- Hakujawa na tathmini ya kweli ya jumla ya athari licha ya kuwa Lamu ni kitovu cha usafiri unaopangwa wa Bandari ya Lamu-Sudan Kusini- Ethiopia (LAPSSET) LAPSSET ni muundombinu mkubwa na mradi wenye maendeleo mbalimbali yanayoandaliwa (pamoja na maegesho ya meli 32, mji wa kitalii, kiwanda cha kusafisha mafuta na mifereji ya mafuta) kwa ajili ya Lamu. Kiwanda cha makaa cha Lamu - kiwe au kisiwe sehemu rasmi ya LAPSSET –kitategemea muundombinu wa mradi huu mkubwa pamoja na bandari. Lakini ESIA haitaji athari za jumla za maendeleo haya makubwa kwa jamii zetu.

- Kumekuwa na juhudi duni za kuhakikisha kuwa watu walioathirika watapata manufaa kutokana na mradi huu; na

- Kwa hivyo wanajamii wengi hawaungi mkono mradi huu.

Kwa sababu hatari za mradi huu ni nyingi mno na juhudi za kuzipunguza makali hazitoshi kamwe, IFC na wateja wake hawawezi kuunga mkono kiwanda cha makaa cha Lamu bila kuvunja pakubwa Viwango vya Utendaji vya IFC (*IFC Performance Standards*) na sera ya IFC ya Mazingira na Jamii Endelevu (*IFC Environmental and Social Sustainability Policy*). Kwa hivyo, IFC haina budi kuchukua hatua kuzuia wateja wake wasishiriki katika mradi huu hatari na itathmini uwekezaji mpya katika sekta ya fedha ili kuzuia mchango zaidi.

Hatimaye tunazingatia kuwa ijapokuwa malalamishi haya yanahusu zaidi athari za kimazingira na kijamii za kiwanda cha makaa kinachokusudiwa, kuna hofu kubwa kuhusu kujitosheleza kiuchumi kwa mradi huu.[4] Hali hii inatuongezea hofu kuhusu hatari za kimazingira na kiuchumi.

[4] Tazama Taarifa ya Mashahidi Hindpal Singh Jabbal katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingiza (National Environment Tribunal ), Nairobi, iliyoambatwa katika Nyongeza 3; barua ya Maseneta wa Marekani kwa Rais wa African Development Bank Group na Mkurugenzi Mtendaji ya tarehe Mei 28, 2018 iliyoambatwa katika Nyongeza 5.

Tunahofia kuwa jamii zetu zitaumia zaidi kwa vile mradi huu hautafikia malengo yake ya kiuchumi.

Hapa chini tunafafanua hofu zetu kupitia mada zifuatazo:


**I. Kiwanda cha makaa cha megawati 1,050 katika Lamu iliyotambuliwa na UNESCO - 5**

**II. IFC kuunga mkono mradi hatari - 14**

*A. Kenya Commercial Bank*

**1.** Mkopo wa 2013 kwa KCB- Mradi 3280 5 **15**

2. Mkopo wa 2016, pamoja na uwezekano wa uwekezaji wa fedha katika KCB **16**

**3.** Mkopo wa KCB kwa Centum Investments **16**

**B.** *Co-Operative Bank of Kenya* **17**

**1.** Mkopo wa 2012 kwa Co-Operative Bank of Kenya **17**

**2.** Uwekezaji wa ziada katika Co-Operative Bank of Kenya **17**

**3.** Co-Operative Bank of Kenya inaunga mkono kiwanda cha makaa cha Lamu. **18**

**C.** *Centum Investments ni mdau muhimu katika kiwanda cha makaa* **21**

*D. IFC imedhihirisha taratibu ya kuhusika katika kiwanda cha makaa* **22**

**E.** *Mahusiano mengine na World Bank Group* **22**

**III. Uwekezaji wa IFC unakiuka, au unaweza kukiuka, sera yake ya Uendelevu na Viwango vya Utendaji vya IFC** **23**

**A.** *Washiriki wa kifedha hawazingatii Viwango vya Utendaji vya IFC (IFC PS) na IFC hailindi na kusimamia wajibu wake ipasavyo* **25**

*B. Tathmini ya athari kufikia sasa inapuuza vipengele muhimu vya mradi* **27**

1. Uchimbaji makaa na mfumo wa usafirishaji **29**

2. Barabara ya kufikia eneo la mradi **31**

**3.** Uchimbaji wa chokaa katika Witu **33**

**4.** Mkataba na General Electric (GE) - Teknolojia ya hali ya juu zaidi **33**

5. Athari za kutozingatia 34

**C.** Mashauriano na wanajamii ni ya juu juu, si kamili na hudidimizwa na vitisho na kulipiza kisasi **41**

D. Kutochambua kikamilifu na kutoonyesha hatua za kupunguza makali ya uchafuzi wa hewa na maji, uanuwai wa viumbe, mfumo wa ekolojia na athari za hali ya anga **41**

**1.** Udhaifu wa taratibu za utafiti wa kimsingi unatilia shaka matokeo ya ESIA **42**

**2.** Tathmini ya athari za uanuwai wa viumbe haina taarifa ya kina inayohitajika ili kuendeleza hatua za kutosha za kupunguza makali **43**
3. Uharibifu wa huduma za viumbehai **50**
**4.** Tathmini ya msingi kuhusu hali ya hewa ina upungufu na uchafuzi wa hewa haujatathminiwa ipasavyo **53**
**5.** Tathmini ya athari ya mabadiliko ya hali ya anga **62**

**E.** *Upeo wa watu kuhamishwa na uchumi kubadilishwa umesitiriwa au kupuuzwa* **63**
**F.** *Tathmini za athari hadi leo zinapuuza watu asilia na makundi mengine yaliyohatarishwa* **71**
**G.** *Turathi za kipekee za kitamaduni zinatishwa* **76**
**H.** Tathmini mbadala inategemea dhana potovu na mantiki isiyofaa **80**
**I.** *Athari za kijumla za LAPSSET zimepuuzwa* **84**
**J.** *Watu walioathirika hawatapata manufaa ya mradi-na hili litasababisha wanajamii kutouunga mkono* **85**

**IV. Jitihada zetu za kubainisha masuala haya na Amu Power, wawekezaji wake na mamlaka zingine 86**

**V. Tunahitaji tathmini ya ridhaa kuchunguza masuala yetu 88**

## I. Kiwanda cha makaa cha megawati 1,050 katika Lamu iliyotambuliwa na UNESCO

Mnamo 2013, Serikali ya Kenya ilipendekeza ujenzi wa kiwanda cha makaa cha megawati 1,050 katika Kaunti ya Lamu. Kiwanda hiki kikijengwa kitakuwa kiwanda cha kwanza cha makaa nchini Kenya.

Kaunti ya Lamu ni Kaunti ya kaskazini katika pwani ya Kenya. Imepakana na Bahari ya Hindi upande wa kusini magharibi na Jamhuri ya Somalia kaskazini mashariki. Ina eneo la bara na zaidi ya visiwa 65 vinavyounda Lamu Visiwani. Kati ya hivyo, visiwa vitano vina makazi ya kudumu: Lamu, Pate, Manda, Kiwayu na Ndau.


Kaunti ya Lamu imetambulika kimataifa kwa ajili ya mazingira yake ya baharini na nchi kavu pamoja na kinamasi, mbuga, savana, misitu ya mibuyu na mikoko, matumbawe, ufuo wa bahari na matuta ya mchanga.[5] Lamu ina asilimia 70 ya mikoko yote ya Kenya. Mikoko ni rasilimali

[5] Pamoja na Hifadhi ya Dodori National Reserve, Kiunga Marine National Reserve (hifadhi iliyotambuliwa kama UNESCO Biosphere Reserve) na maeneo yenye unyevunyevu yaliyohifadhiwa chini ya mkataba wa Ramsar. Tazama Sehemu ya III.D hapo chini.

muhimu inayokinga ardhi dhidi ya mmomonyoko wa udongo na mafuriko na huwa ni mahali pa kutegea mayai na malezi kwa viumbe vingi vya baharini.[6]

Eneo la ekari 975 linalokusudiwa kujengwa kiwanda cha makaa liko Lamu bara, karibu na misitu muhimu ya mikoko ya pwani. Ardhi hii inatwaliwa kwa lazima kutoka kwa wakulima wenyeji. Miaka mingi baada ya kuhamishwa kwao kutangazwa, wakazi hawa bado wamekumbwa na wasiwasi kuhusu kiwango na aina ya fidia na msaada wa kuhamishwa utakaotolewa.[7] Wakulima wapatao 109 na jamii zao tayari wamehamishwa, bila mashauriano wala fidia, kutokana na ujenzi wa barabara ya kufikia kiwanda.[8]

**Kielelezo 1: Mahali panapotarajiwa kujengwa kiwanda cha makaa, Lamu**




6 Tazama Ripoti ya *Lamu County Spatial Plan (2016-2026) Final Report* (Juzuu. I, Mei 2017), uk. 124.

7 Kama ilivyojadiliwa katika Sehemu ya III.E hapo chini, taarifa juu ya kiasi cha ardhi itakayotwaliwa, na aina ya fidia ambayo itatolewa, imebadilika kwa kiasi kikubwa, na Mpango wa Makazi Mapya (Resettlement Action Plan) kamili bado haujawekwa wazi.

8 *Tazama* Sehemu ya III.B.2 hapo chini.

*Chanzo: UNESCO: Ripoti ya Kituo cha Turathi Duniani/ ICOMOS/ ICCROM Ujumbe wa Ushauri kutoka Nairobi kuhusu Lamu - Advisory Mission to Nairobi Concerning Lamu Old Town, Kenya (Aprili 2018, Kielelezo 6.12*

Eneo hili la ujenzi ni takribani kilomita 20 kaskazini mwa Lamu Old Town katika kisiwa cha Lamu. Lamu Old Town ni turathi ya kimataifa ya UNESCO kwa sababu ni makazi ya zamani ya Waswahili katika eneo la Afrika Mashariki yaliyohifadhiwa vyema. Ni jamii ndogo na ya kihafidhina inayojilinda na kuhifadhi hadi sasa utamaduni wa ujenzi na taratibu za kijamii, kitamaduni na kidini.[9]

Tunaelewa kwamba makaa yatakayotumika kiwandani yatatoka Afrika Kusini na meli zitatumia maegesho maalumu katika bandari inayojengwa sasa kisiwani Manda (ambao ni mradi mkubwa sana kivyake, kama inavyofafanuliwa hapo chini).[10]

Mnamo Septemba 2014, serikali iliipa kampuni ya Amu Power kandarasi ya kiwanda cha makaa. Amu Power ni chombo maalumu kilichoundwa na Gulf Energy, kampuni ya kibinafsi ya Kenya na Centum Investments kampuni ya hisa za umma ya Kenya ya uwekezaji. Mnamo Mei 2018, Kampuni ya Kimarekani ya General Electric (GE) na Amu Power na Centum zilitangaza 'Mkataba wa Ushirikiano' wa kuipa Amu Power teknolojia ya kisasa zaidi katika ujenzi wa kiwanda cha makaa (na fursa kutolewa ili GE ipate maslahi sawia katika kampuni ya Amu Power),[11] japo maelezo ya kina kuhusu mkataba huu hayajatolewa. Fedha za mradi za kiasi cha Dola za kimarekani bilioni mbili (US$ 2b) zinatarajiwa kupatikana kupitia:[12]

- Asilimia 75 (75%) ya kugharamia madeni mawili: Deni la Dola (US$) bilioni1.2 za Industrial and Commercial Bank of China na deni la Dola (US$) milioni 3000. Madeni haya yanahusishwa kwa wakati fulani na Standard Bank of South Africa (ambao baadaye waliamua kutoshiriki );[13] na

[9] UNESCO "Lamu Old Town" https://whc.unesco.org/en/list/1055/.

[10] Kurrent Technologies *Environment and Social Impact Assessment (ESIA) Study for the Proposed 1,050MW Coal Fired Power Plant Project, Kenya* (16 Jul. 2016), Sura 4 https://www.amupower.co.ke/esia.html. [2016 ESIA] Kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya III, tumefahamishwa kuwa serikali ya Kenya hatimaye inakusudia kuwa na migodi ya makaa, Kitui Kenya. Hata hata mipango hii itaendelea, kutakuwa na kipindi cha miaka mingi ya kuagiza makaa kutoka nje ya nchi.

[11] Tazama, pamoja na makala zingine, GE Africa Newsroom "Kenya's Amu Power Signs Clean Coal Technology Agreement with GE" (Mei 2018) https://ge.africa-newsroom.com/press/kenyas-amu-power-signs-clean-coal-technology-agreement-with-ge. Hata hivyo, ripoti zingine zimeonyesha wasiwasi kuhusu uwekano wa mkataba huu utahitimishwa: deCOALonize Kenya via Medium "450 million dollar deal between Gulf Energy & General Electric for the development of coal power still under discussion" (Jun. 2018) https://medium.com/@deCOALonize/450-million-dollar-deal-between-gulf-energy-general-electric-for-the-development-of-coal-power-a9c4497fea8; Profesa Daniel Kammen, RAEL Berkeley "General Electric Reconsiders Investment In Lamu Coal Plant" (Jul. 2018) https://rael.berkeley.edu/2018/07/general-electric-reconsiders-investment-in-lamu-coal-plant/. Tazama pia barua ya GE kwa Save Lamu (19 Feb. 2019), imeambatwa katika Nyongeza 4.

[12] Wasilisho la Amu Power, kwa Tume ya Nishati ya Kenya - Kenya Energy Regulatory Commission (28 Sept. 2016); Reuters "UPDATE 2-Kenya's Centum to finalise power plant funding this year" (12 Jun. 2018) https://www.reuters.com/article/centum-invt-results/update-2-kenyas-centum-to-finalise-power-plant-funding-this-year-idUSL8N1TF0CF.

[13] Tumefahamishwa kwamba Standard Bank ilipewa idhini kuongoza mpango wa mkopo wa Dola milioni US$300, lakini baadaye ilikataa kushiriki katika mradi huu: 350.org "Standard Bank Sets The Record Straight on Financing Lamu" (19 Oct. 2017) https://350africa.org/standard-bank-sets-the-record-straight-on-financing-lamu/; The Star "Standard Bank says not funding Lamu Coal" (18 Oct. 2017) https://www.the-star.co.ke/news/2017/10/18/standard-bank-says-not-funding-lamu-coal_c1654106.

- Asilimia 25 (25%) kuongeza mtaji kutoka kwa wanahisa wa Amu Power.

Kama inavyofafanuliwa katika sehemu ya II hapo chini, maelezo mengi ya kina kuhusu mipango ya kugharamia mradi hayako wazi.

Kwa mujibu wa ripoti ya ESIA ya Julai 2016,[14] kiwanda cha makaa kitakuwa na vitengo vitatu[15] vya nishati ya makaa. Kwa jumla, inatarajiwa kuwa kiwanda kitatoa megatani 2.8 (mt) za makaa kila mwaka au metriki tani 10,000 kila siku. Baada ya uchomaji, jivu litamwagwa kwenye yadi ya jivu (itakayojaa baada ya miaka 15). Kiwanda kitatumia aina ya mfumo wa kuweka baridi mara moja. Mfumo huu utatoa maji ya bahari kutoka Kisiwa cha Manda kupitia mtaro. Maji baridi yatarudi Manda kupitia bomba ya chini kwa chini huku yametolewa chumvi na yakiwa na joto. Maji ya bahari pia yatatumika kuoshea gesi ya dohani kama sehemu ya mfumo wa kutoa salfa. Gesi ya moshi itarushwa hewani kufikia mita 210. Kiwanda kitafanya kazi masaa 24 kwa siku, siku saba kila juma isipokuwa siku zilizoratibiwa za matengenezo. Kiwanda cha makaa pia kitahitaji miundombinu ifuatayo:

- Uchimbaji wa chokaa katika Witu. Kibali cha uchimbaji wa ekari 2000 tayari kimetolewa na mamlaka ua Kaunti. Chokaa itahitajika ili kudhibiti mfumo wa uchafuzi wa utoaji salfa kwenye gesi majimaji ya dohani. Itasafirishwa kupitia nchi kavu na baharini hadi kwenye kiwanda cha umeme;
- Mfumo wa kupokea makaa pamoja na maegesho katika bandari ya Lamu, vifaa vya kupokea makaa na mfumo wa takribani kilomita 15 wa kuhawilisha makaa kutoka bandarini hadi kwenye yadi kwa muda;
- Mazizi mawili ya makaa  yanayoweza kuchukua makaa kwa siku 30-38(yanayoweza kuhifadhi metriki tani);
- Kistesheni cha KV 400;
- Eneo la wafanyikazi linaloweza kukaliwa na watu baina ya 250 na 300;
- Mfumo wa gari moshi wa kusafirisha makaa endapo makaa ya Kenya yatapatikana;
- Barabara, majengo na miundo mingine.

Licha ya tangazo la GE la Mei 2018 kwamba itatoa teknolojia ya juu zaidi kwa ajili ya kiwanda cha makaa cha Lamu,[16] hatuna habari kuhusu tathmini za kiufundi au kimazingira na kijamii tangu hapo. Ijapokua teknolojia hii ni hatua bora ilinganishwapo na teknolojia inayofafanuliwa katika ESIA ya 2016, kama inavyoelezwa katika sehemu III B.6 hapo chini, hatari za uchafuzi na athari zingine kwa jamii bado zipo.

---

*Linganisha na* Standard Bank Group, *Annual Integrated Report 2015* at p. 47 "Standard Bank and ICBC have concluded debt financing agreements with a consortium of Kenyan investors for the building of the 1000 megawatt Amu coal-fired power plant." https://thevault.exchange/?get_group_doc=18/1461565691-SBG_FY15_Annualintegratedreport.pdf.

[14] 2016 ESIA, Sura 4.

[15] Kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya III.B.4 hapo chini, teknolojia ya juu zaidi ya GE ina ufanisi mkubwa mkubwa kuliko teknolojia yay a hapo awali inayotolewa maelezo katika ESIA ya 2016. Hata hivyo, teknolojia ya juu zaidi haiondoi hofu zetu kuhusu hatari za uchafuzi wa hewa, watu kuhamishwa na uharibifu wa mazingira na maisha ya jamii.

[16] Tazama angalizo la 11.

Kiwanda kinachokusudiwa kimetimiza kanuni kadha za kisheria za Kenya, japo mna mapengo na udhaifu:

- Machi 14, 2016: Amu Power iliwasilisha Ripoti ya Kutathmini Athari za Kimazingira (*Environmental Impact Assessment Study Report (EIA*) kwa mamlaka za Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA));
- Julai 29, 2016: Gazeti la Serikali lilichapishwa likitaka maoni ya umma kuhusu EIA, na likatoa tarehe ya makataa ya Agosti 29, 2016;
- Septemba 7, 2016: NEMA iliipa EIA leseni, siku nane tu baada ya makataa ya maoni ya umma;
- Septemba 28, 2016: Amu Power waliomba leseni ya umma kutoka kwa Kamisheni ya Kudhibiti Nishati (*Energy Regulatory Commission* (ERC));
- Oktoba 27, 2016: Wakati wa kipindi cha maoni ya umma, Save Lamu iliwasilisha pingamizi zake kuhusu ombi la leseni la ERC;
- Novemba 7, 2016: Save Lamu na wakazi wengi wa Lamu walikata rufaa kuhusu leseni ya EIA katika Mahakama ya Mazingira ya Kitaifa (*National Environment Tribunal* (NET)). Wanasubiria hukumu kuhusu jambo hili;
- Februari 2017: ERC ilitupilia mbali malalamiko ya Save Lamu kuhusu ombi la ERC la leseni. Hata hivyo, leseni bado haijatangazwa katika Gazeti la Serikali.[17]

Ujenzi wa kiwanda cha makaa haujaanza ijapokuwa maendeleo ya barabara ya kufikia eneo la kiwanda na uhamishaji wa wakulima wa Kwasasi yanaendelea. Zaidi ya wakulima 109 na familia zao wamepoteza riziki zao na chakula bila fidia wala mashauriano.[18]

Uelewaji wa kiwanda cha Lamu kinachokusudiwa na athari zake utawezekana tu katika muktadha wa mradi mkubwa wa LAPSSET, unaofafanuliwa na serikali ya Kenya kama muundombinu mkubwa zaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kwa vyovyote, maendeleo ya miradi hii imefungamana sana endapo kiwanda cha makaa cha Lamu kinawakilisha kipengele muhimu cha mradi wa LAPSSET au la. Vipengele muhimu vya LAPSSET vitakavyopatikana Lamu ni pamoja na:[19]

- Maegesho ya meli 32 katika bandari ya Manda. Ujenzi wa Awamu ya Kwanza ya LAPSSET, maegesho matatu, barabara na majengo mengine bandarini unaendelea (Tazama Kielelezo 2). Egesho la kwanza linatarajiwa kukamilika kufikia Juni 2019 na

[17] Baadhi ya rekodi za ERC zinaonyesha kuwa ERC ilitoa leseni ya umeme mnamo Machi 3, 2017, ijapokuwa jambo hili limekuwa gumu kuthibitisha.

[18] *Tazama* Barua ya Kwasasi Farmers Self Help Group kwa Wizara ya Usafiri (31 Aug. 2018), Barua ya Kwasasi Farmerskwa Mwenyekiti Tume ya Kitaifa ya Ardhi ( National Land Commission) (5 Nov. 2018), na barua ya Kwasasi Farmers Self Help Group kwa Mwenyekiti, Tume ya Kitaifa ya Ardhi (National Land Commission) (13 Jan. 2019), zote zik Nyongeza 4.

[19] Tovuti ya LAPSSET http://www.lapsset.go.ke; Ripoti ya UNESCO (2018), §3.2.3; Business Daily “Lamu residents set to reap from completion of mega projects” (8 Jan. 2019) https://www.businessdailyafrica.com/corporate/shipping/Lamu-residents-set-to-reap-from-completion-of-mega-projects/4003122-4926618-11swalp/index.html.

meli ya kwanza kutia nanga mnamo Novemba 2019. Shughuli hizi zimesababisha ung'oaji wa mikoko, uchimbaji na uimarishaji ardhi ufukoni. Kufikia mwaka wa 2030 inatarajiwa kuwa maegesho ya meli 29 yatakuwa yamepangwa: maendeleo ambayo, kwa hakika, ni ya kimataifa;

- Majengo ya viwanda karibu na bandari. Eneo la viwanda litakuwa na shughuli nyingi zinazoweza kuchafua mazingira. Shughuli hizi ni pamoja na viwanda vya usafirishaji wa mafuta na vya kemikali za petroli, viwanda vya chakula na matunda, kituo cha karantini (wanyama kupewa dawa), usafishaji wa mbao, kiwanda cha nguo, matengenezo ya meli, uandaaji wa vifaa vya ujenzi wa ukanda wa LAPSSET, na kituo cha huduma kwa utoaji wa mafuta na gesi sehemu za bara. Eneo la bandarini na viwandani litakuwa Eneo Maalumu la Kiuchumi (*Special Economic Zone* - SEZ));

- Barabara kubwa, pamoja na ya Lamu – Garissa - Isiolo (km 537) na nyingine ya Lamu – Witu - Garissa (115), zimepata kipaumbele ili kuwezesha usafirishaji wa mizigo kuiingia na kutoka bandari ya Lamu (kwa kuunganisha miundombinu ya barabara iliyoko);

- Reli ya Lamu - Isiolo ili kusafirisha mizigo kutoka na kuingia bandari ya Lamu;

- Bomba za mafuta na bidhaa za mafuta kutoka Lamu hadi Lokichar. Bomba hizi zitasafirisha mafuta kutoka Lokichar kusini (Turkana) hadi Lamu ili kupelekwa ng'ambo;

**Kielelezo 2: Bandari ya Lamu, Maegesho 1 -3 yanayojengwa**



*Chanzo: UNESCO, Ripoti ya Kituo cha Turathi Duniani/ ICOMOS/ICCROM Advisory Mission to Nairobi concerning Lamu Old Town, Kenya (Aprili. 2018) Kielelezo 6.4*

- Mji mpya wa Lamu eneo la bara, unaotarajiwa kuwa na wakazi milioni moja kufikia 2030;
- Mji wa kitalii, pamoja na uwanja wa gofu na mahoteli ya maghorofa (Taz. Kielelezo 3);
- Nyaya za kusambaza umeme baina ya Lamu – Garissa – Isiolo – Lokichar;
- Uwanja mpya wa ndege wa kimataifa. Vifaa vya awali, pamoja na barabara ya ndege na kituo cha ndege, vimekamilika;
- Mtambo wa maji ya Lamu kutoka bwawa kubwa la mto Tana;
- Kiwanda cha kutoa maji chumvi; na
- Ujenzi wa gati nyingi mpya.

**Kielelezo 3: Mji wa kitalii wa Lamu**



*Chanzo: Mpango mkuu wa LAPSSET, uliotolewa na UNESCO, Ripoti ya Kituo cha Turathi Duniani/ ICOMOS/ICCROM Advisory Mission to Nairobi Concerning Lamu Old Town, Kenya (Aprili. 2018) Kielelezo 6.8*

Serikali ya Kenya inakifafanua kiwanda cha makaa cha Lamu kinachokusudiwa kama mradi shirikishi wa LAPSSET.[20] Hata hivyo, uhusiano baina ya miradi hii miwili unaonekana kama kwamba una ukuruba mkubwa zaidi. Pamoja na uhusiano mwingine, Mamlaka ya Maendeleo ya

[20] "Associated Projects" http://www.lapsset.go.ke/projects/others/.

LAPSSET (*LAPSSET Corridor Development Authority*) ndiyo inayosimamia ardhi ambapo kitajengwa kiwanda cha makaa kinachokusudiwa.[21]

Kuna mtafaruku miongoni mwa jamii ya Lamu kuhusu kiwanda cha makaa, pamoja na maendeleo mengine ya LAPSSET. Kama ilivyojadiliwa kwa undani Sehemu ya III wanajamii wengi wanakipinga kiwanda hiki na wanahofu kuhusu athari za kujengwa kiwanda cha makaa katika eneo hili lenye utamaduni na ekolojia ya jadi na wamekuwa wakiandamana kupinga kiwanda hiki. Hili hutokea zaidi pindi wanajamii wapatapo taarifa kamili kuhusu athari za mradi. Hata hivyo, baadhi ya wanajamii wamekuwa wakiunga mkono kiwanda hiki kutokana na ahadi za ajira, fidia na maendeleo ya kiuchumi.

Kama inavyobainishwa katika sehemu ya III, ukosefu wa mashauriano huzipa nguvu hofu hizi na migawanyiko ya wanajamii. Taarifa zinazotolewa katika mikutano na wanajamii ni ya juujuu, haieleweki, na sio sahihii wala kamili. Mpango wa Makazi Mapya (*Resettlement Action Plan*) haujatolewa kikamilifu hadharani licha ya mamia ya wakazi kuhamishwa,[22] na ESIA ilicheleweshwa na haijakamilika.[23] Save Lamu wamekumbwa na ulipizaji kisasi na vitisho wakati wakijaribu kuandaa vikao vya wanajamii ili kutoa taarifa kuhusu mradi huu.[24]

Licha ya taarifa zisizokuwa kamili kuhusu athari za mradi, ni wazi kuwa Lamu itahatarishwa na uchafuzi wa hewa, maji na ardhi, upungufu wa rasilimali za majini na uharibifu wa makazi muhimu. Uhamishaji wa watu na shughuli za kiuchumi pamoja na uharibifu wa mazingira ni hatari kubwa kwa afya, riziki, chakula na turathi muhimu za kitamaduni. Athari zake zitadhihirika katika eneo lote la Lamu. Wakazi wanaeleza hivi:

---

[21] *Tazama* Barua ya Mamlaka ya Maendeleo ya LAPSSET ( LAPSSET Corridor Development Authority) kwa Tume ya Kitaifa ya Ardhi (National Land Commission) kuhusu Uidhinishaji wa Mpango wa Makazi Mapya Approval of Resettlement Action Plan) kwa ajili ya Kiwanda cha Makaa cha 1,050 MW katika Kwasasi, Kaunti ya Lamu (23 Aug 2018), iliyoambatishwa kama Nyongeza ya 5 katika malalamishi haya.

[22] "Kenya: Lamu County Puts Coal-Fired Power Plant on Hold" AllAfrica (Aug. 2016), http://allafrica.com/stories/201608100091.html; Barua ya Mamlaka ya Maendeleo ya LAPSSET (LAPSSET Corridor Development Authority) kwa Tume ya Kitaifa ya Ardhi (National Land Commission) kuhusu kuhusu Uidhinishaji wa Mpango wa Makazi Mapya Approval of Resettlement Action Plan) kwa ajili ya Kiwanda cha Makaa cha 1,050 MW katika Kwasasi, Kaunti ya Lamu (23 Aug 2018), iliyoambatishwa kama Nyongeza ya 5 katika malalamishi haya; Baraka FM "Lamu coal plant woes deepen as land owners reject compensation" (5 Sept. 2018) http://barakafm.org/2018/09/05/lamu-coal-plant-woes-deepen-as-land-owners-reject-compensation/. Pamoja na wakulima walioko katika mahali pa mradi, muhtasari wa wa Mpango Kamili wa Makazi Mapya (hauna tarehe) – uliotangazwa na the African Development Bank – unafafanua uwezekano wa kuhamishwa wavuvi, wakataji wa mikoko, wawekaji nyuki na biashara ya nafaka: https://www.afdb.org/fileadmin/uploads/afdb/Documents/Environmental-and-Social-Assessments/Kenya_-_Lamu_Coal_Power_Project_%E2%80%93_RAP_Summary.pdf.

[23] Notisi ya Rufaa, Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environmental Tribunal) Rufani Na. NET/196/2016, 3-4, http://accountabilitycounsel.org/wp-content/uploads/2017/11/NET-Notice-of-Appeal-Cover-Page-w_-NET-Stamp-and-Appeal.pdf; Save Lamu, Barua kwa African Development Bank Atakayezingatia: Gabriel Negatu (24 Nov. 2017) Imeambatwa Nyongeza 4.

[24] *Tazama* Human Rights Watch and National Coalition for Human Rights Defenders, *They Just Want to Silence Us" Abuses Against Environmental Activists at Kenya's Coast Region* (2018) https://www.hrw.org/sites/default/files/report_pdf/kenya1218_web2.pdf; Accountability Counsel "Escalating Threats in Lamu, Kenya Interfere with Local Communities' Right to Public Participation" (24 May 2017) https://www.accountabilitycounsel.org/2017/05/escalating-threats-in-lamu-kenya-interfere-with-local-communities-right-to-public-participation/.

*"Sisi wenyeji wa Lamu tunategemea maliasili ili kupata riziki kwa ajili ya lishe, makazi, afya, ibada katika sehemu takatifu na kuendeleza tamaduni zetu. Mazingira yetu yana afya, nasi pia tuna afya. Mazingira yetu yakiumia nasi pia tunaumia."*[25]

*"Tunahuzunishwa kwamba thamani yoyote ya kiekolojia iliyopo katika eneo hili itapotea daima. Tuna hofu kuwa jivu litapelekwa na upepo wa monsuni na litatua katika paa za nyumba zetu, kwenye mimea na baharini. Huenda uchafuzi huu ukapelekwa na mvua na kuchafua ardhi na maji."*[26]

Kabla hatujaeleza kwa kina hofu hizi tutafafanua  uhusiano baina ya IFC na mradi huu hatari.

## II. IFC inaunga mkono mradi hatari

Kwa sababu ya ukosefu mkubwa wa uwazi, ni vigumu kufahamu utaratibu wa uwekezaji unaounga mkono kiwanda cha makaa cha Lamu. Hata hivyo, huku tukitegemea taarifa ndogo zilizoko, tunaamini IFC inahusika kwa hali fulani na kiwanda cha makaa cha Lamu kupitia wateja wa kati wa kifedha ambao ni Kenya Commercial Bank na Co-Operative Bank of Kenya (Taz. Kielelezo 4). IFC pia ina historia ya uwekezaji katika mashirika mengine ya kifedha yanayohusishwa na kampuni zinazojenga kiwanda cha makaa cha Lamu.

Miradi muhimu, kwa ajili ya uchanganuzi ni:

| Mradi wa IFC | Aina ya msaada wa ugharimiaji | Tarehe ya kudhinishwa | Hali | Uanishaji wa E & S |
|---|---|---|---|---|
| **Kenya Commercial Bank** | | | | |
| Kenya Commercial Bank III – Mradi 32805 | Mkopo | Mei 16, 2013 | Hai | F1- 2 |
| Kenya Commercial Bank III – mradi 36791 | Mkopo na labda mtaji | Septemba 22, 2016 | Hai | F1- 2 |
| **Co-Operative Bank of Kenya** | | | | |
| Co-Operative Bank of Kenya – Mradi 31321 | Mkopo | Oktoba 5, 2012 | Hai | F1- 2 |
| Co-Operative Bank of Kenya II – Mradi 35393 | Mkopo | Disemba 22, 2015 | Hai | F1 - 2 |
| Co-Operative Bank of Kenya III – mradi 41133 | Mkopo | Machi 27, 2018 | Hai | F1 - 2 |
| AMSME Co-Operative Bank of Kenya – Mradi 601493 | Huduma za ushauri | Oktoba 11, 2016 | Hai | F1 - 2 |
| DFS COOP Awamu 2, Mradi 602467 | Huduma za ushauri | Oktoba 12, 2017 | Hai | F1 - 2 |

[25] Save Lamu, *The Lamu County Biocultural Community Protocol: The Lamu Indigenous Community and their Rights to the Preservation of their Natural Resources, Cultures, Heritage and Management of Biodiversity* (Dec. 2018), §6.0. http://www.decoalonize.org/wp-content/uploads/2019/04/Lamu-County-BCP-2.pdf [BCP].

[26] BCP, §9.1.2.

Kabla ya kufafanua uhusiano baina ya IFC na kiwanda cha makaa cha Lamu kwa kina, tunazingatia kuwa IFC hivi majuzi imeanza kuonyesha katika wavuti yake "matumizi ya mapato/walionufaika " – ambao ni sekta 'lengwa' ya deni kutokana na *baadhi* ya mikopo yake. Hili ni tokeo la hivi majuzi. Hata hivyo, katika hali nyingi sekta inayotambulishwa kwenye sehemu ya "matumizi ya mapato" hailingani kikamilifu na upeo wa mradi. Fauka ya hayo, sehemu ya "matumizi ya mapato" haina maelezo kuhusu namna na kama udhibiti wowote unatekelezwa; japo sekta yenye kipaumbele inalengwa, hili halizuii matumizi ya fedha katika shughuli zingine za ukopeshaji.

### A. Kenya Commercial Bank

Mnamo 2013 na 2016, IFC ilitoa mikopo miwili kwa Kenya Commercial Bank (KCB) mkopo wa Dola (US$) milioni 225.[27] Pia, Bodi ya Wakurugenzi iliidhinisha mkopo wa Dola US$ milioni 70 kama hisa bila iba kwa KCB.[28] Mikopo yote miwili iko hai.

1. *Mkopo kwa KCB wa 2013- Mradi 32805*

| *Kenya Commercial Bank III- Mradi 32805* | | |
|---|---|---|
| *Kuidhinishwa: Mei 16, 2013* | *Hali: Hai* | *Uainishaji wa E&S F1-2* |

Mradi huu ni wa Dola (US$) milioni 150 za "mkopo mkubwa usio na dhamana" kutolewa kwa KCB "ili kuiwezesha benki hiyo kuwa na fedha za muda mrefu kutekeleza miradi yake ya kimkakati."[29]

Ijapokuwa mradi unaeleza kuhusu 'haja ya kuongeza ufikiaji wa fedha kwa ajili ya sekta muhimu za uchumi kama vile kampuni ndogo ndogo za biashara (SME), biashara ya kilimo, benki ndogo ndogo na… deni za rehani," mkopo huo hauonyeshi udhibiti ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika kwa shughuli hizo pekee.

Kinyume na hilo, maelezo ya mradi yanasema kuwa mradi huo utakuwa na upeo mpana. "Athari yake ya maendeleo" ni pamoja na malengo mapana kama vile "kuimarisha mashindano katika sekta ya benki ya Kenya" na "kuunga mkono maendeleo ya asasi ya benki kikanda." Upeo huu mpana unapewa nguvu na "mantiki ya IFC ya uainishaji wa kimazingira na kijamii," inayoonyesha kuwa tathmini za IFC ya mradi huu ilijumuisha orodha yote ya fedha za KCB pamoja na deni za kampuni (zenye takribani asilimia 50% ya jumla ya fedha za KCB).

Hakuna sehemu ya "matumizi ya mapato" katika uwazi wa mradi.

---

[27] Isitoshe, IFC ilitoa mkopo wa Dola milion $100 kwa Kenya Commercial Bank mnamo Juni 2011: Tovuti ya IFC Project Information Portal, *Kenya Commercial Bank II* (2011) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SPI/29664. Hata hivyo, hali ya mradi ilibadilika majuzi na kuwa "Imekamilika."

[28] Tovuti ya IFC Project Information Portal, *Kenya Commercial Bank Limited* (2016). https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/36791.

[29] Tovuti ya IFC Project Information Portal, *Kenya Commercial Bank* (2013) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/32805.

2. *Mkopo wa 2016 na uwezekano uwekezaji wa mtaji kwa KCB*

| *Kenya Commercial Bank III- Mradi 36791* | | |
|---|---|---|
| *Kuidhinishwa: Septemba 22, 2016* | *Hali: Hai* | *Uainishaji wa E&S F1-2* |

Mradi huu wa pili ni hasa mkopo wa Dola (US$) milioni 75 zilizotolewa kwa KCB.[30] Ijapokuwa maelezo ya mradi na sehemu ya "matumizi ya mapato" zinasisitiza sekta ya biashara ndogo ndogo za SME, vipengele vingine vya uwazi wa mradi vinaonyesha kuwa mkopo huu utakuwa na upeo mpana zaidi. Maelezo ya mradi yanasema kuwa mkopo huu ni "sehemu ya juhudi za KCB za utafutaji mtaji wa Dola (US$) milioni 250 ili kuimarisha hali yake ya mtaji katika muktadha wa kanuni za udhibiti kupita mtaji wa kinga. "Mantiki ya uainishaji wa kimazingira na kijamii" pia unarejelea mtaji mzima wa KCB kama "benki ya jumla inayotoa huduma za fedha kwa biashara ndogo ndogo (SME), kampuni na wateja wa biashara katika sekta mbalimbali hasa katika ujenzi wa viwanda, huduma na biashara." Kutokana na sababu hizi, hatuna sababu ya kuamini kuwa kuna viwango vinavyoweza *kufuatiliwa na kushurutushwa* katika matumizi ya fedha za sekta ya biashara ndogondogo (SME).

Maelezo ya IFC kuhusu mradi huu pia yanarejelea Dola (US$) milioni 70 za uwekezaji wa mtaji zilizoidhinishwa na Bodi. Hata hivyo, kipengele hiki hakiko wazi. Endapo uwekezaji wa mtaji ulifanywa, basi IFC imejidhihirisha katika uwekezaji wote wa KCB.

3. *Mkopo wa KCB kwa Centum Investments*

Baada ya uwekezaji wa IFC kwa KCB mnamo 2013 na 2016 , KCB imetoa fedha kwa Centum Investments, mhisa mkuu wa Amu Power.

Ripoti ya KCB ya mwaka wa 2017 inaonyesha kuwa Centum ilikuwa na fedha za kiasi cha shilingi milioni 240.7 ndani ya KCB mnamo 2017, ilhali ilikuwa na shilingi bilioni 15.4 mnamo 2016.[31] Centum Investments ilichukua deni hili kama ilivyohitajika ili kugharamia shughuli zake za biashara, pamoja na gharama za kiwanda cha makaa cha Lamu.

Ijapokuwa fedha hizi zenye kusudi maalumu hazionyeshwi kwenye Ripoti ya Centum ya Mwaka wa 2018,[32] taarifa za muda za fedha za 2019 zinaonyesha jumla ya ukopaji wa Shilingi bilioni 1.2 kutoka kwa KCB kufikia Septemba 30, 2018, ambazo ni nyingi ilinganishwapo na Shilingi milioni 128.5 kufikia Machi mwaka huo.[33] Matumizi ya fedha hizi hayako wazi katika taarifa hizo za muda za fedha.

---

[30] Tovuti ya IFC Project Information Portal, *Kenya Commercial Bank Limited* (2016). https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/36791.

[31] Centum Investment, *2017 Annual Report*, pp. 206-207. http://www.centum.co.ke/images/docs/Annual_Report_2017.pdf.

[32] Centum Investment, *2018 Annual Report*, p. 187 http://www.centum.co.ke/images/docs/CICL_Full_-Annual_Report_FY18.pdf.

[33] Centum Investment, *Interim Report and Financial Statements: 6 Month Period Ended 30 September 2018*, p. 30 https://centum.co.ke/images/docs/CICP_Group_Interim_Financial_Statement_30_September_2018.pdf.

## B. Co-Operative Bank of Kenya

### 1. *Mkopo wa 2012 kwa Co-Operative Bank of Kenya*

| *Coop Bank of Kenya- 31321* | | |
|---|---|---|
| Uidhinishaji: Oktoba 5, 2012 | Hali: Hai | *Uainishaji wa E&S F1-2* |

Mnamo Disemba 2012, IFC iliipa Co-Operative Bank of Kenya mkopo wa Dola (US$) milioni 60 utakaolipwa kwa muda wa miaka saba ili "kuunga mkono deni za muda mrefu" na "madeni kwa kampuni za biashara," pamoja na malengo mengine.[34]

Ijapokuwa maelezo ya mradi wa IFC na sehemu ya "matumizi ya mapato" zinaonyesha kuwa walengwa wa mikopo haya ni biashara ndogo ndogo (SME), mkopo huu hauonekani kuwa na udhibiti kamili ufikiapo walengwa hawa. Lengo kuu la mradi huu limeelezwa kwa mapana: "Kuunga mkono maendeleo ya Benki, kushughulikia mizani ya Benki na ukosefu wa urari, na kuisaidia kufikia malengo yake ya gharama za Dola (US$)." "Mantiki ya uainishaji wa kimazingira na kijamii" ya IFC pia inaonyesha kuwa mkopo utatolewa kwa upana katika orodha yote ya fedha za Co-Operative Bank: "Biashara hii inahusu mpango wa deni wa kufikia Dola (US$) milioni 60 zitakazotolewa kwa **kampuni za biashara**,"[35] nyumba na biashara za kilimo (msisitizo wetu). Kwa hivyo hapaonekani chochote kinachoeleza kuzuia mapato ya mkopo huu kutumiwa kwa ajili ya kiwanda cha makaa cha Lamu.

### 2. *Uwekezaji wa ziada katika Co-Operative Bank of Kenya*

IFC imeendelea kuunga mkono shughuli za Co-Operative Bank of Kenya kupitia mikopo mingine miwili na miradi miwili ya ushauri.[36]

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| *Co-Operative Bank II, Mradi 35393* | *Mkopo: Dola US$ milioni 105* | *Uidhinishaji: Disemba 22, 2015* | *Hali: Hai* | *Uainishaji wa E&S: F1-2* |
| *Co-Operative Bank III, Mradi 41133* | *Mkopo: Dola US$ milioni 150* | *Uidhinishaji: Machi 27, 2018* | *Hali: Hai* | *Uainishaji wa E&S: F1-2* |

[34] Tovuti ya IFC Project Information Portal, *Coop Bank* (2012) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/31321. Pamoja na mkopo, pesa nyingi za kiasi cha Dola milioni US$ 5 za biashara zilipendekezewa benki, chini ya Programu ya fedha za biashara kimataifa (Global Trade Finance Program) (GTFP). Hata hivyo, uwekezeaji huu hauonekani kama "umeidhinishwa na Bodi.".
[35] Hii ni asilimia 19% ya jumla za fedha za Co-Operative Bank, kwa mujibu wa tangazo la IFC la uwazi wa mradi.
[36] Mikopo: Co-Operative Bank II, Mradi 35393 (Uliidhinishwa : 22 Dec. 2015) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/35393; na Co-Operative Bank III, Mradi 41133 (uliidhinishwa: 27 Machi. 2018) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/41133. Huduma za Ushauri: AMSME Coop Bank, Mradi 601493 (Uliidhinishwa: 11 Okt. 2016) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/AS/601493; DFS Coop Phase 2, Mradi 602467 (Uliidhinishwa 12 Okt. 2017) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/AS/602467.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| *AMSME Coop Bank, Mradi: 601493* | *Huduma ya ushauri* | *Uidhinishaji: Oktoba 11, 2016* | *Hali: Hai* | *Uainishaji wa E&S: F1-2* |
| *DFS Coop, Awamu , Mradi: 602467* | *Huduma ya ushauri* | *Uidhinishaji: Oktoba 12, 2017* | *Hali: Hai* | *Uainishaji wa E&S: F1-2* |

Mikopo ya 2015 a 2018 inaonyesha uwezekano wa uhusiano na kiwanda cha makaa.

- Mradi wa 2015 unahusu mkopo mkubwa wa Dola (US$) milioni 105 ili "kuiwezesha benki iwe na deni la muda mrefu la (i) kuunga mkono madeni ya biashara ndogo ndogo (SME) na vyama vya ushirika… na (ii) kuimarisha ujenzi wa nyumba …"[37] Ijapokuwa maelezi yanaonyesha mkopo umelengwa, hakuna ufafanuzi kuhusu namna fedha hizi zimedhibitiwa ili zisitumike katika shughuli zingine.

- Mradi wa 2018 unahusu mkopo mkubwa wa Dola (US$) milioni 150 kwa Co-Operative Bank ili kuimarisha uwezo wa Benki kwa kutoa ufadhili wa muda mrefu na kuiwezesha kupanua juhudi zake za kutoa madeni miongoni mwa wafanyabiashara wadogo na wa kati (MSMEs) wasiohudumiwa vyema nchini Kenya.[38] Ijapokuwa kwa mara nyingine tena maelezo ya mradi yanataja biashara ndogo ndogo na za kati, hakuna ithibati ya wazi ya udhibiti wa sekta hii.

Huduma za ushauri pia zinaonekana kuwa zitaunga mkono uwezo wa Benki kuhudumia biashara ndogo ndogo na za kati[39] na pia katika kipindi cha mpito ili iwe ya dijitali.[40] Hata hivyo, bila taarifa ya ziada kuhusu huduma zinazotolewa hasa, inawezekana huduma hizi za ushauri zikaimarisha mfumo wa huduma na madeni katika Co-Operative Bank hivi kwamba zinachangia kiwanda cha makaa cha Lamu.

### *3. Co-Operative Bank inaunga mkono kiwanda cha makaa cha Lamu*

Co-Operative Bank inachangia, ama itachangia, maendeleo ya kiwanda cha makaa kwa njia mbili.

Kwanza, mnamo Aprili 2014, baada ya mkopo wa kwanza wa IFC, Co-Operative Bank ilitoa hatifungani ya usalama (dhamana ya mkopaji) kuunga mkono pendekezo la Amu Power la kujenga kiwanda.[41] Hatifungani hiyo, inayoonekana kwamba iko hai, ni bima kwa Kenya Power

[37] Coop Bank II, Mradi 35393 (Uliidhinishwa: Desemba. 22, 2015) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/35393.
[38] Co-Operative Bank III, Mradi 41133 (Uliidhinishwa: 27 Machi. 2018) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/41133.
[39] AMSME Co-op Bank, Mradi 601493 (Uliidhinishwa: Okt. 11, 2016) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/AS/601493.
[40] DFS Coop Phase 2, Mradi 602467 (Mradi: Okt. 12, 2017) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/AS/602467.
[41] Mkataba wa Kununua Umeme (Power Purchase Agreement) kwa ajili ya Kiwanda cha Makaa cha 981.5 Mw baina ya Amu Power and Kenya Power & Lighting (4 Aug. 2017) http://www.decoalonize.org/wp-content/uploads/2018/07/170804.-Amu-Power-KPLC-Power-Purchase-Agreement-lamu-coal.pdf.

of Lighting Company (KPLC) – ambayo imetia saini mkataba wa miaka 25 ili kununua umeme kutoka kwa kiwanda cha Amu Power[42]- endapo Amu Power itashindwa kukifanya kiwanda kuanza kazi kufikia tarehe ya maafikiano.

Pili, ni dhahiri kuwa Co-Operative Bank ina uhusiano uliohai na wa muda mrefu na Centum Investment.[43]

Hivi majuzi, mnamo Aprili 3, 2017, Co-Operative Bank iliwezesha ovadrafti ya Ksh. milioni 981.1 inayoweza kutolewa upya kila mwaka.[44] Katika Ripoti ya Centum ya Mwaka wa 2018, overdraft hiyo ilikuwa bado ipo na thamani yake ilikuwa imepanda na kufikia takribani Ksh. bilioni 1.5.[45]

Ripoti ya Centum ya Mwaka wa 2017 pia inaonyesha fedha zilizotengwa na zilizokuwa zimetolewa na Co-Operative Bank za kiasi cha takribani Ksh milioni 17.8, ambazo ni chache ilinganishwapo na Ksh bilioni 2.3 za 2016.[46] Ripoti ya Mwaka ya 2018 inaonyesha fedha ambazo zilikuwa bado hazijatolewa kuwa ni takribani Ksh milioni 29.[47]

Huduma hizi zote ni za jumla na hii inamaanisha kwamba Centum inaweza kutumia mtaji kama itakavyo, pamoja na kugharamia maendeleo ya kiwanda cha makaa cha Lamu.

Ijapokuwa taarifa za muda za fedha za Centum za 2019 haziorodheshi mikopo yoyote ya benki kutoka Co-Operative Bank kuanzia Septemba 30, 2018 (kutoka takribani Ksh bilioni 1.5 mnamo Machi 2018) taarifa hizi ni za muhtasari na hazina fedha zilizotengwa kama zilizoorodheshwa katika Ripoti Kamili ya Mwaka. Tunaamini kwamba Co-Operative Bank inaendelea kushiriki kwa kuzingatia historia ndefu ya kuipa Centum Investment huduma za fedha.

---

[42] *Id.*

[43] *Tazama*, kwa mfano, Centum Investment, *2017 Annual Report*, p. 6 http://www.centum.co.ke/images/docs/Annual_Report_2017.pdf; Centum Investment, *2016 Annual Report*, p. 3 http://www.centum.co.ke/images/docs/CentumAnnual_Report.pdf; Centum Investment, *2014-2015 Annual Report*, p. 10 http://www.centum.co.ke/images/docs/Annual_Report_2014_2015.pdf.


[44] Centum Investment, *2017 Annual Report*, p. 208.

[45] Centum Investment, *2018 Annual Report*, p. 188 http://www.centum.co.ke/images/docs/CICL_Full_-Annual_Report_FY18.pdf.

[46] Centum Investment, *2017 Annual Report*, pp. 206-207.

[47] Centum Investment, *2018 Annual Report*, p. 187.

**Kielelezo 4: Uhusiano wa IFC na kiwanda cha makaa**



### C. Uwekezaji wa Shirika la Centum ni muhimu kwa maendeleo ya kiwanda cha makaa

Uhusiano wa kifedha baina ya IFC na Centum kupitia Co-Operative Bank na Kenya Commercial Bank, unajidhihirisha kwa kiwango kikubwa katika kiwanda cha makaa kinachopendekezwa Lamu.

Kufikia tarehe ya malalamishi haya, na kwa kadri tunavyofahamu, Centum ina idadi kubwa ya hisa (asilimia 51%) katika Amu Power: Shirika lenye kusudi maalumu la kujenga na kuendesha kiwanda cha makaa. Hata kama GE itapata mtaji katika Amu Power,[48] uwekezaji wa Centum utaendelea kuwa na mtaji mkubwa katika asasi hiyo. Kama mhisa mkubwa, Centum itachanga idadi kubwa ya fedha za kiasi cha Dola (US$) milioni 500 (asilimia 25%) ambazo wanahisa wanatarajiwa kuchanga.[49]

Pia tuna sababu ya kuamini kwamba Afisa Mkuu Mtendaji wa Uwekezaji wa Centum (James Mworia) anahusika kikamilifu katika upangaji na uamuzi kuhusu kiwanda cha makaa. Mara nyingi, James Mworia hutajwa na ripoti za habari kwa kutoa taarifa kuhusu kiwanda cha makaa.[50] Na wakati tulionyesha hofu zetu kuhusu mradi kwa Afisa Mkuu Mtendaji wa Amu Power (Francis Njogu), Bw. Mworia alihuzishwa katika jibu lililotolewa.[51]

Kwa hivyo, ujidhihirishaji wa kifedha katika IFC kupitia uwekezaji wa Centum ni kielelezo cha ujidhihirishaji kihali katika kiwanda cha makaa kinachopendekezwa Lamu na athari zake.

Ni dhahiri kuwa uhusiano wa kifedha unaojulikana baina ya IFC na kiwanda cha makaa kinachopendekezwa Lamu kwa ujumla unaongozwa na uwekezaji wa Centum. Hata hivyo, hili halimaanishi kwamba hakuna uhusiano mwingine wa IFC . Uwekezaji wa kampuni ya Centum ni wa umma; kwa hivyo, Centum huchapisha Ripoti za Mwaka zenye taarifa kuhusu wawekezaji wanaohusika. Mhusika mwengine ni kampuni ya Gulf Energy – na imethibitishwa kushiriki katika mradi huu. Hii ni kampuni ya kibinafsi na haina ruhusa ya kuchapisha hata habari hii chache. Kwa hivyo, muhtasari wa hapo juu kuhusu uhusiano katika IFC haupaswi kuchukuliwa kwamba umekamilika.

---

[48] Kupitia barua, GE imefahamisha Save Lamu kwamba "GE ina fursa ya kupata asilimia 20% ya mtaji katika mradi wa Lamu. Hata hivyo, kabla GE haijawekeza mtaji … haina budi kufanya tathmini ya kina…kabla ya kutafuta uidhinishaji wa ndani ili kuendelea na uwekezaji huu wa mtaji": Barua ya GE to kwa Lamu (19 Feb. 2019) imeambatwa katika Nyongeza 4.

[49] Wasilisho la Amu Power, kwa Tume ya Kenya ya Udhibiti wa Nishati ( Kenya Energy Regulatory Commission) (28 Sept. 2016); Reuters "UPDATE 2-Kenya's Centum to finalise power plant funding this year" (12 Jun. 2018) https://www.reuters.com/article/centum-invt-results/update-2-kenyas-centum-to-finalise-power-plant-funding-this-year-idUSL8N1TF0CF

[50] *Tazama* , kwa mfano, Reuters "UPDATE 2-Kenya's Centum to finalise power plant funding this year" (12 Jun. 2018) https://www.reuters.com/article/centum-invt-results/update-2-kenyas-centum-to-finalise-power-plant-funding-this-year-idUSL8N1TF0CF.

[51] Baruapepe ya Bw. Njogu (Amu Power) kwa Lani Inverarity (kwa niaba ya Save Lamu) (14 Machi. 2016), imeambatwa katika Nyongeza 4. Zingatia kwamba licha ya ahadi ya Bw. Njogu kutoa jibu, hapakawa na jibu lingine.

### D. IFC imekuwa ikijidhihirisha katika kiwanda cha makaa cha Lamu

Uwekezaji wa IFC katika Co-Operative Bank na Kenya Commercial Bank sio uhusiano wa kwanza ambao tumeutambua kati ya IFC na kiwanda cha makaa kinachopendekezwa Lamu.

Mnamo Aprili 2016, Save Lamu iliandikia IFC kuwatahadhirisha kwamba wateja wake wawili wa kifedha wa kati, Kenya Equity Bank Limited na Standard Bank of South Africa, walionekana kuwa wawekezaji katika kiwanda cha makaa.[52] IFC ilijibu mawasiliano hayo ikishauri kuwa Equity Bank ilikuwa imethibitisha kwamba haiwezi kutoa fedha zozote kwa mradi uliopendekezwa wa kiwanda cha makaa, ingawa kitengo chake cha uwekezaji kilikuwa kinatoa huduma za kukusanya fedha.[53] IFC pia ilifafanua kuwa Standard Bank haikuwa tena mteja wao, ingawa haijulikani uhusiano huo ulimalizika lini. Tunaelewa kwamba, kwa wakati mmoja, Standard Bank ilikuwa imepiga hatua ya kupanga fungu la pili la deni ili kutoa fedha kwa ajili ya kiwanda cha makaa cha Lamu.[54] Stanbic Bank, kampuni ndogo ya Standard Bank, inaendelea kutoa huduma za ovadrafti na suhula za mikopo kwa uwekezaji wa Centum, ingawa inaripotiwa kuwa haihusiki tena. Taarifa hii ni kulingana na Ripoti ya hivi karibuni ya kampuni.[55]

Kwa hivyo basi, ni dhahiri kwamba IFC inawekeza - au ishawekeza – kote nchini Kenya na taasisi pana za kifedha ambazo zinafadhili au husaidia vinginevyo kampuni ambazo zinahusika katika maendeleo ya kiwanda cha makaa cha Lamu.

Kutokana na taarifa hii, tunahofia kwamba uwekezaji wa sasa wa IFC katika Co-Operative Bank na Kenya Commercial Bank sio - wala hautakuwa - uhusiano wa kipekee wa IFC katika kiwanda cha makaa cha Lamu, pamoja na hatari kubwa na athari zitakazotokea katika jamii zetu.

### E. Mahusiano Mengine ya World Bank Group

Ili kukamilisha kauli yetu, tunaongezea kwamba Benki ya Dunia (World Bank) inaonekana kuwa imefadhili juhudi za serikali ya Kenya kuendeleza kiwanda cha makaa cha Lamu kupitia mpango wa msaada wa Dola (US$) milioni 40 kugharimia miundombinu.

Mradi wa World Bank wa Fedha za Miundombinu/Ubia Baina ya Mashirika ya Watu Binafsi na ya Umma (*Infrastructure Finance/Public Private Partnership Project -IFPPP*) wa Dola (US$) milioni 40, uliyozinduliwa mwaka wa 2012 na uliopangwa kukamilika mwaka wa 2022, unatarajiwa kuboresha uwezo wa Kenya wa kuvutia ufadhili wa kibinafsi kwa miradi ya miundombinu.[56] IFPPP ina idadi kadha ya vipengele. Kipengele kinachojulikana zaidi ni utaratibu ulioundwa wa Dola (US$) milioni 20 ili kuhakikisha bomba la miradi ya miundombinu

---

[52] Barua ya Save Lamu kwa IFC (8 Apr. 2016), imeambatwa katika Nyongeza 4.
[53] Barua ya IFC kwa Save Lamu (22 Apr. 2016), imeambatwa katika Nyongeza 4.
[54] *Tazama* angalizo 13.
[55] Centum Investment, *2018 Annual Report,* pp. 189-190 http://www.centum.co.ke/images/docs/CICL_Full_-Annual_Report_FY18.pdf.
[56] The World Bank, *Kenya Infrastructure Finance/PPP Project* (Project ID P121019) http://projects.worldbank.org/P121019/kenya-infrastructure-financeppp-project?lang=en&tab=overview.

"kuwa ya thamani."[57] Kupitia kipengele hiki, fedha za World Bank zinatumiwa "kushirikisha washauri wa ufanisi wa shughuli, wanasheria na washauri wengine. Jambo hili ni muhimu kwa kuandaa vizuri miradi ya zabuni kama ubia wa mashirika ya kibinafsi na ya umma (PPP), "ikiwa ni pamoja na" ufadhili wa tathmini ya ulinzi."[58] Vipengele vingine vya programu vimeundwa ili kuboresha uwezo wa serikali kwa jumla kwa madhumuni ya kuvutia uwekezaji wa kibinafsi katika miradi ya miundombinu.

IFPPP inaonekana kuwa imesaidia katika mambo mawili muhimu ya maendeleo ya kiwanda cha makaa cha Lamu. Haya ni kwa mujibu wa ripoti za ufuatiliaji wa mara kwa mara uliotolewa na World Bank na serikali ya Kenya.

Kulingana na Ripoti ya utekelezaji ya Januari 2018, World Bank ilitoa huduma za ushauri wa shughuli ambazo zilifanikisha mashauriano ya mikataba ya ununuzi wa umeme wa kiwanda cha makaa.[59] Mashauriano kuhusu mikataba ya ununuzi wa umeme yangekuwa hatua kubwa katika kuufanya mradi uwe wa thamani. Mapema, mwaka wa 2015, World Bank ilionyesha kufurahi wakati serikali ya Kenya ilifanikiwa kutoa hisa yake kwa kiwanda cha makaa cha Lamu na miradi mingine mitano kama sehemu ya "programu pana ya Kenya ya ubia wa mashirika ya kibinafsi na ya umma (PPP)."[60]

Tunaelewa kuwa mradi huu wa World Bank uko nje ya upeo wa mamlaka ya Afisa Mkuu Mtendaji (CAO). Hata hivyo, tunatoa taarifa hii kwa kuzingatia muktadha: IFC inapaswa kufahamu kwamba Kenya inafuatilia kwa hima mipango ya miundombinu inayojumuisha kiwanda cha makaa cha Lamu na inapaswa kuwajibika kwa hili wakati wa kuzingatia na kufuatilia uwekezaji katika sekta ya kifedha ya Kenya.

## III. Uwekezaji wa IFC unakiuka, au una hatari ya kukiuka Sera ya Uendelevu na Viwango vya Utendaji vya IFC

Uwekezaji mbalimbali wa IFC katika KCB na Co-Operative Bank[61] unategemea Viwango vya 2012 vya Utendakazi vya IFC[62] (IFC PS) pamoja na Sera ya IFC juu ya Uendelevu wa

---

[57] The World Bank, *Integrated Safeguards Data Sheet: Concept Stage for the Kenya Infrastructure Finance/PPP project (P121019)* (8 May 2012) http://documents.worldbank.org/curated/en/853661468752729275/pdf/ISDS0Print0P12008201201336528716007.pdf.

[58] *Id.*

[59] The World Bank, *Kenya Infrastructure Finance/PPP project (P121019): Implementation Status & Results Report* (2 Jan. 2018) http://documents.worldbank.org/curated/en/485711514922420354/pdf/Disclosable-Version-of-the-ISR-Kenya-Infrastructure-Finance-PPP-project-P121019-Sequence-No-10.pdf; The World Bank, *Report of Auditor-General* (30 Jun. 2017), p. 3 http://documents.worldbank.org/curated/en/744861516799074909/pdf/Infrastructure-Finance-and-Public-Private-Partnership-Project-IDA-Cr.pdf.

[60] The World Bank, *Report of Auditor-General* (30 Jun. 2015) http://documents.worldbank.org/curated/en/858931468043510937/pdf/IDA-51570-KE-FY2015-AUDITS.pdf.

[61] Ijapokuwa taarifa ya tovuti ya IFC haifafanui wazi jambo hili, tumechukulia kwamba mkopo wa 2012 ulipewa Co-Operative Bank (Mradi 31321) unapaswa kuzingatia Viwango vya Utendaji (Performance Standards) kwa sababu mkopo huu uliidhinishwa baada ya Viwango vya Utendaji kuanza kutekelezwa..

[62] International Finance Corporation, *Performance Standards on Environmental and Social Sustainability* (1 Jan. 2012), https://www.ifc.org/wps/wcm/connect/115482804a0255db96fbffd1a5d13d27/PS_English_2012_Full-Document.pdf?MOD=AJPERES. [IFC PS]

Mazingira na Jamii[63] (Sera ya IFC ya Uendelevu), na viwango vingine vinavyohusika, kama ilivyoelezwa kwa undani hapo chini. Kwa pamoja, sera hizi zinaagiza Benki za IFC, KCB na Co-Operative Bank kuchukua hatua ili kuepuka, kupunguza na kusimamia hatari za kimazingira na kijamii zitakazosababishwa na kiwanda cha makaa cha Lamu.[64] Na, hatimaye, kama IFC haiwezi kujihakikishia kuwa uwekezaji utazingatia mahitaji ya IFC PS kwa muda uliofaa, basi haitakiwi kutekeleza uwekezaji huo.[65]

Mbali na IFC PS na Sera ya Uendelevu, kanuni na taratibu zifuatazo pia ni muhimu.[66]

- Miongozo ya IFC ya Viwango vya Utenda kazi kuhusu Uendelevu wa Mazingira na Jamii;[67]
- Miongozo ya IFC ya Kutathmini Mazingira na Jamii;[68]
- Miongozo kuhusu Mazingira, Afya na Usalama wa IFC/ World Bank Group (Miongozo ya EHS);[69]
- Miongozo kuhusu Afya na Usalama wa Mazingira katika Viwanda vya Umeme wa Gesi;[70]
- Maelekezo ya Sekta ya Nishati ya World Bank Group (ambayo inazuia msaada wa kifedha kwa miradi ya uzalishaji wa umeme wa makaa kwa kiasi, kwa sababu ya athari za kimazingira na kijamii)[71] na "vigezo vya kuchunguza miradi ya makaa chini ya Mfumo wa Mkakati wa Maendeleo na Mabadiliko ya Hali ya Anga."[72]

Kama inavyoelezwa hapa chini, licha ya hatua ya mwanzo ya mradi huu, ukiukaji wa sera hizi tayari umetokea. Kutokana na hali kuwa hatari za mradi huu ni za kina na kwamba hatua

[63] International Finance Corporation, *Policy on Environmental and Social Sustainability* (1 Jan. 2012) https://www.ifc.org/wps/wcm/connect/7540778049a792dcb87efaa8c6a8312a/SP_English_2012.pdf?MOD=AJPERES. [Sustainability Policy]

[64] *Tazama,* pamoja na kanuni zingine, Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy) aya ya. 33-37.

[65] Sustainability Policy, para. 22.

[66] Tathmini ya ridhaa ya CAO inahusisha sera zote za IFC/MIGA pamoja na Viwango vya Utendaji, kanuni, taratibu, na mahitaji na ukiukaji wake unaweza kusababibisa matokeo makubwa ya kimazingira na kijamii. procedures, and requirements: Operational Guidelines, aya. 4.3.

[67] IFC *International Finance Corporation's Guidance Notes: Performance Standards on Environmental and Social Sustainability* (1 Jan. 2012). https://www.ifc.org/wps/wcm/connect/e280ef804a0256609709ffd1a5d13d27/GN_English_2012_Full-Document.pdf?MOD=AJPERES.

[68] IFC Environment, Social and Governance Department *Environmental and Social Review Procedures Manual* https://www.ifc.org/wps/wcm/connect/d0db8c41-cfb0-45e9-b66a-522c88f270a5/ESRP_Oct2016.pdf?MOD=AJPERES.

[69] IFC / World Bank Group *Environmental, Health, and Safety General Guidelines* (30 Apr. 2007) https://www.ifc.org/wps/wcm/connect/554e8d80488658e4b76af76a6515bb18/Final%2B-%2BGeneral%2BEHS%2BGuidelines.pdf?MOD=AJPERES

[70] IFC / World Bank Group *Environmental, Health, and Safety Guidelines for Thermal Power Plants* (19 Dec. 2008) https://www.ifc.org/wps/wcm/connect/dfb6a60048855a21852cd76a6515bb18/FINAL_Thermal%2BPower.pdf?MOD=AJPERES&id=1323162579734. Note that a revision process is underway: IFC / World Bank Group *Environmental, Health, and Safety Guidelines for Thermal Power Plants* (draft revised version) (Jun. 2017) https://www.ifc.org/wps/wcm/connect/9a362534-bd1b-4f3a-9b42-a870e9b208a8/Thermal+Power+Guideline+2017+clean.pdf?MOD=AJPERES.

[71] "Toward a Sustainable Energy Future for All: Directions for the World Bank Group's Energy Sector" (2013) http://documents.worldbank.org/curated/en/745601468160524040/pdf/795970SST0SecM00box377380B00PUBLIC0.pdf.

[72] World Bank Group *Operational Guidance for World Bank Group Staff Criteria for Screening Coal Projects under the Strategic Framework for Development and Climate Change* (Mar. 2010) http://siteresources.worldbank.org/EXTENERGY2/Resources/CGN_20100331.pdf.

zilizopendekezwa za kupunguza makali hazitoshi, asasii hizi haziwezi kuunga mkono kiwanda cha makaa cha Lamu bila kukiuka sera hizi. Kwa hivyo, IFC inapaswa kuchukua hatua za haraka ili kuzuia ushiriki wa wateja wake katika mradi huu.

### A. Washiriki wa kifedha hawazingatii viwango vya IFC PS, na IFC hailindi na kusimamia wajibu huu ipasavyo

Sera ya IFC na ya Uendelevu inalazimisha majukumu muhimu ili kupunguza hatari za kimazingira na kijamii (E & S) katika kila ngazi ya mpangilio wa uwekezaji kati ya IFC na kiwanda cha makaa cha Lamu. Kutokana na upungufu wa uchunguzi wa kina wa E&S hadi sasa – inavyodokezwa kwa kina hapa chini – mpango wa kupunguza makali wa E&S uliopo kwenye tovuti ya mradi wa IFC hauna uwazi wala umakinifu. Hauonyeshi kwamba IFC na wateja wake wanazingatia uwajibikaji huo.

Kwa upande wake, IFC inapaswa kufanya uchunguzi wa kina kuhusu mazingira na jamii kabla ya kutafuta idhini ya uwekezaji wowote ili kujihakikishia uzingatiaji wa malengo ya IFC PS katika uwekezaji na matokeo yake - yaani, kuthibitisha kwamba mradi hautazua hatari zisizofaa na zisizokubaliwa ama kudhuru mazingira au jamii.[73] IFC inapaswa kufadhili tu shughuli za uwekezaji zinazotarajiwa kufikia mahitaji ya IFC PS kwa kipindi cha muda ufaao.[74] Uchunguzi huu wa kina ni pamoja na kuchunguza tathmini za mteja kuhusu hatari za kimazingira na kijamii na kuhakikisha kuwa hatari hizi zinatambuliwa ipasavyo na mna mipango mwafaka ya kuzipunguza. Katika hali ya uwekezaji wa kifedha kupitia mashirika ya kati (FI), IFC inapaswa kutathmini jumla ya fedha za mashirika hayo na shughuli za kibiashara za wateja wake wa kati . Lengo la tathmini ni kutambua namna shughuli za biashara za mashirika haya ya kati (FI), na kwa hivyo za IFC, zinavyoweza kuhatarishwa na uwekezaji wake. Hapo itabidi pawe na ufafanuzi wa mahitaji ya kudhibiti hatari hizi. IFC inapaswa pia kuchunguza uwezo wa mashirika haya ya kati (FI) kutekeleza mradi pamoja na mfumo wao wa kusimamia hatari za kijamii na kimazingira.[75]

IFC inapaswa kuanzisha masharti yafaayo ya kulinda mazingira na jamii katika mikataba yake ya uwekezaji na wateja wake. Masharti haya ni pamoja na kuzingatia mahitaji ya IFC PS na masharti maalumu yaliyojumuishwa katika mipango ya utekelezaji, pamoja na masharti mwafaka ya taarifa za mazingira na kijamii, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya mabadiliko yoyote ya kihali ambayo yanaweza kusababisha hatari na kuathiri mazingira na jamii.[76]

---

[73] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 7, 20-21.
[74] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 22.
[75] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 34.
[76] Wateja sharti waifahamishe IFC kila panapotokea mabadiliko katika biashara zao au wanapotaka kuingia katika eneo mpya la biashara ambalo ni tofauti na lile lililowasilishwa ili kuidhinishwa na Bodi. Katika hali hiyo, IFC itatathmini kama eneo mpya la biashara linahatarisha mazingira na/au jamii na athari zake, na kama ndivyo IFC itahitaji mteja abadilishe Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (.Environmental and Social Management System (ESMS)) kwa njia inayoafikiana na hatari na/au athari hizo.: Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya 25.

Baada ya hayo, IFC haina budi kuwa na ufuatiliaji wa mara kwa mara na kusimamia wawekezaji wake.[77] Usimamizi wa IFC unaweza kuhusisha ziara kwa wapokeaji wa mikopo/uwekezeji katika mashirika ya kati (FI) hasa katika miradi midogo yenye hatari kubwa.[78] Ikiwa IFC itagundua kuwa mteja hawezi kuzingatia sera hizo, IFC inapaswa kufanya kazi na mteja huyo ili aweze kuzingatia sera za utendakazi. Na kama mteja atashindwa kufuata sera, IFC itachukua hatua za haki za uzuilifu wa makali kama itakikanavyo.[79]

Tovuti ya Taarifa ya Mradi wa IFC haitoi uhakika kwamba uchunguzi huu wa kina na uwajibikaji wa usimamizi unafikiwa. Chini ya kichwa cha E & S "Hatua za Kupunguza Makali/ ESAP", kwa kila mojawapo ya miradi muhimu iliyojadiliwa hapo juu, IFC inachapisha tu taarifa isiyo makinifu inayohitaji "wateja wake ambao ni washiriki wa kati wa kifedha wanaozingatia Viwango vya Utendaji ... kuunda Mifumo ya Mawasiliano ya Nje ili kupokea na kutathmini maswali au malalamiko kutoka kwa chama chochote chenye nia kuhusu hatari za E & S na athari za shughuli zao."[80]

Taarifa hii isiyo makinifu - inarejelea tu kuwepo kwa utaratibu wa malalamiko – na haiafikiani kabisa na hatua za za E & S za kupunguza makali zilizowekwa na IFC PS kwa wateja wake wa kifedha wa kati. Kama wateja wa IFC, KCB na Co-Operative Bank lazima:

- Zifanye uchunguzi wa kina wa E & S kwa shughuli za kibinafsi;[81]
- Ziwe na mifumo ya usimamizi kuhusu hatari za E & S inayofuata kanuni zilizomo katika IFC PS 1;[82]
- Zizingatie orodha iliyotengwa ya IFC na kufuata sheria za kitaifa zinazohusika;[83]
- Zihakikishe kwamba shughuli za kibiashara wanazounga mkono na zenye hatari zinazingatia mahitaji ya IFC PS (mahitaji hayo yatajadiliwa kwa kina katika sehemu nyingine hapo chini).[84] Shughuli yoyote ya uwekezaji inayohusiana na Amu Power inahitaji kuzingatia hili. Zaidi ya hayo, kutokana na jukumu muhimu la uwekezaji wa Centum katika maendeleo ya kiwanda cha makaa cha Lamu kama mhisa mkuu wa Amu Power, msaada wowote wa kifedha kwa Centum ambao unaweza kushirikishwa kwa

---

[77] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 45.

[78] *Id*.

[79] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 24.

[80] *Kenya Commercial Bank* (2013) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/32805; *Kenya Commercial Bank Limited* (2016). https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/36791; *Coop Bank* (2012) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/31321; Mikopo: Co-Operative Bank II, Miradi 35393 (Desemba: 22 Desemba. 2015) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/35393; *Co-Operative Bank III* (2018) https://disclosures.ifc.org/#/projectDetail/SII/41133.

[81] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 33 na 35: Usimamizi wa mazingira na hatari za kijamii ni sehemu muhimu sana ya majukumu ya wateja wa kati wa fedha (FI). Sera za IFC zinaagiza wateja wa kati wa fedha kutathmini na kufuatilia biashara zao na pia usimamizi wa jumla ya fedha kwa mujibu way ale yafahamikayo kuhusu hatari kwa kimazingira na kijamii ya shughuli na biashara zao.

[82] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 35; IFC PS 1, aya. 1, 5-6.

[83] *Id*.

[84] *Id*. Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 35 inaeleza wazi kwamba: explicitly provides: "Wateja wa kati (FI) wenye jumla ya biashara na/au shughuli za kibiashara zenye uwezekano wa hatari kubwa au ya wastani juu ya mazingira au jamii (yaani kiwango cha F1-2) wanahitaji shughuli hatari za kibiashara wanazoziunga mkono zifuate Kanuni za Viwango vya Utendaji zinazofaa." Uwekezaji wa IFC kwa KCB na Cooperative Bank ni wa kiwango cha F1-2.

maendeleo ya Lamu (ikiwa ni pamoja na jumla ya mitaji) pia utakuwa uwekezaji wenye hatari mkubwa;

- Zifuatilie shughuli hizo za kibiashara ili kuhakikisha kulindwa kwa mazingira na jamii.[85]

Katika hali ambapo IFC inayapa mashirika ya kati (FI) mtaji au msaada wa kifedha kwa kusudi la jumla, bila mpaka wa matumizi ya mwisho, mahitaji haya yatatumika kwa jumla ya fedha zote za FI tangu wakati IFC ilipokuwa mhisa au mwekezaji.[86]

Hakuna taarifa iliyowekwa wazi na IFC au wateja wake, KCB au Co-Operative Bank, kwamba mashirika haya yanachukua hatua maalumu ili kuhakikisha kwamba Kampuni za Centum na Amu Power zinafanya uchunguzi mpana na wa kina kuhusu kupunguza makali kwa E&S, kwa mujibu wa viwango vya IFC PS. Kinyume chake, kama tunavyoeleza hapa chini, ingawa Amu Power inadai kuwa inazingatia viwango vya IFC PS,[87] ni wazi kwamba viwango hivi tayari vimevunjwa. Tunahofu kwamba ukiukaji huu utakuwa mbaya zaidi wakati mradi utakapokuwa unaendelea.

### B. Tathmini ya athari hadi sasa inapuuza vipengele muhimu vya mradi

Tathmini ya kina kuhusu athari iliyotolewa hadi sasa ni ya kimanzingira na kijamii iitwayo '*Environmental and Social Impact Assessment Study'* na iliyotayarishwa na *Kurrent Technologies for Amu Power*, mnamo tarehe 10 Julai 2016 (2016 ESIA).[88] Tathmini hii ilifuata Ripoti ya Mradi wa Mazingira (EPR), iliyokuwa waraka wa upeo wa ESIA, mnamo Septemba 2015.[89] Tathmini hizi za EPR na ESIA, hata hivyo, zina upungufu wa kina na hazibainishi hatari kubwa zinazotokana na ujenzi wa kiwanda cha umeme wa makaa katika eneo hili lenye utamaduni na ekolojia yenye thamani kubwa.

Tathmini ya ESIA ya 2016 kuhusu makali na athari za kijamii na kimazingira haijakamilika kwa sababu haikuchunguza athari za vipengele mbalimbali vya mradi na huduma zinazohusika. Hasa ESIA haina taarifa yoyote ya kimsingi kuhusu uchimbaji wa makaa na usafirishaji ikiwa ni pamoja na mfumo wa kusafirisha makaa wa kilomita 15, shughuli za uchimbaji wa chokaa, na barabara ya kufikia eneo hilo la kilomita 9.

Kama ilivyojadiliwa Benki za KCB na Co-Operative, kama wateja wa IFC, zinahitajika kuzingatia viwango vya IFC PS. Zaidi ya hayo, benki hizi zinapaswa kuhakikisha uzingatiaji wa viwango vya IFC PS miongoni mwa shughuli za kibiashara zenye hatari na ambazo zinaziunga mkono - ikiwa ni pamoja na shughuli za Amu Power na Uwekezaji wa Centum katika maendeleo ya kiwanda cha makaa Lamu.[90]

---

[85] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 33.
[86] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 37.
[87] Kurrent Technologies *Environment and Social Impact Assessment (ESIA) Study for the Proposed 1,050MW Coal Fired Power Plant Project, Kenya* (Jul. 16, 2016), Sura 2.6 https://www.amupower.co.ke/esia.html. [2016 ESIA]
[88] *Id.*
[89] Kurrent Technologies *Environment Project Report Study for the Proposed 1050MW Coal Power Plant, Lamu County, Kenya* (Sept. 2015) http://www.decoalonize.org/wp-content/uploads/2017/03/Coal-Plant-EPR-1.pdf.
[90] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 35.

Mahitaji ya kimsingi ya IFC PS ni utambuzi wa kina (na wa mapema) wa "yote" yanayoweza kuhatarisha mazingira na jamii kutokana na "athari" za "mradi", ili taarifa sahihi ya kimsingi iweze kukusanywa na hivyo athari halisi kupunguzwa na kufuatiliwa. IFC PS 1 inahitaji kwamba mteja aanzishe na adumishe mchakato wa kutambua makali ya E & S na athari za "mradi".[91] Mradi huo" unafafanuliwa kama "*seti iliyoelezwa ya shughuli za kibiashara, ikiwa ni pamoja na vitu maalumu vya kimaumbile, vipengele, na vifaa ambavyo vinaweza kusababisha makali na athari na bado havijabainishwa"* (msisitizo wetu).[92] Uchunguzi wa kina wa E & S hauna budi "kuzingatia hatari na athari za kimazingira na kijamii zinazotokana *na mradi*" (msisitizo wetu).[93]

Kuhusu maendeleo ya kiwanda cha umeme wa makaa ambacho kinaweza kuleta athari kubwa za kimazingira au kijamii – kigezo ambacho kimefikiwa na kiwanda cha makaa Lamu - IFC PS inahitaji "ESIA" kutambua na kutathmini kikamilifu hatari na athari hizo.[94]

Pia tathmini hizo za hatari na athari lazima zifikie "eneo zima la kuathirika" na mradi. Yaani:[95]

- Eneo la uwezekano wa kuathiriwa na: (i) mradi na shughuli za mteja na vifaa ambavyo vinamilikiwa moja kwa moja, vinavyoendeshwa au kusimamiwa (ikiwa ni pamoja na makandarasi) na ambavyo ni vipengele vya mradi huo; (ii) athari kutokana na maendeleo yasiyopangwa lakini yanayotabirika na yanayosababishwa na mradi ambao unaweza kutokea baadaye au mahali tofauti; au (iii) athari za mradi zisizo za moja kwa moja juu ya uanuwai wa viumbe hai au kwenye mfumo wa ekolojia unaotegemewa kwa ajili ya riziki za jamii zinazoathiriwa;
- Vifaa vya ushirika, ambavyo ni vifaa visivyofadhiliwa kama sehemu ya mradi na havingejengwa au kupanuliwa kama mradi haungekuwepo na bila vifaa hivyo, mradi huo haungewezekana; na
- Athari za jumla (zinazojadiliwa zaidi katika kifungu cha III.I hapo chini).

Ikiwa rasilmali itakayoundwa, itakayotwaliwa ama itakayofadhiliwa bado haijatambuliwa, mteja anapaswa kuhifadhi uanzishwaji wa mchakato wa kutathmini mazingira na jamii kwa kina ili kuhakikisha kwamba hatari na athari zitatambuliwa wakati fulani baada ya kuelewa vyema vipengele maalumu, rasilmali na vifaa.[96]

Mchakato huu wa kutambua hatari ni msingi wa maendeleo ya taratibu za kupunguza makali, usimamizi na mipango ambayo ni muhimu kuhakikisha kuwa hatari za E & S zinazotokana na mradi zitaepukwa au kushughulikiwa.[97]

---

[91] IFC PS 1, aya. 7. Kama ilivyofafanuliwa kwa kina hapo chini, katika Sehemu ya III.E-III.G, ESIA ilikosa kufafanua vyema upeo wa "mradi" na haikufaulu kushughulikia athari zinazohusu watu kuhamishwa, jamii asilia na turathi za kitamaduni.
[92] IFC PS 1, aya. 4
[93] IFC PS 1, aya. 7.
[94] IFC PS 1, angalizo 11; Angalizo la Mwongozo 1, GN23. Hatua muhimu za mchakato wa ESIA kwa jumla ni: (i) Upitiaji wa mradi na kuchunguza hali ya tathmini ; (ii) kutathmini njia mbadala; (iii) kutambua wadau (kwa kuzingatia wanaoathirika moja kwa moja) na kukusanya data ya awali ya kimazingira na kijamii; (iv) kutambua athari, kutabiri, na kuchanganua ; (v) kubuni hatua za kupunguza makali au usimamizi; (vi) umuhimu wa athari na tathmini za athari zilizobaki; na (vii) uwekaji nyaraka za mchakato wa tathmini ( ripoti ya ESIA): Angalizo la Mwongozo (Guidance Note) 1, GN23.
[95] IFC PS 1, aya. 8; Angalizo la Mwongozo( Guidance Note) 1, GN21.
[96] IFC PS 1, aya. 7; Angalizo la Mwongozo (Guidance Note) 1, GN30 and GN60.
[97] IFC PS 1, aya. 13-16.

Katika hali hiyo, ili kuzingatia masharti ya IFC PS, mashirika ya kati lazima yawe yameelewa hatari zitakazotokana na msaada wa kifedha kwa maendeleo ya kiwanda cha makaa cha Lamu, kama sehemu ya shughuli za kibiashara, na kufanya kazi na wateja wao (Amu Power na Uwekezaji wa Centum) ili kupunguza na kusimamia makali yanayotokana na kiwanda hicho cha makaa kwa mujibu wa IFC PS.


Kwa upande wao, Amu Power na Uwekezaji wa Centum wanatakiwa na IFC PS kutambua vizuri makali na kutathmini madhara yatakayotokana na mradi wa kiwanda cha makaa cha Lamu katika "sehemu zote zitakazoathiriwa", ikiwa ni pamoja na maendeleo yoyote makubwa katika mipango ya mradi huo.[98] Tathmini za E&S hadi sasa hazijafikia viwango hivyo, kwa sababu zinashindwa kushughulikia sehemu muhimu za mradi.

1. *Uchimbaji wa makaa na mfumo wa usafirishaji*

ESIA inaorodhesha mfumo wa uhawilishaji makaa kama mojawapo ya "vipengele muhimu" vya mradi uliopendekezwa, lakini haitambui au kutathmini athari zake. Vile vile, mfumo wa uhawilishaji wa makaa haukuzingatiwa katika tafiti za awali zinazoweka msingi wa ESIA, kama vile EPR au Mabadiliko ya Hali ya Anga na tafiti za GHG za Moshi.[99]

**Mchoro wa 5: Upokeaji makaa na njia ya uhawilishaji ya karibu**.

[98] 2016 ESIA, Sura 1: Muhtasari, §1.3.
[99] *Tazama* 2016 ESIA, Nyongeza 4: Climate Change and GHG Emissions Study, §4.4: Overview of Lamu Power Plant Emission Causing Activities.




*Rejeleo: 2016 ESIA, Sura ya 4, Kielelezo: 4-2, §4.6.1.2.*

Mfumo wa uhawilishaji wa makaa utajengwa kwa madhumuni ya kipekee ya kusafirisha makaa kwenye eneo la mradi na itaendelezwa na kudhibitiwa na mwendesha mradi, Amu Power.

ESIA inafafanua kwa kifupi mfumo wa uhawilishaji wa makaa wa kilomita 15 na minara ambayo itaunganisha eneo la maegesho ya kupokea makaa katika bandari ya Kililana kuelekea

yadi ya makaa kwenye eneo la mradi,[100] halafu inajaribu kueleza kwa nini haikuhusisha tathmini yoyote ya athari kwa kusema kuwa “muundo wa mfumo wa uhawilishaji makaa kwa sasa uko katika awamu ya kuundwa na haukuwepo wakati wa kufanya utafiti huu wa ESIA. Kwa hivyo, hakuna athari za mazingira na kijamii ambazo zimegunduliwa au kutathminiwa."[101] Hata hivyo, ingawa mfumo wa uhawilishaji ulikuwa bado upo katika awamu ya kuundwa,na unaweza kuwa umezuia kwa kiasi fulani uwezo wa ESIA kujadili athari zake kwa namna iliyo sahihi, hakuna sababu yoyote kwa ESIA kushindwa kufanya jaribio lolote la kukadiria athari zake kwa kuzingatia aina za athari ambazo mtu anaweza kutarajia kwamba zitatokea kutokana na mfumo huo wa uhawilishaji. Ramani inayojumuishwa katika ESIA (angalia Kielelezo 5) inaonyesha kuwa mipango imekamilika kwa kiasi kikubwa hivi kwamba njia ya mfumo wa uhawilishaji wa makaa imejulikana kwa kiasi fulani.

Kama ilivyojadiliwa hapo juu, IFC PS 1 inaagiza kwamba madhara yatambuliwe na yatathminiwe kwa kuzingatia vipengele vyote vya mradi "vilivyotambuliwa kimakusudi", hali na vifaa; haihitaji kwamba miundo ya mwisho iwepo kabla ya tathmini yoyote ya athari kufanywa.[102]

Mfumo wa uhawilishaji wa makaa ni sehemu muhimu ya mradi; umetambuliwa kimakusudi, na ni eneo la athari katika mradi . Kwa hivyo, mfumo huu ungekuwa umejumuishwa katika tathmini ya ESIA kuhusu athari za mradi.

ESIA haijatoa maelezo kuhusu mchakato wowote wa uchunguzi wa kina uliotarajiwa kwa ajili ya kutathmini athari za vipengele vya mradi huu mara tu muundo wa mwisho utakapotambuliwa.[103] Tangu ESIA itolewe kwa umma zaidi ya miaka miwili iliyopita, hakuna tathmini ya ziada iliyochapishwa na watu wa eneo hilo hawana habari ya uwezekano wa athari za mfumo wa uhawilishaji wa makaa.

Mwisho, ESIA haielezi kwa kina kuhusu mchakato wa uchimbaji na usafirishaji wa makaa kabla ya mfumo wa uhawilishaji. Badala yake inadokeza kwamba, kwa kurejelea utafiti fulani, “usafirishaji wa makaa unatarajiwa kufanyika kutoka kwa makampuni makubwa ya uchimbaji nchini Afrika Kusini na Msumbiji, kupitia meli au reli."[104] Ukosefu huu wa taarifa ya kina unazuia tathmini ya maana ya athari na uchambuzi mbadala kuhusiana na upatikanaji wa makaa na usafirishaji wake.

### 2. *Barabara ya kufikia eneo la Mradi*

Mbali na mfumo wa uhawilishaji makaa , barabara ya kufikia eneo la mradi inajengwa ili kukabiliana na msongamano wowote. Ingawa barabara ya kufikia eneo la mradi inajengwa na Wizara ya Usafiri, ni wazi kuwa ni sehemu ya mradi wa makaa kwa lengo la IFC PS.

---

[100] 2016 ESIA, Sura 1, §1.3.
[101] 2016 ESIA, Sura 4: Maelezo kuhusu mradi, §4.6.1.2.
[102] IFC PS 1, aya. 8.
[103] Kinyume na IFC PS 1, aya. 7.
[104] 2016 ESIA, Sura 4 Maelezo kuhusu mradi,, §4.6.1.1.

Zaidi ya wakulima 109 wa eneo hili na familia zao, pamoja na WaBajuni, WaAweer na WaGiriama, tayari wamehamishwa kutoka makao yao ili kujenga barabara hii ya kufikia eneo la mradi . Pia wamepoteza nyumba na makazi yao ya muda. Kwa vile kilimo ni cha msimu, wengi wa wakulima hao - wengi wao wanaoishi kisiwa cha Pate wakati usiokuwa wa msimu - hawakuwepo wakati ardhi yao ikiharibiwa. Wakulima hawa hawakushauriwa , au kufidiwa kutokana na athari za barabara. Mmoja wa wakulima hao anaelezea:[105]

> *"Katika makazi yangu, miti ya korosho ilikatwa kwa ajili ya barabara, wakati nilikuwa mbali. Katika shamba langu, barabara imepita katikati yake. Sikuwa karibu. Haukuwa wakati wa msimu. kama ningekuwepo, ningejitahidi kupinga kwa nguvu kuzuia kitendo hicho. Badala yake, nilirudi shambani mwangu na kushuhudia kile kilichotokea. Miti yangu ya korosho ilikatwa kwa ajili ya barabara. ... Walikuja na mashine. Walikuja hapa na wakaharibu miti yetu. Sikushauriwa kamwe. Hadi sasa, sijafahamishwa habari yoyote kamwe. Hakuna aina yoyote ya mawasiliano. Tuko hapa. Hili limeniacha nashangaa; je, sisi ni nyani, wanyama, au sisi ni wanadamu? Ingekuwa bora kuwa mnyama kuliko kutendewa hivi.* "

Kama ilivyojadiliwa zaidi katika sehemu ya hapa chini, wasiwasi huu kuhusu kiwango cha uhamisho na ikiwa wakulima watapewa fidia umesababisha jamii hizi kuwa katika hali ya kuhatarishwa zaidi. Baadhi ya wakulima wameacha kushughulikia ardhi iliyokaribu na eneo la mradi, ingawa ni msimu wa maandalizi, kwa sababu wanaogopa uharibifu zaidi wa mazao yao. Wahuni wamechukua fursa hiyo kudai ardhi ambayo imeachwa na wakazi kwa matumaini kwamba watapata fidia (wamiliki / watumiaji halali watahamishwa zaidi).

> *Ukosefu wa uhakika kuhusu mahali [barabara ya kufikia eneo la mradi] itafika, na ardhi gani itakayochukuliwa baadaye, huathiri sio tu wakulima ambao tayari wamehamishwa, lakini pia kila mtu aliye karibu na eneo hilo. Hakuna mtu anayejua nani atakayefuata, wala kile kitakachotokea. Waendelezaji mradi hufanya chochote wanachotaka; hakuna mashauriano, wala taarifa. Na wakulima hawa wako nje ya eneo la mradi [mpaka wa kiwanda cha makaa] - ardhi yao haikupaswa kuathiriwa na kiwanda cha makaa. Basi ikiwa wamehamishwa na ardhi yao imeharibiwa, ni nani atakayefuata? "*

Wakulima walijipanga kama Kwasasi Mvunjeni Farmers Self-Help Group na wamekuwa wakitoa malalamishi yao kwa Serikali ya Kenya tangu 2018. Hadi leo, hakuna mashauriano yaliyofanywa wala fidia kutolewa kwao.[106]

ESIA ya 2016 inapuuza kipengele hiki cha mradi. Inasema hivi: "Athari za kimazingira na kijamii zitokanazo na barabara ya kufikia mradi itazingatiwa wakati uteuzi wa njia utakuwa umeamuliwa na Leseni Mbadala ya EIA itatumika."[107] Huku ni kukiuka mahitaji ya kutathmini

---

[105] *Tazama pia* Barua ya from Kwasasi Farmers Self Help Group kwa Wizara ya Usafiri (31 Aug. 2018) iliyoambatwa katika Nyongeza 4.

[106] Barua ya Kwasasi Farmers Self Help Group kwa Mwenyekiti, Tume ya Kitaifa ya Ardhi (National Land Commission (13 Jan. 2019) iliyoambatwa katika Nyongeza 4.

[107] 2016 ESIA, Sura 4, §4.7.1.

athari ya kipengele hiki cha mradi baada ya "kueleweka vizuri."[108] Hatuna ufahamu wowote wa tathmini mbadala ya athari, wala tofauti yoyote katika Leseni ya EIA, kwa ajili ya barabara hii. Isitoshe, hatujui  Leseni yoyote tofauti ya EIA, inayoruhusu barabara hii. Wakati huo huo, wakulima waliohamishwa wameachwa katika hali mbaya ya uhaba wa chakula na fedha, bila kulipwa fidia au mashauriano. Mambo haya ni ukiukaji mkubwa wa IFC PS 5 (habari hii imejadiliwa kando katika kifungu cha III.E hapo chini).

### 3. *Uchimbaji wa chokaa katika Witu*

Vile vile, ESIA haitathmini athari za uchimbaji wa chokaa katika Witu, wala usafirishaji wa chokaa hiyo kupitia ardhi na bahari hadi kiwanda cha umeme. ESIA inaonyesha wazi kuwa uchimbaji wa chokaa utakuwa shughuli muhimu ya mradi huo.[109] Mfumo wa kupokea chokaa na mfumo wa kushughulikia jasi ni vipengele vya mradi vilivyoorodheshwa kuwa ni muhimu, lakini ESIA haina ufafanuzi wowote wa shughuli za uchimbaji  wa chokaa, athari zake, au mipango iliyopo ya kupunguza makali.[110] Shughuli za uchimbaji chokaa mara nyingi zinahusishwa na athari kubwa, ikiwa ni pamoja na athari za vumbi na kelele na uwezo wa mabadiliko ya maji ya chini ya ardhi ya eneo hilo.

Witu ni eneo litakaloathirika wakati wa shughuli hiyo. Ni makazi ya Hifadhi ya Msitu wa Witu, makazi muhimu ya uanuwai wa viumbe,[111] pamoja na Tana River Delta, na mkondo wa maji yake ya kudumu na ya msimu. Witu pia ni sehemu ya jadi ya malisho ya WaOrma .[112] Aidha, tuna wasiwasi juu ya athari zitakazotokana na usafirishaji wa chokaa mijini na miongoni mwa jamii zilizoko katika njia ya usafirishaji.

Athari za uchimbaji wa chokaa za E&S katika Witu na usafirishaji wake kutoka Witu hadi kwenye kiwanda cha umeme zingepaswa kutambuliwa mapema, kutathminiwa  na kujulikana vizuri na watu walioathirika katika duru ya  mradi. ESIA 2016 haitoi sababu yoyote ya kutofanikisha hili, wala haitambui uchimbaji wa chokaa kama shughuli itakayofanyika na shirika la kati au kuchukuliwa kama athari za kijumla.

### 4. *Mkataba wa General Electric (GE) – Teknolojia ya hali ya juu zaidi*

Kwa muda wa takribani miaka miwili baada ya ESIA ya 2016 kuchapishwa Centum, Amu Power na GE walitangaza kwamba GE ingetoa teknolojia ya hali ya juu zaidi (USC) kwa ajili ya kiwanda cha  makaa cha  Lamu. Kwa mujibu wa habari nyingi zilizotolewa na vyombo vya

---

[108] IFC PS 1, Sura. 8.

[109] Kibali cha ekari 2,000 kilitolewa na Baraza la Kaunti (labda kwa Amu Power) kwa ajili ya uchimbaji wa makaa katika Witu: ESIA ya 2016 Sura  4, §4.2. Tazama pia  §4.3, inayoelezea umuhmu wa chokaa katika mfumo ya dohani wa kutoa salfa.

[110] Katika kujadili athari za jumla magari na usafiri, ESIA ya 2016 inataja athari zinazoweza kutokea za usafarishaji wa chokaa "kutoka matimbo yaliyotambulika" hadi katika kiwanda cha makaa. ESIA ya 2016 Sura 19: Tathmini ya Athari kwa Jumla (Cumulative Impact Assessment), §10.3.14.  Hata hivyo athari za uchimbaji makaa hazijatambuliwa wala kujadiliwa.

[111] Lamu County Spatial Plan (2016-2026) Ripoti ya Mwisho (Juzuu I, Mei 2017) §4.3.1.2.

[112] BCP, §4.2 na kama ilivyojadiliwa zaidi katika Sehemu ya 111.F hapo chini.

habari, kampuni ya GE Power iliweka saini mkataba na Kampuni ya Gulf Energy, mmoja wa wanahisa wakuu katika Amu Power, ili kutoa "vipengele safi vya kiteknoloji ya hali ya juu zaidi ya makaa (boila na jenereta ya mvuke) na mfumo wa kudhibiti hewa safi kwa kiwanda cha makaa ya umeme cha Lamu, " na pia kutoa fursa ili GE iweze kupata hisa katika mradi huo.[113] Kufuatia tangazo hilo, hakujawa na ufafanuzi au madhibitisho zaidi kuhusu mpango huu.[114]

Kutokana na habari mbali mbali , Amu Power na wawekezaji wake wanasisitiza kuwa teknolojia hii ya USC itapunguza makali ya athari za E&S katika kiwanda cha makaa cha Lamu kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na teknolojia ya hali ya juu iliyotathminiwa katika ESIA 2016.[115] Hata hivyo, hawajachapisha tathmini yoyote ya E&S ili kuunga mkono taarifa hizo. Inaonekana kuwa kipengele muhimu cha mradi kilibadilishwa bila kutolewa kwa tathmini zozote sahihi za E&S wala mipango ya kupunguza uchafuzi. Kitendo hiki ni dhihirisho la mara kwa mara kuwa mna ukosefu wa ushauriano na wa uchunguzi wa kina katika maendeleo ya mradi huu. Aidha, kauli kwamba hofu za E&S zitasuluhishwa pakubwa kupitia teknolojia mpya, kimsingi zinapotosha na si sahihi.Ni kweli kwamba viwanda vya USC vinachukuliwa kuwa vyenye ufanisi zaidi kuliko viwanda vya makaa vya teknolojia ya juu zaidi kwa sababu vinaweza kuzalisha umeme zaidi kwa kila tani ya makaa.[116] Hata hivyo, aina ya teknolojia ya mvuke itakayotumika - iwe ni ya chini, ya kati, au ya juu zaidi -haina athari yoyote kwa moshi utakaotolewa na kila tani ya makaa iliyochomwa; kiwanda cha USC kitakuwa kikichoma tani ya makaa kwa njia ya polepole kidogo kuliko aina zingine za viwanda.[117] Kama inavyojadiliwa kwa undani zaidi hapa chini, aina ya uchafuzi ni ule wa salfa diokside, nitriki okside na chembechembe hewani, zinazoathiri vibaya mfumo wa kupumua, na zebaki, ambayo huathiri afya ya akili. Mbali na athari hizi za afya, matokeo mengine ya kiwanda cha umeme, kama vile maji moto chafu na mvua ya asidi, hutishia mazingira ya mikoko na uvuvi katika kisiwa cha Manda na huhatarisha Turathi ya Dunia ya Lamu Old Town.

### *5. Athari za kutozingatia*

Kutotia maanani mahitaji haya ni kinyume na malengo ya IFC PS 1 na mchakato wa ESIA, ambao unahitaji mkabala kamili ili kuhakikisha uzingatiaji wa athari changamano kutokana na vipengele tofauti vya mradi na kuimarisha hatua za kupunguza makali na za kujiepusha na hatari, ambazo ndizo hali zinazotoa taswira ya upeo na ya kiwango cha athari. Pia kutozingatia huku kumesababisha mapungufu katika mashauriano na wanajamii kwa sababu mashauriano hayo

[113] Tazama, pamoja na kwingine, GE Africa Newsroom "Kenya's Amu Power Signs Clean Coal Technology Agreement with GE" (Mei 2018) https://ge.africa-newsroom.com/press/kenyas-amu-power-signs-clean-coal-technology-agreement-with-ge. Hata hivyo, ripoti zingine zimeonyesha wasiwasi kuhusu ukamilishaji wa mkataba: deCOALonize Kenya via Medium "450 million dollar deal between Gulf Energy & General Electric for the development of coal power still under discussion" (Jun. 2018) https://medium.com/@deCOALonize/450-million-dollar-deal-between-gulf-energy-general-electric-for-the-development-of-coal-power-a9c4497fea8; Profesa Daniel Kammen, RAEL Berkeley "General Electric Reconsiders Investment In Lamu Coal Plant" (Jul. 2018) https://rael.berkeley.edu/2018/07/general-electric-reconsiders-investment-in-lamu-coal-plant/.

[114] Tazama Barua ya GE kwa Save Lamu (19 Feb. 2019), iliyoambatwa katika Nyongeza 4

[115] 2016 ESIA, Sura 4.

[116] Lauri Myllyvirta, Energy Post "How much do ultra-supercritical coal plants really reduce air pollution?" (28 Jun. 2017) http://energypost.eu/how-much-do-ultra-supercritical-coal-plants-really-reduce-air-pollution/.

[117] *Id*.

hayashughulikii vipengele muhimu vya mradi. Hata kama muundo wa vipengele vingine haujulikani, tathmini ya mwanzo ingefanywa na data ya kimsingi ya kutosha ingekusanywa ili kuhakikisha tathmini kamili ya athari ipo wakati muundo wa mradi utakapojulikana. Na ingawa ESIA ilitolewa zaidi ya miaka miwili iliyopita, watetezi wa mradi hawajafanya marekebisho au maongezo ili kurekebisha upungufu huu.

### C. Mashauriano ya kijamii yamekuwa ya juu juu, si kamili, na hudidimizwa na vitisho vikubwa na kulipiza kisasi

Kipengele kingine muhimu cha mchakato wa utambulisho wa hatari za E&S na pia mpango wa kupunguza makali ni mashauriano ya kijamii yanayofaa. IFC PS 1 iko wazi kwamba mashauriano hayo lazima yawe halisi, ya mara kwa mara na ya pande zote mbili.[118]

- Mteja atafaulisha mchakato wa mashauriano kwa namna ambayo inawezesha jamii zilizoathiriwa kuwa na fursa ya kutoa maoni yao kuhusu hatari za mradi, athari na hatua za kupunguza makali, na kumruhusu mteja kuzingatia maoni hayo na kuyajibu.
- Mashauriano yenye ufanisi ni mchakato wa pande mbili. Mchakato huu unapaswa: (i) kuanza mapema katika taratibu za kutambua hatari na athari za mazingira na jamii na kuendelea kadri hatari na athari hizo zinavyotokea; (ii) kuzingatia ufafanuzi wa awali na usambazaji wa taarifa zinazofaa, zilizo wazi, zenye maana na zinazopatikana kwa urahisi, zinazozingatia tamaduni na lugha na muundo na zinazoeleweka kwa jamii zilizoathirika; (iii) kuzingatia ushirikishwaji wa pamoja kwa wale walioathiriwa moja kwa moja kinyume na wale ambao hawajaathirika moja kwa moja; (iv) kuepukana na udanganyifu kutoka nje, kuingiliwa, kulazimishwa, au kutishwa; (v) kuwezesha ushiriki wenye maana, panapofaa; na (vi) kuweka nyaraka. Mteja atafanya mchakato wake wa mashauriano kwa lugha inayofaa ya jamii zilizoathirika; mchakato wao wa kufanya maamuzi, na mahitaji ya makundi yaliyo katika hali ngumu au yanayoathirika.

Katika hali zinazohusisha "uwezekano mkubwa wa athari mbaya kwenye Jamii Zilizoathirika" (kiwango kinachoweza kufikiwa kutokana na ujenzi wa kiwanda kikubwa cha umeme wa makaa), mteja lazima awe na mchakato unaofaa wa Ushauriano na Ushiriki (ICP).[119]

- ICP inahusisha ubadilishanaji wa kina wa maoni na taarifa, na ushauri uliopangwa na wa mara kwa mara, ambao hatima yake ni mteja kuzingatia, katika maamuzi yake, maoni ya jamii zilizoathirika kuhusu masuala yanayowaathiri moja kwa moja, kama vile hatua zilizopendekezwa za kupunguza makali, mgawo wa faida na fursa ya maendeleo, na masuala ya utekelezaji.
- Mchakato wa ushauriano unapaswa: (i) kuzingatia maoni yote ya wanaume na wanawake, ikiwezekena kupitia vikao tofauti au ushirikishaji; na (ii) kuonyesha matatizo na vipaumbele miongoni mwa wanaume na wanawake kuhusu athari, taratibu za kupunguza makali na manufaa, panapowezekana.

---

[118] IFC PS 1, aya. 30.
[119] IFC PS 1, aya. 31.

- Mteja ataweka waraka kuhusu mchakato huo, hususan hatua zilizochukuliwa ili kuepuka au kupunguza hatari na athari mbaya kwa jamii zilizoathiriwa, na kuwajulisha wale walioathirika kuhusu namna matakwa yao yamezingatiwa.

Katika miradi yenye athari mbaya kwa Watu Asilia, mteja anahitajika kuwashirikisha katika mchakato wa ICP na kwa kiwango fulani mteja anahitajika kupata Mwafaka Huru, wa Awali na wenye Ufahamu (FPIC) kutoka kwao: Tazama sehemu III.F hapa chini.

Hatimaye, ili kuhakikisha kuwa mahitaji hayo yanafikiwa, "IFC kupitia uchunguzi wake mwenyewe, itaamua ikiwa ushirikishwaji wa jamii na mteja ni ule unaohusisha ICP na unawezesha ushirikishwaji wa Jamii Zilizoathiriwa, na ili kusababisha Uungwaji Mkono na jamii zilizoathiriwa kwa shughuli za kibiashara."[120]

Mashauriano hadi sasa hayajafikia viwango hivi.

Mikutano kuhusu mradi ilifanyika mapema mwaka 2015, lakini ikasitishwa ghafla mnamo Juni 2015. Wakati wa mikutano hii ya awali, hakuna maelezo ya kina au ya maana yaliyotolewa kuhusu mradi huo, athari zake (ikiwa ni pamoja na wasiwasi mkubwa wa jamii kuhusu athari za afya, hewa na uchafuzi wa maji, uhifadhi wa majivu na makazi mapya) au hatua zilizopendekezwa za kupunguza makali. Katika baadhi ya mikutano, washiriki hawakupata kamwe taarifa kuhusu vifaa vya mradi. Kwenye mikutano mingine, waliohudhuria walipokea brosha ya taarifa za mradi, lakini brosha hii ilikosa taarifa kuhusu vipengele vya msingi kuhusu mradi na ikarejelea kwa kifupi athari hasi za mradi.[121] Vipengele muhimu, kama vile kituo cha kuhifadhi taka hatari, havikuwekwa katika nyaraka hizi, na maelezo ya mifumo ya uhifadhi na usafirishaji wa makaa yalikuwa na upungufu na hivyo kutatiza uelewa wa maana. Brosha hiyo haikutafsiriwa kwa lugha ya wenyeji, Kiswahili. Utaratibu huu wa kiwango cha juu cha kuchukulia mradi bila kuzingatia utamaduni, haujitoshelezi kufanya jamii kuwa na maoni ya kina kuhusu mradi uliopendekezwa.

Raya Ahmed, mwanachama wa Save Lamu anakumbuka:[122]

> *"Nilihudhuria mkutano wa kiwanda cha makaa kilichopendekezwa tarehe 24 Januari 2015 uliofanyika katika Warsha ya Save Lamu Representatives kwenye Bustani ya Mkahawa wa Mwana Arafa katika Kisiwa cha Lamu. ... tulipewa muda mchache wa kuuliza maswali kuhusu mradi kwa vile Msimamizi Mradi alipaswa kuhudhuria mkutano mwingine uliopangwa kufanyika siku hiyo hiyo. ... maswali yaliyozingatiwa yaliulizwa kuhusu shughuli za kiwanda; kwa mfano, kama kiwanda cha makaa kitatoa aina zingine za taka zaidi ya yadi ya jivu na moshi usiothibitika zilizoonyeshwa katika uwasilishaji na ni sumu gani taka hizi huwa nayo. pamoja na hayo, niliuliza swali langu juu ya ni hatua gani zilizowekwa kukabiliana na ajali kubwa za dharura kutokana na mradi, Bw.Gandhi*

[120] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 30.
[121] 2016 ESIA, Nyongeza 9B: Social Impact Assessment Study Appendices, at 1.1 (Brosha ya Mradi).
[122] Taarifa ya Shahidi Raya Famau Ahmed katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environment Tribunal), Nairobi. Tazama pia Taarifa ya Shahidi Mohamed Athman Bakar katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environment Tribunal) Nairobi. Zote zimeambatwa katika Nyongeza 3.

*[mwandishi wa ushauri wa ESIA] alibainisha kuwa utafiti wa wataalamu ulikuwa unaendelea kuamua athari sahihi za kiwanda hiki na angeweza kushirikisha jamii kwa kwa hilo mara tu utakapokamilika "*

Maswali mengine yalijibiwa kwa habari za kupotosha na zisizo sahihi. Mwanachama mwingine wa Save Lamu, katika mkutano huo, anakumbuka kuwa:[123]

*"[Bwana. Gandhi] pia alisema kuwa maji ya bahari hata hivyo hayataathirika na kiwanda cha kuzalisha makaa kwa sababu watatumia teknolojia ya hali ya juu. Hata hivyo, baadaye niligundua kwamba teknolojia hii itakuwa na mfumo wa kutia maji baridi mara moja kutoka kwenye kiwanda cha umeme ambapo maji yatarudishwa tena kwenye Manda yakiwa joto. "*

Kwa sababu ya ukosefu huu wa maelezo ya kina na sahihi, maoni mengi kutoka kwa wajumbe wa jamii wakati wa mikutano ya mapema ya kushauriana yalizingatia kuomba maelezo ya ziada, badala ya kuwa na uwezo wa kutoa maoni yanayofaa juu ya vipengele maalumu vya mradi huo. Kiambatisho 9B cha ESIA kinaonyesha kwamba katika matukio mengi, wawakilishi wa mradi hawakuweza kujibu maswali kuhusu athari za mradi kwa jamii na mazingira na hatua zilizopendekezwa za kupunguza makali. Badala yake, wawakilishi hao walieleza kuwa masuala haya yatashughulikiwa katika utafiti wa baadaye.[124]

Ripoti ya Mradi ya Mazingira (EPR), iliyotolewa mwishoni mwa mwaka wa 2015, ilikuwa na maelezo ya ziada kuhusu mradi, lakini hakuna mashauriano yaliyofanyika mara tu au kufuatia kutolewa kwake. Baada ya kutolewa kwa ESIA mwezi Julai 2016, tunafahamu tu mkutano mmoja wa kijamii wa tarehe Agosti, 26 2016, ambao hauwezi chukuliwa kuwa wa mashauriano kwa sababu, baada ya kubadilishwa mahali pa mkutano dakika za mwisho, mkutano huu ulifanyika mahali ambapo hapangefikika kwa urahisi na wakazi wa Lamu, kutokana na umbali wa kusafiri na gharama. Mohamed Bakar, mwanachama mwingine wa Save Lamu, anaeleza:[125]

*"Mkutano huo ulikuwa vigumu kuhudhuria kwa sababu Kwasasi ambalo ni kundi la wakulima na wavuvi huishi mashambani katika eneo la kilomita 21 kutoka mji wa Lamu na kuna upungufu wa usafiri wa umma kutoka eneo hilo."*

Wanachama wa Kundi la Mvunjeni Self-Help hawakujua kuwepo kwa mkutano huo; hawakuambiwa wala kufahamishwa, na hawakutafakari wakati huo kwamba wangeathirika na barabara ya kufikia eneo la kiwanda cha makaa.

---

[123] Taarifa ya Shahidi Mohamed Mbwana katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environmental Tribunal), Nairobi, iliyoambatwa katika Nyongeza 3.
[124] *Tazama* kwa mfano., 2016 ESIA, Kiambatisho 9B katika 3.1.1 (Stakeholder Engagement Log No. 1:Wawakilishi wa Save Lamu), kipengee 18 (swali kuhusu hatua za dharura kukiwa na ajali); 14, kipengee 20 (swali kuhusu athari kwa vyanzo vya tiba ya jadi kama vile mizizi na matawi); 111, kipengee 11 (kuhusu athari kwa samaki na jamii ya wavuvi); 125, kipengee 8 (swali kuhusu athari kwa ekolojia ya baharini na maisha ya majini).
[125] Taarifa ya shahidi Mohamed Athman Bakar katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environment Tribunal), Nairobi, imeambatwa katika Nyongeza 3.

ESIA pia inajumuisha marejeleo ya tafiti na miongozo[126] ambayo haijafikiwi na jamii zilizoathirika.

Zaidi ya hayo, kinyume na mahitaji ya ICP, ESIA inashindwa kujibu kikamilifu maoni na malalamishi yoyote yaliyotolewa wakati wa mikutano hiyo ya awali ya jamii. Kwa mfano, wadau wa mradi na makundi ya jamii mara kwa mara walitoa malalamishi yao juu ya ukosefu wa tathmini za ziada za mapema katika kupanga mradi ili kuthibitisha ujenzi wa kiwanda cha makaa. Hata hivyo, ESIA haijumuishi tathmini hii (angalia Sehemu ya III.H hapo chini). Isitoshe, makundi ya wenyeji na watu walioathirika walilalamika juu ya hatari za mchakato wa mfumo wa kutia baridi na eneo lililochaguliwa kwa ajili ya mradi kando ya mikoko na pwani ya Manda katika awamu ya mwanzo ya mradi.[127] Jamii pia ililalamika kuhusu athari za afya kutokana na moshi , yadi ya majivu na taka zingine hatari zinazotolewa na kiwanda. Hata hivyo, muundo wa mradi katika ESIA unafanana sana na muundo ulioelezwa katika EPR ya 2015 na unalingana na taarifa katika brosha iliyosambazwa wakati wa mikutano ya utangulizi mwanzoni mwa mwaka wa 2015. Aidha, ESIA haielezi vile muundo wa mradi ulikosa kubadilishwa kutokana na malalamishi makubwa ya wanajamii.[128]

Maoni ya umma ya ESIA, na mchakato wa serikali wa kuidhinisha, ni dhihirisho zaidi kuwa ushirikishwaji wa wadau haukuwa wa maana. Licha ya makosa makubwa yaliyotajwa katika maoni ya umma yaliyotolewa kwa Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (*Kenyan National Environmental Management Authority - NEMA*), shirika hilo lilitoa idhini ya Leseni ya EIA mnamo Septemba 7, 2016, siku sita tu baada ya kufungwa kwa kutolewa maoni ya umma, bila kuhitaji mabadiliko yoyote kwa ESIA kwa mujibu wa maoni ya wadau ambayo NEMA ilikuwa imepokea. Haya ni pamoja na maoni yaliyoandikwa na yaliyotolewa na Save Lamu na Natural Justice.[129] Kutokana na matukio haya ya mradi, ni wazi kuwa kipindi cha maoni ya umma hakikuwa fursa kamili kwa wadau kutoa maoni yao kuhusu maendeleo ya ESIA, kama inavyotakiwa na Mfumo Endelevu wa IFC.

Kama ilivyojadiliwa hapo juu, kesi inayobainisha upungufu wa NEMA kukosa kuzingatia maoni ya umma kabla ya kutoa Leseni ya EIA inasubiri hukumu kutoka kwa Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (*Kenya National Environmental Tribunal-NET*).[130] Kesi hii iliwasilishwa mahakamani na Save Lamu pamoja na wakazi kadha mnamo Novemba 2016 na inadai kwamba NEMA ilikosea kwa kutoa leseni kwa msingi wa tathmini duni kuhusu jamii na mazingira na kwamba mchakato wa kushauriana na umma haukutosha. Kesi inajumuisha kufutiliwa mbali kwa leseni ya EIA na kufanya ESIA upya, kwa kuzingatia taarifa ya sasa na kuhusisha ushauriano na wadau wote wanaohusika. NET ilielekeza kwamba shughuli zote zinazohusiana na kiwanda cha makaa

[126] Pamja na miongozo kwa Kichina kama vile GB 18599-2001 kuhusu uhifadhi wa majivu.
[127] *Tazama* Barua ya Save Lamu kwa Amu Power (13 Mar. 2016), imeambatwa katika Nyongeza 4.
[128] IFC PS 1, aya 31: " Mteja…atawafahamisha watu wale walioathirika kuhusu namna hofu zao zilivyoshughulikiwa."
[129] *Tazama* Barua ya Save Lamu na Natural Justice kwa Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamzi wa Mazingira (National Environment Management Authority)(29 Aug. 2016)), imeambatwa katika Nyongeza 4.
[130] Notisi ya Rufani , Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environmental Tribunal) Rufani Na. NET/196/2016, 3-4, http://accountabilitycounsel.org/wp-content/uploads/2017/11/NET-Notice-of-Appeal-Cover-Page-w_-NET-Stamp-and-Appeal.pdf.

lazima ziachwe na kusubiri uamuzi wa kesi na hali hiyo imekuwa hivyo tangu Novemba 2016.[131] Usikilizaji wa kesi hiyo umekamilika, lakini hukumu bado haijatolewa.

Fauka ya hayo, tayari tumeelezea kuhusu ukosefu wa mashauriano yoyote ya umma au tathmini mpya za hatari ya E&S au mipango ya kupunguza uchafuzi kufuatia kutangazwa kuwa GE itatoa teknolojia ya hali ya juu zaidi (USC) kwa kiwanda cha makaa, kinyume na teknolojia ya kati iliyoelezwa na ESIA 2016.

Aidha, upungufu wa mashauriano ulioelezwa hapo juu unaongezeka zaidi kwa sababu wadau wa mradi wanaotambuliwa na ESIA hawajumuishi vikundi vyote vitakavyoathiriwa na mradi huo. Kama ilivyojadiliwa hapo awali, wakulima waliohamishwa kwa ajili ya barabara hawakushauriwa kabisa. Zaidi ya hayo, orodha ya wadau wa mradi haijahusisha wakazi wa Witu,[132] ingawa maelezo ya Mradi ya ESIA inathibitisha kwamba makubaliano makubwa ya kupewa ardhi katika Witu yalitolewa kama sehemu ya mchakato wa idhini ya mradi, hasa kwa lengo la uchimbaji wa madini ya chokaa.[133] Imeelezwa hapo juu kwamba athari za barabara ya kufikia eneo la mradi, uchimbaji chokaa katika eneo la Witu, na usafirishaji wake kutoka Witu hadi eneo la mradi hayajazingatiwa kabisa katika ESIA. Utozingatiaji huu usiokuwa wa haki wala halali unafungamana na kushindwa kutambua au kushauriana na wakulima wa Kwasasi Mvunjeni, wakazi wa Witu, au watu wale wanaoishi katika njia ya usafirishaji wa chokaa kuhusu jinsi mradi huo unaweza kuwaathiri moja kwa moja.

Vile vile, jamii za asili zilizoathiriwa na kiwanda cha makaa zimeachwa nje. Makundi ya asili tu ambayo yamehusishwa na ESIA ya 2016 na Summary RAP ni WaAweer (ambao wanatumia eneo la mradi kwa uwindaji na ulaji) na WaBajuni. Hata hivyo, jamii za WaOrma, WaSanye, na WaSwahili wataathirika pia na mradi huo. Makundi haya yote hayajashauriwa kikamilifu hadi kiwango cha ICP.[134] Kwa hakika, jamii nyingi za kiasili hazijashauriwa kabisa.

Hatimaye, tabia iliyopo ya kutishwa na viongozi wa serikali imekwamisha jitihada za vikundi vya wanajamii kuwa ma vikao ili kushiriki na kujadili athari za mradi kama jamii. Hasa, katika kipindi ambacho Amu Power alifanya mikutano ya jamii na baada ya Amu Power kuacha mikutano hii mwaka 2015 na 2016, Save Lamu na mashirika mengi ya wanachama walijaribu kufanya mikutano ili kuimarisha ubora wa mazungumzo miongoni mwa jamii nyingi za Lamu kuhusu maendeleo endelevu, miradi iliyopendekezwa, na hatari kwa riziki za wenyeji, mfumo wa ekolojia, uanuwai wa viumbe, afya na ustawi. Hata hivyo, wafanyakazi wa serikali wameweka vizuizi ili mikutano hii ya jamii isifanywe na hata wamefedhehesha kazi ya vikundi hivi. Vitisho hivyo vimeongezeka na vimeendelea kwa miaka mingi. Simu za wajumbe wa Save Lamu zinafuatiliwa , na uwezo wao wa kufanya shughuli zao katika maeneo fulani ya Kaunti ya Lamu, kwa mfano katika Mpeketoni na Hindi, umezuiliwa.

---

131 Kuh: Amri ya Kuacha Ujenzi wa Kiwanda cha Makaa cha S 1050 MW na Vifaa Vingine Vinavyohusika katikat Eneo la Kwasasi, Kata ya Hindi, Kaunti ya Lamu, Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environmental Tribunal) (14 Nov. 2016)) http://www.decoalonize.org/wp-content/uploads/2017/04/NET.pdf.

132 2016 ESIA, Kiambatisho 10: Mpango wa Kuwashirikisha Wadau, §4.

133 2016 ESIA, Sura 4, §4.2. Orodha ya wadau wa mradi iliandaliwa kwa msigi wa uchanganuzi wa tathmini iliyofanywa 2014.

134 *Tazama* pia Sehemu III.F hapo chini.

Mnamo Machi 2015, muda mchache baada ya Save Lamu kuanza kuhusika katika mikutano ya kiwanda cha makaa kilichopendekezwa, shirika na viongozi wake kadha walikabiliwa na vitisho vikubwa kwa njia ya uchunguzi wa makosa ya jinai kutoka Idara ya Upelelezi wa Uhalifu, Kenya (CID). Huku wakitumia fursa ya uchunguzi wa mashambulizi ya magaidi ya Juni 2014 huko Mpeketoni kama kisingizio, wapelelezi wa CID waliwasingizia Save Lamu kuwa walishiriki katika mashambulizi. Walipata kibali cha kuchunguza Save Lamu, walivamia ofisi ya Save Lamu na kuchukua faili, taarifa za benki za dhamana kutoka benki ya Save Lamu, na wakawaagiza viongozi wa Save Lamu kwenda Nairobi kwa ajili ya kuhojiwa.[135] Ijapokuwa uchunguzi wa CID unaonekana kusitishwa hatimaye, Save Lamu haijui uamuzi rasmi uliofikiwa.

Katika matukio mengine mengi, maafisa wa serikali wameyanyima makundi ruhusa ya kuandaa mikutano ya kutaarifisha umma kuhusu mradi, au kuzuia kabisa mikutano kutokea kwa kuahirisha uamuzi wao mara kwa mara.[136] Mnamo mwaka wa 2017, Kamishna wa Kaunti ya Lamu aliwashutumu wanaharakati hadharani na kudai kuwa wanachukua rushwa na kukubali malipo ili wapinge mradi huo, bila kutoa ushahidi wowote.[137] Mnamo mwaka wa 2018, Walid Ahmed na Ishaq Abubakar, wanaharakati wawili wa Lamu, walikamatwa baada ya maandamano yaliyoandaliwa ili kuomba kusimamishwa kwa mradi wa mkaa wa Lamu kwa sababu njia ya maandamano ilikuwa tofauti kidogo na ile iliyotolewa katika taarifa zao rasmi kuhusu maandamano ya amani.[138] Baadaye waliachiliwa kwa dhamana, ingawa walikabiliwa na vitisho kwa wiki moja. Vitisho hivi viliwazuia kusafiri au kufanya shughuli za kawaida.

Ripoti ya hivi karibuni ya vikundi vya haki za binadamu vya *Human Rights Watch* (HRW) na *Kenyan National Coalition for Human Rights Defenders* (KNCHRD) inabainisha kwamba matukio haya si ya kipekee: utafiti wao unadhihirisha unyanyasaji na vitisho vilivyotekelezwa na polisi, jeshi, na viongozi wengine wa serikali baina ya 2013-2018 dhidi ya wanaharakati wa mazingira wapatao zaidi ya 35 katika Kaunti ya Lamu.[139] Vikosi vya Usalama wamesambaratisha maandamano na kuzuia mikutano ya umma - ikiwa ni pamoja na ile inayohusiana na LAPSSET na kiwanda cha makaa kilichopendekezwa - na kutishia, kukamata, na kushitaki wanaharakati kwa mashtaka mbalimbali. Zaidi ya hayo, ripoti ina taarifa kuhusu kutoweka kwa watu wawili waliohusika katika kupinga unyakuzi wa ardhi, inayohusiana na LAPSSET, katika eneo la Lamu. Mnamo mwaka wa 2016, Mohamed Avukame, mwanaharakati wa haki za ardhi kutoka Kisiwa cha Manda, alikamatwa Mombasa na watu waliovaa sare za polisi. Wakati huo, alikuwa nje ya ofisi za Muslims for Human Rights (MUHURI), ambako alikuwa amechukua nyaraka kuhusu unyakuzi wa ardhi usio halali na pia fidia kutokana na

[135] *Tazama* Nyongeza 8 (siri) kwa taarifa zaidi.

[136] *Tazama*, kwa mfano, deCOALonize Kenya via Medium "Save Lamu Facing Intimidation and Interference" (9 Mei 2017) https://medium.com/@deCOAL/save-lamu-facing-intimidation-and-interference-9007309d166e.

[137] The Star, "Critics of Lamu coal-fired plant are corrupt, says state official" (29 Machi. 2017) http://www.the-star.co.ke/news/2017/03/29/critics-of-lamu-coal-fired-plant-are-corrupt-says-state-official_c1533287.

[138] Save Lamu "Two Save Lamu Activists Arrested For Organizing Fossil Free Protest" (26 Machi 2018) https://www.savelamu.org/lamu-break-free-campaign-against-coal-goes-bad-as-2-arrested/; Human Rights Watch and National Coalition for Human Rights Defenders "They Just Want to Silence Us" Abuses Against Environmental Activists at Kenya's Coast Region" (2018) https://www.hrw.org/report/2018/12/17/they-just-want-silence-us/abuses-against-environmental-activists-kenyas-coast.

[139] Human Rights Watch and National Coalition for Human Rights Defenders, uk. 2, 60.

mradi wa LAPSSET.[140] Hajaonekana tangu wakati huo. Katika tukio lingine kama hilo, mwaka wa 2016, Ali Bunu mwenyeji wa Pate alikamatwa karibu na nyumba yake pamoja na mwanawe na ndugu yake; mtu wa nasaba yake alimwona akipigwa risasi na washambuliaji, na inaaminika amekufa. Alikuwa akipinga unyakuzi wa ardhi yake inayohusiana na LAPSSET.[141]

Wakati ambapo vitisho vya maafisa wa serikali vinaathiri uwezo wa jamii kukutana hadharani kuujadili mradi huo, IFC na wateja wake wana jukumu maalumu la kuhakikisha kuwa mashauriano yenye maana yanafanyika na jamii zilizoathiriwa ziko huru kushiriki bila ya kutishwa au kulazimishwa.[142] ESIA, ambayo haina ushahidi wowote wa mikutano ya mashauriano katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, haijaweka msingi wa kiwango kinachohitajika cha mashauriano.

Kwa hivyo, mchakato huu wa mashauriano ya wadau unakosa kufikia kiwango cha chini cha mahitaji ya Mfumo Endelevu wa IFC. Upungufu wa habari iliyotolewa kabla ya mikutano ya mashauriano ilizuia watu walioathiriwa kushiriki kikamilifu katika kupanga na kubuni mradi. Zaidi ya hayo, mazungumzo yangepaswa kuendelea katika hatua za mipango ya muundo wa mradi. Kadri taarifa mpya zilivyojitokeza kuhusu muundo wa mradi, athari zitakazoweza kutokea na hatua za kupunguza makali, taarifa hii ilipaswa kuwasilishiwa wanajamii kwa muda ufaao, kabla ya mikutano ya mashauriano na jamii na wakati wa mikutano hiyo. Bila hatua hizi za kimsingi, washiriki wa mradi hawajafikia kiwango cha Uungwaji Mkono na Jamii Nzima katika mradi huu. Hawajaungwa mkono na wenyeji walioathiriwa na wadau wengine wa jamii.[143] Mashauriano zaidi lazima yafanyike, na IFC na wateja wake wanapaswa kuchukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha kwamba mashauriano haya yana fursa kwa watu wote walioathirika kutoa malalamishi yao kwa sauti, bila hofu yoyote au kulazimishwa.

### D. Kutochambua kikamilifu na kutoonyesha hatua za kupunguza makali ya uchafuzi wa hewa na maji, uanuwai wa viumbe, mfumo wa ekolojia na athari za hali ya anga

Pamoja na majukumu mapana katika IFC PS yanayowajibisha uchukuaji wa hatua ili kuepuka, kupunguza na kufidia athari za kimazingira na jamii,[144] PS 3 (Ufanisi wa rasilmali na kuzuia uchafuzi wa mazingira), PS 4 (Afya ya jamii na usalama) na PS 6 (uanuwai wa viumbehai, uhifadhi na usimamizi endelevu wa maliasili hai) zina maagizo maalumu ya kuepuka na kupunguza kuharibiwa kwa mazingira ya asili, na athari zinazohusiana na afya na riziki. Pamoja na majukumu mengine muhimu, kuna yafuatayo:

- IFC PS 3 imeagiza kuwa miradi itumie mbinu bora za kiufundi za kuzuia uchafuzi wa mazingira ili kuepuka, au ikiwa kuepuka hakuwezekani, kupunguza madhara kwa afya ya binadamu na mazingira;[145]

[140] *Id.*, uk. 26-27.
[141] *Id.*, uk. 27-28.
[142] " Mashauriano yenye ufanisi …yawe …huru, yasiyoingiliwa, kulazimishwa au kutishwa": IFC PS 1, aya. 30.
[143] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 30.
[144] Tazama ngazi ya kupunguza makali inayorejelewa katika IFC PS 1, "Malengo".
[145] IFC PS 3, aya. 4.

- IFC PS 4 vilevile imeshurutisha kwamba miradi iwe na  hatua za kukinga na kudhibiti ambazo zinalingana na mazoea mazuri ya viwanda kimataifa ili kuepuka au kupunguza kabisa madhara kwa afya ya jamii na usalama. Pia, vipimo vya kupunguza madhara havina budi kuegemea uepukaji wa hatari na athari badala ya kupunguza;[146] na
- IFC PS 6 inahitaji, kama suala la kipaumbele, miradi iepuke athari  kwa uanuwai wa viumbe na mfumo wa ekolojia (manufaa ambayo watu hupata kutoka kwa mazingira).[147] Majukumu yanapewa nguvu zaidi wakati mazingira ya kiasili[148] na makazi muhimu yanapohusika,[149] ambayo ni mengi katika eneo la kiwanda kinachokusudiwa.

1. *Udhaifu wa taratibu za utafiti wa kimsingi unatilia shaka matokeo ya ESIA*

Hatua ya kwanza katika kutambua hatari na madhara ya kijamii na mazingira ni ukusanyaji wa "data ya kimsingi ya hivi karibuni ya kimazingira na kijamii katika kiwango cha undani kifaacho." [150]

Utafiti wa Tathmini ya Athari kwa Ekolojia, unaojumuishwa kama Kiambatisho cha 5 katika ESIA ya 2016, unatambua mapengo na masuala kadha kuhusu ukusanyaji wa taarifa za eneo la mradi. Masuala haya yanasaili ukubalifu wa baadhi ya matokeo ya utafiti.[151] Kwa mfano, sehemu hii inabainisha kwamba utafiti wa ndege wa mahali hapo uliangazia eneo dogo kuliko inavyopendekezwa katika tafiti za aina hii na kwamba utazamaji wa eneo uliangazia sehemu moja kwa masaa machache tu, wakati wa mchana ambapo ndege kwa kawaida wamepumzika. Kwa pamoja,[152] masuala haya yanafanya iwe vigumu kuamini matokeo ya utafiti kuhusu ndege wa mahali hapo.

Utafiti wa wanyama  pia unaeleza kuwa sampuli za nyanjani zilikuwa za siku tano pekee, na matokeo yake yakawa kwamba kuna wanyama ambao hawakuwa sehemu ya sampuli kamwe.[153] Utafiti huu unaeleza kuwa tafiti kama hizi kwa kawaida huzingatia sampuli za mchana na usiku, wakati wa msimu wa kiangazi na masika, lakini ufanyaji sampuli wa usiku na masika haukuwezekana kwa sababu ya hofu ya usalama (kuzuiliwa kwa ziara za usiku) na vikwazo vya wakati.[154]

Utafiti wa maeneo chepechepe ya pwani na ya viumbe wa baharini pia ulikuwa na vikwazo. ESIA ya 2016 inakiri kwamba jitihada za uchukuaji wa sampuli za wanyama wa baharini wasio

---

[146] IFC PS 4, aya. 5.
[147] IFC PS 6, aya. 7.
[148] IFC PS 6, aya. 13-15 (Makazi ya asili) na aya 16-19 (Makazi muhimu).
[149] IFC PS 6, aya. 20.
[150] IFC PS 1, aya. 7.
[151] 2016 ESIA, Kiambatisho 5, §7.1.
[152] *Id.*
[153] *Id.* at §7.3.
[154] *Id.*  Angalizo kuhusu ukosefu wa muda uliozuia kuchukua sampuli za msimu wa mvua ni linashangaza kwa sababu uchukuaji sampuli ulifanywa Januari 2015, and ESIA haikutangazwa hadi Julai 2016, na hili linaonyesha kulikuwa na muda wa kutosha kuchukua sampuli za ziada katika muda uliokuwepo.

na uti wa mgongo, mwani, uvuvi, miamba ya matumbawe na mikoko zilikuwa "chini ....kwa sababu siku za kuchukua sampuli zilikuwa kumi tu".[155]

Mapengo haya katika ukusanyaji wa taarifa nyanjani yanatilia shaka matokeo ya utafiti wa msingi, hasa kuhusu mimea na maeneo ya baharini yanayozunguka mradi. Pia, mapengo haya yanaonyesha ukiukaji wa mahitaji bayana ya IFC PS yanayoagiza kwamba "tathmini za nyanjani za mradi na hatari maalumu za eneo la miradi na athari zinapaswa kuzingatia maelezo ya msingi yaliyopo na yanayoweza kuthibitika."[156] Zaidi ya hayo, ufafanuzi wa upungufu huu – kuhusu vikwazo vya wakati vilivyowekwa na mkandarasi wa ESIA, Kurrent Technologies, au hofu ya usalama – vinatisha, tuzingatiapo kwamba tathmini sahihi na ya kimsingi ni agizo muhimu kwa tathmini yoyote ya athari za kijamii na kimazingira. Vikwazo vilivyowekwa na mkandarasi kuhusu muda unaoruhusiwa kwa wataalamu ili kukusanya data ya msingi ni dhihirisho la ukosefu wa kujitolea ili kufuatilia athari za kijamii na kimazingira. Jambo hili ni kinyume na maagizo ya IFC PS. Fauka ya hayo, hakuna ushahidi ya kwamba washiriki wa mradi wametumia miaka ya kati tangu sampuli ya msingi ya awali kufanyika ili kushirikisha maelezo ya ziada ya kuimarisha data ya msingi na kurekebisha upungufu wowote wa tafiti za awali. Vikwazo vya wakati vinavyotokana na na hofu ya usalama, vinaonyesha kwamba eneo la mradi uliopendekezwa linaweza kuwa hatari sana, jambo ambalo pia limepuuzwa kabisa na ESIA.

Mapengo na masuala ya upungufu katika taratibu za sampuli yaliyotambuliwa katika Utafiti wa Tathmini ya Athari za Kiekolojia yanaibua maswali kama matokeo yake ni kielelezo sahihi cha mazingira yaliyopo, na mazingira ya kabla ya mradi. Tathmini ya msingi ni kipengele muhimu cha tathmini yoyote ya athari, kwa sababu baada ya kuanzisha ujenzi, itakuwa vigumu kukabiliana na upungufu wowote wa msingi.

2. *Tathmini ya athari za uanuwai wa viumbe haina taarifa ya kina inayohitajika ili kuendeleza hatua za kutosha za kupunguza makali*

Kama ilivyoelezwa hapo juu, IFC PS 6 inajumuisha maagizo magumu kwa wateja ili kuepuka kudhuru uanuwai wa viumbe na huduma za mfumo wa ekolojia.[157] Maagizo yaliyowekwa na IFC PS 6 yanashadidiwa wakati mradi unahatarisha mazingira muhimu na ya asili, yaliyoko karibu na kiwanda cha makaa kilichopendekezwa Lamu:

- Kuhusu mazingira ya asili (yaani maeneo mengi ya asili, au yenye hali ambayo haijabadilishwa ama kufanyiwa kazi za kiekolojia),[158] mteja hatakiwi kubadilisha au kuharibu makazi hayo isipokuwa iwe kwamba: hakuna maeneo mengine yanayofaa kwa maendeleo ya mradi katika makazi yaliyobadilishwa; mashauriano yamezingatia maoni

---

[155] *Id.* katika §7.5.
[156] Angalizo la Mwongozo: 1, GN20. Ayah ii inaendelea " Taarifa ya msingi iliyosahihi na ya wakati ni muhimu, kwa sababu hali zinazobadilika haraka kama vile uhamiaji wa watu kwa sababu ya ujenzi wa mradi au maendeleo, ama ukosefu wa data kuhusu watu na jamii zilizohatarini na makundi katika jamii zilizoathirika, huweza kuathiri ufanisi wa hatua za kupunguza makali kijamii."
[157] IFC PS 6, aya 7.
[158] IFC PS 6, aya. 13.

ya wadau, ikiwa ni pamoja na jamii zilizoathirika, kutia maanani kiwango vya ubadilishaji na uharibifu; na ubadilishaji au uharibifu wowote umepunguzwa makali kwa mujibu wa ngazi ya udhibiti (bila kupotezwa kwa uanuwai wa viumbe kadri iwezekanavyo).[159]

- Katika maeneo ya makao maalumu (yenye thamani kubwa ya uanuwai),[160] IFC PS 6 inaweka wazi kuwa mradi usitekeleze shughuli zozote isipokuwa iwe kwamba: hakuna maeneo mengine yanayofaa kwa maendeleo ya mradi kwenye makao yasiyo muhimu; mradi hauna madhara kwa thamani ya uanuwai wa viumbe ambapo makazi maalumu yalichaguliwa, na juu ya michakato ya kiekolojia inayounga mkono thamani ya uanuwai wa viumbe; mradi haupelekei kupunguza kimataifa na / au kitaifa / kikanda idadi ya viumbe wa aina yoyote wanaohatarishwa katika kipindi maalumu cha wakati; na mpango imara na wa kudumu, ulioundwa vizuri wa ufuatiliaji na tathmini ya uanuwai wa viumbe umejumuishwa katika mpango wa usimamizi wa mradi.[161]

Mteja lazima pia ahifadhi wataalamu wa nje wenye uzoefu unaofaa wa kikanda ili kusaidia katika kuimarisha hatua za mipango inayozingatia PS 6 na kuthibitisha utekelezaji wa hatua hizo.[162]

Katika Kaunti ya Lamu mna viumbe kadha wa baharini wanaolindwa kisheria, misitu na hifadhi ya wanyamapori. Vitu hivi vinastahili ulinzi wa ziada kama makazi asili na muhimu chini ya IFC PS 6.[163] Izingatiwe zaidi kwamba:

- Katika kaskazini mashariki ya eneo la mradi kuna Mazingira ya Msitu wa Boni-Lungi , pamoja na Boni na Hifadhi ya Taifa ya Dodori.[164] Hifadhi hizi zinaunganisha misitu na nyika kuelekea kaskazini na kusini-magharibi ili kuunda ukanda muhimu wa wanyamapori. Ni sehemu muhimu ya msitu wa ekolojia ya Pwani ya Afrika Mashariki inayojulikana kimataifa.[165] Hifadhi hii ni makazi muhimu kwa tembo, paa,[166] swala, ndege, simba, twiga na kiboko.[167] Hifadhi hizi kwa pamoja zinaunda sehemu ya ardhi ya WaAweer (WaBoni).[168] Misitu hii ya pwani pia ni muhimu kama eneo la chanzo cha mvua na inatoa rasilimali nyingi za thamani mitaani, na pia kitaifa na kimataifa.[169]


---

159 IFC PS 6, aya. 14.
160 IFC PS 6, aya. 16.
161 IFC PS 6, aya. 17.
162 IFC PS 6, aya. 8.
163 IFC PS 6, aya. 20.
164 Hifadhi za Kitaifa za Boni and Dodori zilitangazwa rasmi katika gazeti la serikali mnamo 1976.
165 Lamu County Spatial Plan, §4.3.1.1; https://www.cepf.net/our-work/biodiversity-hotspots/coastal-forests-eastern-africa.
166 Anachukuliwa kama paa wa kipee duniani: IUCN Red List, "Hirola", https://www.iucnredlist.org/species/6234/50185297.
167 Lamu County Spatial Plan, §4.3.
168 BCP, §§4.4 and 6.4. Utangazaji rasmi wa hifadhi hizi katika gazeti la serikali ulizuia jamii wa WaAweer kufikia rasilmali muhimu kwa riziki zao na maeneo matakatifu, na hivyo kuchangia katika kuhatarishwa kwao.
169 *Tazama* kwa mfano, ., Paul Matiku, Nature Kenya "The Coastal Forests of Kenya: Forests data, threats, socio-economic issues, values, stakeholders, challenges, strategies, investment and enabling environment: A national synthesis report for the development of the WWF-EARPO Eastern Africa Coastal Forests Ecoregion Programme" (2004) http://coastalforests.tfcg.org/pubs/National-Synthesis-Ken.pdf.

- Pia kaskazini mashariki mwa eneo la mradi, Hifadhi ya Taifa ya Bahari Kiunga (*Kiunga Marine National Reserve*) inajumuisha pwani na visiwa 50 na miamba ya matumbawe katika eneo la Lamu.[170] Hifadhi ni muhimu kwa kupumzisha ndege wa baharini, kasa wa kijani na nguva, pamoja na mikoko inayopendeza. Eneo hili limeteuliwa kama Sehemu ya Hifadhi ya UNESCO.[171]
- Katika kusini-magharibi mwa eneo la mradi, karibu na mahali panapokusudiwa kuwa na na machimbo ya chokaa, mna Hifadhi ya Msitu wa Witu inayojulikana kuwa na angalau aina tisa za mimea iliyotishiwa, pamoja na *Euphorbia tanaensis* iliyohatarishwa. Nyika yake ni eneo muhimu ya malisho kwa nyati, nyamera, kuro, na pongo.[172]

Aidha, Lamu imezingirwa na aina nyingi za viumbe wa baharini na makazi, kama ilivyoonyeshwa kwenye Mchoro wa 6.

**Mchoro wa 6: Maeneo muhimu ya mazingira katika Kaunti ya Lamu**




*Chanzo: Mpango wa Kaunti ya Lamu (2016-2026) Ripoti ya Mwisho (Juzuu I, Mei 2017).*

---

[170] Ilitangazwa rasmi katika gazeti la serikali mnamo 1979.

[171] Hifadhi hizi ni maeneo yalipangwa na kutambuliwa na UNESCO katika mradi wa UNESCO's Man and the Biosphere Programme: http://www.unesco.org/mabdb/br/brdir/directory/biores.asp?code=KEN+04&mode=all.

[172] Lamu County Spatial Plan, §4.3.1.2.

Tunahofia kwamba kiwanda cha makaa kilichopendekezwa Lamu kinahatarisha eneo hili na sehemu zingine muhimu kimazingira: wote walio karibu na miundombinu ya mradi pamoja na walio maeneo mengine kwa sababu ya uhamaji kutokana na uchafuzi wa hewa na wa bahari. Hata hivyo, kinyume na matarajio ya IFC PS 6, ESIA ya 2016 haijatoa maelezo kamili ili kupima athari hizo. Pia haijatambua hatua za kutosha za kuepuka na kupunguza makali ya kiwanda. Upungufu huu umezuia mashauriano yoyote ya maana kuhusu madhara hayo, jambo ambalo ni ukiukaji zaidi wa IFC PS 6.

Utafiti wa Tathmini ya Athari za Kiekolojia ( *Ecological Impact Assessment Study*) unaohusishwa na ESIA, unaonyesha kwamba kuna makazi mengi ya asili na muhimu yaliyo karibu na eneo la mradi,[173] na kwamba mradi utabadilisha angalau baadhi ya makazi haya. Hata hivyo, ESIA haitoi maelezo ya kiwango au upana wa madhara haya. Kwa mfano, kama ilivyojadiliwa hapo chini, ESIA haina taarifa kuhusu athari halisi ya uchimbaji, upakiaji viumbe wa baharini katika mifumo ya kutia maji baridi, na utolewaji wa maji moto kuelekea katika mazingira ya baharini. Haishughulikii kabisa athari za uanuwai wa viumbe na mfumo wa usafirishaji wa makaa wa kilomita 15 uliopangwa na uchimbaji wa chokaa katika eneo la Witu. Bila taarifa hii, mradi hauwezi kuendeleza hatua zinazofaa za kuzuia na kupunguza athari chanya, wala hauwezi kutambua kwa usahihi thamani ya uanuwai wa viumbe na mfumo wa ekolojia ambao utaharibiwa.

*a. Athari kutokana na uchimbaji*

ESIA 2016 inakiri kuwa "shughuli za uchimbaji wakati wa awamu ya ujenzi zinaweza kusababisha uharibifu mkubwa na mbaya katika makazi jirani ya mikoko, mwani na makazi ya miamba ya matumbawe."[174] Inatoa mfano wa ujenzi wa kiwanda cha ndege cha Mokowe, ambapo karibu hekta 100 za misitu ya mikoko iliharibiwa na mchanga kutokana na shughuli za uchimbaji.[175]

Ijapokuwa taarifa hizi zinatisha, ESIA ya 2016 inakabiliana na athari za uchimbaji kwa njia ya ujumla badala ya njia maalumu kutegemea ubainifu wa nyanjani. ESIA yenyewe inabainisha kwamba vipengele vingi muhimu havikuzingatiwa. Jambo hili linazuia utabiri wowote maalumu wa aina, kiwango na upeo wa athari hizi. Kwa mfano, tathmini haizingatii miundo maalumu ya uchukuaji na utoaji, ujenzi ambao "unaweza kuhusisha" uchimbaji wa maeneo kando ya bahari.[176] Aidha, ESIA haijakadiria kiasi cha vifaa vitakavyochimbwa, au kutathmini uwezekano wa athari za mchanga.[177] Isitoshe, wakati ESIA inatahadharisha kuwa mchanga unaotokana na uchimbaji ni wa masikitisho makubwa,[178] inakosa kutoa makadirio ya uharibifu wa eneo hilo hasa. Mabadiliko katika upatikanaji wa virutubisho, utawanyikaji wa uchafu wakati wa

---

[173] *Tazama* 2016 ESIA, Kiambatisho 5, Tathmini ya Athari za Kiekolojia (Ecological Impact Assessment Study), §7.4, listing critical habitats including sea grass beds, coral reefs, estuaries, mangroves, lagoons and rocky shores. *Tazama* pia 2016 ESIA, Appendix 5, §3.2.10-3.2.13.
[174] 2016 ESIA, Sura ya 8: Assessment of Potential Environmental and Social Impacts and Mitigation Measures, §8.9.1, p. 53.
[175] *Id.*
[176] *Id.* uk. 52.
[177] ESIA ya 2016 ESIA inataja tu kwamba " huenda ikafikia mamia ya maelfu $m^3$." *Id.*
[178] *Id.*

uchimbaji na utupaji taka unatajwa kama athari za kinadharia za uchimbaji. ESIA haitoi maelezo au tathmini ya jinsi athari hizi zinavyoweza kukadiriwa katika eneo hili la mradi.[179]

Mbali na upungufu huu mkubwa wa maelezo kuhusu athari za uchimbaji, hatua za kupunguza makali ni za hali ya chini sana . Kwa mfano, hatua za kupunguza makali ni pamoja na mapendekezo ya "kuzingatia wakati wa uchimbaji" kutegemea maarifa ya mikondo ya maji na mawimbi ili kupunguza utupaji wa mchanga, na kutambua njia ya kufikia eneo la uchimbaji pamoja na tishali itakayozuia uharibifu wa miamba ya matumbawe, bila kujumuisha tathmini yoyote ya namna ya kuyatekeleza au kama hatua hizi ziko wazi na zenye ufanisi.[180] Bila uchunguzi zaidi, ni vigumu kuamini kwamba mabadiliko machache ya wakati na mkondo yatakuwa ya kutosha katika kuepuka madhara makubwa na madhubuti ya uchimbaji na mchanga kwenye maeneo mepesi ya baharini yaliyo karibu na mradi

*b. Athari kutokana na upakiaji na ugongwaji wa viumbe wa baharini*

Licha ya kuwepo kwa teknolojia isiyo madhara makubwa,[181] kiwanda cha makaa kinapendekeza kutumia mfumo wa kutia baridi mara moja. ESIA inakiri kwamba viumbe wa baharini wanaweza kuathiriwa na/au kupakiwa na mifumo wa kuingiza maji na / au kushikwa kwenye skrini ya nje ya kilango cha kuingiza baridi (kugongwa).[182] Inasema kuwa matukio hayo yote yanaweza kusababisha vifo vya viumbe wa baharini wa eneo hilo,[183] lakini haitoi tathmini yoyote ya kiwango au ukubwa wa athari hizo (yaani ni viumbe wangapi wanaoweza kustahimili hatima hii na hili litaathiri vipi viumbe wa baharini kwa jumla). Hakuna hatua zinazopendekezwa ili kuepuka au kupunguza madhara haya.

*c. Athari kutokana na maji kupanda joto*

Kisiwa cha Manda kina bahari ya pwani na ni mahali pa mapumziko na milango ya mito yenye maji ya chumvi kiasi tu, inayoathiri mawimbi. Milango hiyo ya mito ni rasilimali kubwa inayorutubisha bahari.[184]

Mfumo wa kutia baridi mara moja unaokusudiwa na mradi utatoa maji ya baridi yaliyotumika na kuyarudisha baharini kwa joto la juu la nyuzi 9 Celsius zaidi kuliko joto ya maji iliyoko humo.[185] Hata kuongezeka kidogo kwa joto la maji huweza kusababisha athari kubwa katika mifumo changamano ya maji, kwa kupunguza kiwango cha oksijeni iliyoyeyuka, kuongeza viwango vya

[179] *Id.* uk. 53.
[180] *Id.* uk. 55, Jedwali 8-31.
[181] Tazama Taarifa ya Shahidi Mark Chernaik katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environmental Tribunal), Nairobi, 1.4 iliyoambatwa katika Nyongeza 3.
[182] 2016 ESIA, Sura 8, §8.9.1 katika 54-55.
[183] 2016 ESIA katika 54.
[184] Tazama tena Taarifa ya shahidi Mark Chernaik katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environmental Tribunal), 3.2 iliyoambatwa katka Nyongeza 3.
[185] 2016 ESIA, Sura 8, §8.4.1 at 22.

umetaboli na kulazimisha uhamaji. Athari hizi zote za kiekolojia zinaweza kusababisha mabadiliko makubwa katika uanuwai wa viumbe wa majini.[186]

ESIA ya 2016 inakiri kuwa uchafuzi huu wa joto unaweza kubadilisha hali na namna viumbe wa baharini wamegawanywa katika eneo, huku ikitaja madhara yaliyoenea na yanayosababishwa na tofauti nyingine, japo ndogo (ya kiwango cha nyuzi 1-2 Celsius pekee) ya mabadiliko ya joto la maji katika eneo hilohilo.[187] Hata hivyo, bila uthibitishaji wa kutosha, ESIA ya 2016 inashindwa kutoa uchunguzi wowote wa eneo ili kuamua athari zinazowezekana kwenye maisha ya baharini katika hali hii.[188] Kwa kuzingatia kwamba kiwanda cha makaa cha Lamu kinaweza kuachilia maji ambayo ni ya nyuzi 9 Celsius zaidi kuliko joto la maji ya kawaida, athari hizo zinaweza kuwa kubwa sana. Aidha, mradi huo unaweza kuepuka athari hizo kupitia matumizi ya mfumo mbadala wa kutia baridi kiwandani.[189]

Utafiti wa Esia wa Utoaji Joto naViumbe wa Baharini (*Marine Thermal Discharge Study)* unatathmini aina za utoaji joto na unadai kuwa aina inayochaguliwa iafikiani na maagizo ya IFC kwamba utoaji joto usiongeza joto ya maji kwa zaidi ya digrii tatu Celsius katika eneo fulani.[190] Hata hivyo, kiwango hiki cha digrii tatu kichukuliwe kama cha chini zaidi na ambacho si lazima iwe kimetosha kulinda mimea na wanyama katika eneo laini la baharini na mazingira yake.[191] IFC ina viwango vingine vinavyoagiza waziwazi kwamba mfumo wa utoaji joto uandaliwe ili kuzuia athari mbaya na uhatarishaji wa maeneo laini au kuathiri mienendo ya uzazi na ulishaji.[192] Ukosefu kabisa wa uchanganuzi wa athari mahususi katika muundo wa mradi, licha ya matokeo makubwa yawezekanayo katika makazi ya baharini, ni dhihirisho la upungufu uliopo ili kufikia viwango vya IFC PS.

*d. . Athari kutoka yadi ya jivu*

Mbali na majukumu makubwa ya kuzuia uchafuzi wa mazingira na kuepuka athari kwa huduma za uanuwai wa viumbe na mfumo wa ekolojia, IFC PS 3 huweka majukumu maalumu kwa

---

[186] Taarifa ya shahidi Mark Chernaik katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environmental Tribunal), 3.2, iliyoambatwa katika Nyongeza 3 3.

[187] 2016 ESIA, Sura 8, §8.4.1 katika 22 (“ Maji ya kutia baridi mfumo yatatolewa moja kwa moja kutoka baharini, na yakishatumiwa yatarejeshwa baharini. Wakati yakiachiliwa tofauti ya joto itakuwa nyuzi 9 Celsius zaidi kuliko joto la maji ya kawaida. Bila kuzingatia njia za kupunguza makali, maji yenye tofauti ya joto kiasi hicho yataathiri makazi laini kama vile matumbawe na vilivyomo. Kwa mfano, mnamo 1997–1998 hali ya El Niño Afrika Mashariki ilisababisha joto la baharini kupanda kwa kiasi cha 1–2°C mnamo Machi – Aprili 1998, na kusababisha uharibifu wa matumbawe na hali ya uhai katika eneo hilo.” .

[188] *Id.* katika23.

[189] Taarifa ya Shahidi Mark Chernaik in the National Environmental Tribunal, 3.2 attached in Annex 3.

[190] Tazama ESIA 2016 Kiambatisho 1: Hydrodynamic Modelling Report, §4.1 katika 27.

[191] Kiwango kinapatikana katika Miongozo ya Jumla ya IFC kuhusu Afya ya Mazingira na Usalama (General Environmental Health and Safety Guidelines) na kimeelezwa kama mojawapo wa mambo ya kuzingatiwa wakati wa kuweka viwango vya utendaji vya mradi katika kudhibiti maji machafu. IFC General EHS Guidelines (30 Apr. 2007), uk. 26 http://www.ifc.org/wps/wcm/connect/554e8d80488658e4b76af76a6515bb18/Final%2B-%2BGeneral%2BEHS%2BGuidelines.pdf?MOD=AJPERES

[192] IFC Environmental Health and Safety Guidelines for Thermal Power Plants (19 Dec. 2008), uk. 10 http://www.ifc.org/wps/wcm/connect/dfb6a60048855a21852cd76a6515bb18/FINAL_Thermal%2BPower.pdf?MOD=AJPERES&id=1323162579734. NoteZingatia kwamba kiwango hiki hasa kimelenga viwanda vya umeme, kinyume na kanuni ya digrii 3 Celsius, inayohusu maji machafu yote [EHS Guidelines for Thermal Power Plants].

wateja ili kuepuka na kupunguza taka. Endapo taka haiwezi kuepukwa, kurejeshwa au kutumika tena, mteja lazima aitibu, aiharibu, au kuitupa kwa njia inayofaa kimazingira na ambayo inajumuisha udhibiti sahihi wa moshi na mabaki kutokana na utunzaji na usindikaji wa vifaa vya taka. Ikiwa taka iliyozalishwa inachukuliwa kuwa hatari, mteja lazima azingatie mazoea bora ya kimataifa kuhusu viwanda ili kufaulisha utupaji taka unaofaa kimazingira.[193]

Kwa mujibu wa ESIA, taka kutoka mradi huo, ikiwa ni pamoja na jivu lililoponyoka na kuingia hewani, jivu la chini na jasi, itatupwa katika yadi ya majivu kwa miaka 15.[194] Yadi ya jivu itapokea takribani 592,000 m3 ya taka ya majivu kwa kipindi cha miaka 15.[195] Jumla ya majivu ya makaa ambayo eneo litakuwa nayo ni 26,740,000 m3.[196] Hakuna mikakati yoyote ya kurejesha taka, kama inavyohitajika na IFC PS 3, ili kutengenezea aina ya bidhaa za mwako wa makaa zisizo na madhara na zenye manufaa kiuchumi.[197]

Yadi za majivu zinahitaji kiasi kikubwa cha ardhi ya kilimo, na zina hatari kubwa kimazingira na ni hatarishi kwa afya ya jamii, pamoja na uvujaji na uchafuzi wa hewa na huwa na athari za kimazingira zisizoweza kurekebishwa. Licha ya hayo, ESIA ina taarifa chache kuhusu viwango ambavyo vitatumiwa kujenga yadi za jivu, ikitoa mfano kutoka China wa Chinese Standard GB 18599-2001 bila kutoa tafsiri ya Kiingereza.[198]

Isitoshe, ESIA haitoi maelezo yoyote kuhusu jinsi yadi za majivu ya makaa zitahifadhiwa, hata baada ya kueleza kwamba eneo hilo huwa na monsuni zinazoweza kueneza na kuharibu majivu.[199] Hatari zinazohusiana na uvujaji ni mbaya mno. Mnamo 2008, kiasi cha majivu 4,200,000 m3 (sehemu ndogo kabisa ya majivu ambayo hatimaye yatahifadhiwa Lamu) kilitolewa wakati wa umwagikaji katika kiwanda cha makaa ya umeme huko TVA Kingston nchini Marekani.[200] Kufuatia uchafuzi huo, majaribio ya ubora wa maji karibu na eneo la uchafuzi yalionyesha viwango vya juu vya sumu ya madini ya risasi na thaliamu (*thallium*) ambayo inahusishwa na kasoro za kuzaliwa na matatizo ya mfumo wa neva.[201] Katika miaka kumi tangu uchafuzi huo, mashtaka yaliyoko yanadai kuwa wafanyakazi zaidi ya 180 ambao walisaidia katika jitihada za usafishaji wamekufa au ni wagonjwa sana kutokana na kuhatarishwa kwao na jivu la makaa.[202] Huku ikikiri kwamba yadi ya majivu ya makaa huko Lamu

[193] IFC PS 3, aya. 12. Tazama pia Miongozo EHS Guidelines for Thermal Power Plants, uk. 12.
[194] 2016 ESIA, Sura 4, §4.6.5.
[195] *Id*. katika 20.
[196] *Id*.
[197] *Tazama* pia Mwongozo wa EHS Guidelines for Thermal Power Plants, unaopendekeza matumizi ya takataka kama 'hatua mojawapo ya kuzuia, kupunguza, na kudhibiti wingi wa takataka viwandani vya umeme" – uk. 12.
[198] 2016 ESIA, Sura 4, §4.6.5.
[199] *Id.* katika 21.
[200] "Kingston Fossil Plant coal fly ash slurry spill," Wikipedia https://en.wikipedia.org/wiki/Kingston_Fossil_Plant_coal_fly_ash_slurry_spill.
[201] "The Lasting Damage of the Tennessee Coal Ash Spill," *Scientific American* (undated, but 2009) https://www.scientificamerican.com/article/tennessee-coal-ash-spill/.
[202] Jamie Satterfield, "180 new cases of dead or dying coal ash spill workers, lawsuit says," *Knox News* (28 Mar. 2018) https://www.knoxnews.com/story/news/crime/2018/03/28/tva-coal-ash-spill-cleanup-roane-county-lawsuits-dead-dying-workers/458342002/.

"itahifadhiwa, ikizingatia mahitaji ya utulivu,"[203] ESIA haitoi maelezo zaidi kuhusu hatua hizo za uhifadhi.

Ripoti hiyo pia haijaeleza namna jivu litakavyohifadhiwa baada ya miaka 15 inayokadiriwa-licha ya muda wa mradi kuwa miaka 25 na jinsi taka hiyo itakavyofanywa baada ya kufungwa kwa kiwanda.

Mwisho, ESIA ya 2016 haijaeleza jinsi itakapodhibiti hewa itakayotoka kwenye hifadhi la jivu-jambo ambalo limejadiliwa zaidi katika sehemu ya III.D.4 hapo chini.[204]

### *3. Uharibifu wa huduma za viumbehai*

IFC PS imeagiza ulinzi maalumu kwa ajili ya huduma za viumbehai: manufaa ya viumbehai kwa watu.[205] Manufaa hayo ni pamoja na bidhaa zinazoimarisha chakula, riziki, ama huduma za kitamaduni zisizogusika.[206] Pamoja na jukumu la jumla la kupunguza athari za huduma za viumbehai, IFC PS ina maagizo muhimu ya kutoluwa na athari kubwa kwa huduma za viumbehai zenye kipaumbele katika jamii zinazohusika, pale ambapo mteja ana udhibiti wa usimamizi wa moja kwa moja au athari kubwa katika huduma hizo za viumbehai.[207] Ikiwa athari hizo haziepukiki, mteja anapaswa kuzipunguza na kutekeleza hatua za kupunguza makali ili kuimarisha thamani na utendakazi wa huduma hizi zenye kipaumbele.

Kama tulivyoeleza, kiwanda cha makaa kinachokusudiwa kina hatari kubwa kwa viumbehai vyenye huduma za kipaumble kwa wanajamii walioathirika katika eneo la Lamu. Jamii nyingi za Lamu bado zinategemea riziki za asili kama vile uvuvi, kukata mikoko, uwindaji na uchumaji, ufugaji wa wanyama, kilimo, utalii wa viumbehai, na kadhalika.[208] Riziki hizi zitaathiriwa na kiwanda cha makaa kinachokusudiwa. Wenyeji wa Lamu wanaeleza hivi:

*"Sisi kama wavuvi na wakataji wa mikoko tunafahamu kwamba baada ya kukamilika, mfumo wa kutia baridi utakaotumiwa na Amu Power utahatarisha viumbe wa baharini kutokana na maji mengi yatakayotolewa baharini ili kutia mashine baridi na maji yenye joto kurudishwa baharini. Mfumo huo wa kutia baridi utasababisha viumbe wengi wa baharini kufa kutokana na mvuto wa maji unaochukua idadi kubwa ya samaki, samakigamba, na mayai yake, na unaowaua kutokana na joto, wasiwasi, na kemikali zinazotumiwa kunadhifisha mfumo wa kutia baridi. Tunafahamu kuwa viumbe wa baharini huenda wakafa au kujeruhiwa wakijikuta wamebanwa na vioo. Tunafahamu pia kuwa mfumo wa kutia baridi utahatarisha misitu yetu ya mikoko kwa sababu itafikiwa na maji machafu yenye joto. Tunasikitika kwamba ekolojia yetu ya pwani itaathirika sana na tutapoteza maliasili yetu, tunayoitegemea kujipatia riziki.*"[209]

[203] 2016 ESIA, Sura 4, 21.
[204] *Contra* EHS Guidelines on Thermal Power Plants, uk. 5 na 12-13.
[205] IFC PS 6, aya. 7.
[206] IFC PS 6, aya. 2.
[207] IFC PS 6, aya. 25.
[208] BCP, §8.1.5.
[209] BCP, §9.1.

"*Sisi, wakulima wa Kaunti ya Lamu, pia tunajua kuwa uchomaji wa makaa unachafua hewa ambayo ni mchanganyiko wa kaboni diokside na kemikali nyingine. Tunafahamu kuwa kukinyesha, mchanganyiko huu unabadilika na kuwa mvua ya aside na inaweza kuangamiza mimea na kudhuru afya ya binadamu. Tuna hofu kuhusu athari hizi mbaya, ambazo tunaelewa zitaangamiza riziki zetu na kudhuru afya zetu.*"[210]


*"Maliasili yetu …ni sumaku kwa utalii. Tuna watalii wanaokuja Lamu ili kuona utamaduni wa jadi wa Waswahili… Pia wanakuja kuona fukwe zetu, kuogelea katika maji yetu safi na kusafiri katika dau zetu."*[211]

"*Misitu ya mikoko ni ya thamani kubwa ya kiekolojia na kiuchumi hapa Lamu. Ndipo viumbe wengi wa baharini wanapolea wanao wachanga lakini pia ina thamani kiuchumi.*"[212]

Kama inavyoonyeshwa katika mchoro 7, zoezi la ramani ya jamii ya rasilmali lililofanywa na Save Lamu mnano 2014 – 2016 linadhihirisha kuwa mna rasilmai nyingi  muhimu za kiasili na kitamaduni katika eneo la kiwanda cha makaa na maendeleo mengine yanayohusiana na kiwanda hicho.

[210] BCP, §9.1.7.
[211] BCP, §6.6
[212] BCP, §8.1.4.

**Mchoro 7: Rasilmali za kiasili na kitamaduni za Lamu**




*Chanzo: Ramani ya Jamii ya Rasilmali za Kiasili na Kijamii katika Lamu, Nyongeza 6*

ESIA ya 2016 inaeleza kwa jumla kwamba baadhi ya huduma za viumbehai zinazonufaisha wanajamii zinaweza kuangamizwa au kupunguzwa kutokana na shughuli za mradi, endapo, hakuna tathmini ya kina kuhusu kiwango au upeo wa athari ama kipaumbele chake kwa jamii zinazohusika.[213] Jedwali 8-33 ya ESIA inadai kutathmini namna huduma za viumbehai zitakavyoathiriwa na mradi. Kwa mfano, kama ilivyoelezwa hapo juu, viumbe vya baharini huenda vikaathiriwa pakubwa na vipengele fulani vya muundo wa kiwanda cha makaa ambao bado haujaeleweka vyema, kama vile utupaji wa maji ya kutia baridi yaliyotumiwa kwenye mazingira ya baharini, na kushikwa kwa viumbe ndani ya mfumo wa maji ya kutia baridi.

Taratibu hizi huenda zikawa na athari kwa samaki na riziki zinazohusiana na samaki kwa jumla. Hata hivyo, hatari zake hazijatathminiwa na si wazi kama ziliwekwa ndani ya muhtasari wa ESIA wa ukurasa mmoja kuhusu athari za huduma za viumbehai. Japo ni vigumu kujua kabisa athari za mradi kwa huduma za viumbehai kwa kutegemea tathmini ya ESIA, Mahakama ya Juu ya Kenya hivi majuzi iliagiza Kshs Bilioni 1.7 zilipwe kama fidia kwa wavuvi 4,700

[213] 2016 ESIA, Sura 8, §8.10.1.

walioathiriwa na ujenzi wa bandari ya Lamu.[214] Kiwanda cha makaa kitakuwa na athari mbaya kama hizo kwa maelfu ya wavuvi, pamoja na athari kwa wakulima na watu wengine wanaotegemea maliasili katika eneo la mradi.

Isitoshe, ESIA inatambua hatua mbili tu za kupunguza makali ya athari hizi:  kuunga mkono juhudi za kubuni vyanzo vingine vya riziki mbadala katika jamii, na kuunga mkono sharia za uvuvi ili kuzuia uvuvi uliokithiri na kuvua katika sehemu zilizolindwa.[215] Hatua hizi mbili ni za jumla mno na ni vigumu kuzitekeleza. Hakuna maelezo kuhusu namna mradi utakavyounga mkono juhudi za riziki wala kutathmini kama riziki mbadala zilizoorodheswa zitakuwa zinafaa kwa  uvuvi, ambaoo ni shughuli muhimu zaidi katika kaunti hii. Haiwekani kutathmini vya kutosha kama mpango wa riziki mbadala unafaa bila taarifa zaidi.

Fauka ya hayo, hatua hizi za kupunguza makali haziwezi kuimarisha huduma za viumbehai kwa manufaa ya wanajamii. Badala yake, zote zinaonyesha mkakati wa kumaliza au kupunguza uvuvi wa jadi katika eneo la mradi. Jambo hili litaathiri riziki za jamii na pia maarifa ya jadi na turathi za kitamaduni. Mbajuni mmoja anaeleza kwamba upotezaji wa turathi za kitamaduni tayari unatokea; upotezaji utakaoongezeka kadri wakazi watakavyoondolewa katika riziki zao za jadi. “Zamani tulijua namna ya kutengeneza dau vyema, lakini maarifa haya yanapotea…”[216]

Pamoja na kuwa mkabala huu haujakamilika, haufuati viwango vya kupunguza makali vilivyokisiwa na IFC PS vinavyoagiza kuwa uepushaji wa athari upewe kipaumbele na hatua zingine kama ulipaji fidia ziwe za mwisho. Hatimaye, mkabala wa ESIA wa hatua za kupunguza makali hautekelezi wajibu wa “*Kuimarisha thamani na utendakazi wa huduma za viumbehai zinazoathiriwa*.”[217]

### 4. *Tathmini ya msingi kuhusu hali ya hewa ina upungufu na uchafuzi wa hewa haujatathminiwa ipasavyo*

Kama tulivyotaja hapo juu, IFC PS3 inaagiza kwamba, katika duara ya mradi, mteja afuate kanuni na mbinu za kiufundi na kifedha zenye ufanisi:  ziwe bora katika uzuiaji wa uchafuzi na athari kwa afya na mazingira ziwe chache, endapo si rahisi kuepukika.[218] Utaratibu wa kutambua hatari na athari utumie data za msingi za hivi karibuni.[219]

#### a) *Tathmini ya msingi ya hali ya hewa ina makosa na athari za uchafuzi wa hewa hazijatathminiwa ipasavyo*

---

[214] *Mohamed Ali Baadi and others v. the Attorney-General and others* (No. 22 of 2012) High Court of Kenya (Judgment dated 30 Apr. 2018) https://www.elaw.org/ke_LAPSSET_Summary_30April2018. Hukumu imefika mahakama ya rufani, na fidia bado haijatolewa, na jambo hili limeleta fadhaiko na tuhuma katika jamii.
[215] 2016 ESIA, Sura 8, Jedwali 8-33.
[216] BCP, §6.1.
[217] IFC PS 6, aya 25.
[218] IFC PS 3, aya. 4.
[219] IFC PS 1, aya. 7.

Tathmini ya kina na ya kuaminika ni muhimu sana ili kupima athari za uchafuzi wa hewa katika utekelezaji wa mradi. Tathmini ya msingi ya uchafuzi wa hewa katika mradi huu ilifanywa kwa kutumia mbinu dhaifu ya sampuli na ina matokeo yasiyotegemewa. Hali hii inahatarisha tathmini zote zilizofanywa kuhusu mradi huu kwa kutumia data hii. Matokeo yake yanazua maswali mengi na wataalamu wengi wamesema "hayawezekani kamwe."[220] Kwa mfano, Ripoti ya Ufuatiliaji wa Mtawanyiko Hewani [*Atmospheric Dispersal Monitoring Report*] inaeleza kwamba athari za uchafuzi wa hewa zilihesabiwa kwa kujumlisha uzito wa hewa-chafuzi itakayowezekana na hewa-chafuzi iliyopo (ya msingi).[221] Uzito utakaotokea baada ya ujumlishaji wa chembechembe hizi sharti uwe wa chini ya kiwango fulani. Katika hali hii, hewa chafuzi iliyopo (ya msingi) ilifahamika kutokana na kukusanya sampuli za chembechembe kwa masaa manne kwa kipindi kimoja katika maeneo kumi ya ufuatiliaji.[222] Kipindi kimoja cha masaa manne ni muda mfupi sana wa kuweza kutoa maelezo ya uzito wa chembechembe.[223] Njia ya kawaida ya kutambua uzito wa chembechembe umefafanuliwa na Tathmini ya Athari kwa Mazingira (*Environmental Impact Assessment*) kwa ajili ya migodi ya makaa ya India: "Muda wa kupata sampuli za PM10, PM2.5, SO2, na NO2 ulikuwa wa masaa ishirini na manne mfululizo kila siku na CO na Ozoni zilifanyiwa sampuli kwa muda wa masaa nane mfululizo mara tatu kwa kipindi cha masaa ishirini na nne cha ufuatiliaji. Ufuatiliaji ulifanywa siku mbili kila juma kwa miezi mitatu.[224]

Kwa hali hii, muda usiotosha wa majaribio ulisababisha vipimo vya chini na visivyoaminika vya uchafuzi katika tathmini ya misingi. Rekodi za ESIA za uzito wa PM2.5 na PM10 viko chini ya 1µg/M$^2$ katika kila eneo la ufuatiliaji.[225] Hata katika mazingira bora, chembechembe za uzito hewa za PM2.5 kwa kawaida huwa baina ya 5-10 µg/M$^3$.[226] Ijapokuwa inawezekena kwamba chembechembe za hewa chafuzi zilizorekodiwa katika eneo la kiwanda ziko sahihi, tukijumlisha muda mfupi wa kuchukua sampuli na matokeo ya chini yasiyoaminika tunakuwa na maswali mengi kuhusu uchanganuzi wa hali ya hewa ya msingi.

Pia kuna tofauti kubwa katika ripoti ya ufuatiliaji wa hali ya hewa ya msingi zinazopatikana katika nyongeza. Kwa mfano, Nyongeza 14a na 14b zinatoa taarifa kwamba kuwepo kwa PM2.5 katika kijiji cha Bargoni kulikochunguzwa kwa takribani masaa manne mnamo Januari 10, 2015 kulionyesha wingi wa 17,917 µg/M$^3$,[227] wakati nyongeza 2 inatoa taarifa kuwa wingi wa PM2.5 katika eneo hilo kwa kipindi cha masaa manne baina ya Januari 10 na Februari 17, 2015 ni 18.0

---

[220] Taarifa ya shahidi Mark Chernaik, 4.1 iliyoambatwa katika Nyongeza 3.
[221] 2016 ESIA, Kiambatisho 2: Atmospheric Dispersion Modelling Report, §5.7.1 katika 36.
[222] *Id.* katika §3.1, uk. 16; 2016 ESIA Kiambatsho 14A: Baseline Air Quality Assessment Report for the Proposed Lamu Coal Power Plant Project katika 10.
[223] Taarifa ya shahidi Mark Chernaik, 4.1 iliyoambatwa katika Nyongeza 3.
[224] Environmental Impact Assessment for the Proposed Expansion of Parsa East and Kanta Basan Opencast Mine and Pit Head Coal Washery, Chapter 3: Baseline Environment Status, Vimta Labs Limited, 23.
[225] 2016 ESIA Kiambatisho 2 katika 19, Jedwali 3-4 na 3-5.
[226] Kwa mfano, wakati wanasayansi walipoangalia viwango vya msingi vya PM2.5 katika "mazingira ya hali safi kwa jumla katika savana ya Afrika Kusini" ' - hifadhi ya wanyama ya Botsalano, Afrika Kusini, iliyoko kilomita 50 kutoka mji wa karibu- kiwango cha msingi walichokiona kilikuwa 10.5 µg/m3. Laakso, L., Laakso, H., Aalto, P. P., Keronen, P., Petäjä, T., Nieminen, T., ... & Molefe, M. (2008). Basic characteristics of atmospheric particles, trace gases and meteorology in a relatively clean Southern African Savannah environment. *Atmospheric Chemistry and Physics Discussions*, 8(2), 6313-6353, *available at* https://hal.archives-ouvertes.fr/file/index/docid/304062/filename/acpd-8-6313-2008.pdf.
[227] 2016 ESIA, Kiambatisho 14a at 16; Kiambatisho 14b.

μg/M³.[228] Tofauti kama hizi zinaonekana katika maeneo mbalimbali yaliyofanyiwa sampuli. Tofauti kubwa kama hii sharti ichunguzwe na ielezwe kabla ya ripoti kuhuru aina ya hewa kuchukuliwa kwamba inaaminika.

Kwa sababu data ya msingi inaongezwa kwa makisio ya moshi wa kiwanda cha makaa, ili kubainisha athari za kiwango cha hewa, mapungufu haya katika utafiti wa msingi yanahatarisha uchanganuzi mzima wa athari ya vichaguzi katika mradi.

b) *Mapengo katika hatua za kupunguza makali ya athari za uchafuzi wa hewa*

Kama vile ilivyo katika viwanda vyote vya makaa, kiwanda cha makaa cha Lamu kitatoa kemikali nyingi na chembechembe zinazohusika katika athari kali za kiafya na kimazingira, ambazo ni pamoja na salfa diokside ($SO_2$), okside za nitrojeni ($NO_x$), chembechembe (PM) na zebaki.[229]

Licha ya madai kinzani yanayotolewa,[230] kiwanda cha makaa cha Lamu kitatoa moshi kama huo hata endapo teknolojia yake itaboreshwa kutoka ya juu hadi ya juu zaidi (yenye ufanisi), kama ilivyotangazwa na Amu Power na GE. Kwa kulinganisha, kabla ya hatua za upunguzaji, moshi ufuatao ni wa kawaida katika viwanda vya umeme vinavyotumia teknolojia ya juu na teknolojia ya juu zaidi (USC):

**Mchoro 8: Matokeo muhimu ya utendaji kutoka utafiti wa A-USC**

| | Siya juu | Ya juu | Ya sasa | A-USC |
|---|---|---|---|---|
| Ufanisi wa joto, %(HHV) | 36.2 | 38.5 | 39.2 | 42.7 |
| Jumla kiwango cha joto, Btu/kwh (HHV) | 9,430 | 8,860 | 8,700 | 7,990 |
| Kiwango cha kuweka makaa, kg/saa | 384,000 | 361,000 | 355,000 | 326,000 |
| Utokaji wa gesi ya dohani, kg/saa | 3,420,000 | 3,151,000 | 2,098,000 | 2,827,000 |
| Ujazo katika boila, hasa | 66,700 | 61,400 | 60,400 | 55,100 |

[228] 2016 ESIA, Kiambatisho 2, Jedwali 3-4.
[229] Angalia Office of the Compliance Advisor Ombudsman, *CAO Audit of IFC Investment in Coastal Gujarat Power Limited, India*, 31 (22 Aug. 2013).
[230] Tazama, kwa mfano, Kenya News Agency "The 'Pains And Gains' Of Lamu's Mega Projects" (12 Jan. 2019) http://www.kenyanews.go.ke/the-pains-and-gains-of-lamus-mega-projects/.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| $M^3$/dakika | | | | |
| $NO_x$ na $SO_2$, kg/MWh | 0.127 | 0.121 | 0.118 | 0.109 |
| $PM_{10}$, kg/MWh | 0.0422 | 0.0399 | 0.0395 | 0.0363 |
| $PM_{2.5}$, kg/MWh | 0.0535 | 0.0508 | 0.0499 | 0.0458 |
| $CO_2$, kg/MWh | 900 | 851 | 836 | 763 |

*Chanzo: Jeffrey N. Phillips and John M. Wheeldon, "Economic Analysis of Advanced Ultra-Supercritical Pulverized Coal Power Plants: A Cost-Effective CO2 Emission Reduction Option?" Advances in Materials Technology for Fossil Power Plants: Proceedings from the Sixth International Conference, 55, Jedwali 3 (2010).*

Kwa mujibu wa IFC PS3, kiwanda cha makaa cha Lamu kinapaswa kutumia mbinu za kuzuia madhara ya kiafya na kimazingira. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa hapo chini, ESIA ya 2016 haitoi hakikisho kuwa hatua za kupunguza madhara zimechukuliwa.

*Okside ya Nitrojeni ($NO_x$)*

Okside ya Nitrojeni inayotolewa na viwanda vya makaa huchanganyana na kemikali zilizohewani ili kuunda ni ukungumoshi, nitri okside na nitrojeni diokside ($NO_2$).[231] Mchanganyiko huu wa hewa chafuzi husababisha athari za afya, pamoja na ugonjwa wa mkamba hasa miongoni mwa watoto wenye pumu na kupunguza uwezo wa mapafu.[232] $NO_2$ pia inahusishwa na maradhi ya bakteria na maumivu ya kikoromeo na kupumua.[233]

Miongozo ya IFC EHS kuhusu viwanda vya nguvu za umeme imependekeza kwamba kiwanda kichukue hatua ili kupunguza moshi wa $NO_x$, pamoja na kutumia majiko yanayotoa $NO_x$ ndogo.[234] Fauka ya haya, miongozo inapendekeza mabadiliko katika uchomaji kama vile utoaji hewa ya ziada isiyokuwa nyingi na udhibiti mwingine wa $NO_x$ ya ziada katika boila, kwa mfano kwenye mfumo chaguzi wa kupunguza kasi.[235]

Kwa mujibu wa ESIA ya 2016, kiwanda cha makaa cha Lamu kinakusudia kupunguza makali ya moshi wa $NO_x$ kwa kutumia majiko yanayotoa nitrojeni okside ndogo, kama inavyopendekezwa na miongozo.[236] Hata hivyo, haitaji kama hatua za ziada zilizopendekezwa na IFC zitajumuishwa katika muundo. Inataja tu kwamba "mfumo utaundwa ili kufikia au kuzidi miongozo ya kutoa

[231] Erica Burt et. al, "Scientific Evidence of Health Effects from Coal Use in Energy Generation," University of Illinois at Chicago School of Public Health, 6 (Apr. 2013).
[232] World Health Organization, "WHO Air quality guidelines for particulate matter, ozone, nitrogen dioxide and sulfur dioxide: Global update 2005," 16 (2006) [WHO Guidelines].
[233] U.S. Environmental Protection Agency, "Risk and Exposure Assessment to Support the Review of the NO2 Primary National Ambient Air Quality Standard," 31 (Nov. 2008).
[234] EHS Guidelines on Thermal Power Plants, 4.
[235] *Id*.
[236] 2016 ESIA, Sura 4, §4.6.4.

hewa iliyopendekezwa na World Bank Group mnamo 2008."[237] Ni vigumu kujua vile, au kama, miongozo hii itatekelezwa bila taarifa kuhusu hatua hizi za ziada.

*Salfa Dioksidi ($SO_2$)*

Moshi wa salfa dioksidi ($SO_2$) kutoka viwanda vya makaa unahusishwa na athari za kupumua, hasa miongoni mwa watoto wenye pumu.[238] Tafiti zinazohusishwa watu wenye pumu zinaonyesha kwamba kupumua $SO_2$ kwa muda mfupi wa dakika kumi hivi kunaweza kubadilisha utendakazi wa mapafu na dalili za kupumua.[239] $SO_2$ inaweza pia kuchapuza kasi ya ugonjwa na kupunguza maisha katika maeneo yaliyo karibu na viwanda vya umeme.[240]

Miongozo ya IFC kuhusu moshi wa $SO_2$ inapendekeza mafuta ya uchomaji yenye salfa ndogo kadri iwezakanavyo na kutumia teknolojia ya dohani za gesi ya kuondoa salfa (FGD) ili kupunguza moshi wa salfa kutoka kiwandani.[241] Kulingana na ESIA ya 2016, kiwanda cha makaa cha Lamu kitachoma makaa yenye salfa ya baina ya 0.5% na 2.4%[242] na kitakuwa na lengo la kupunguza makali ya moshi wa $SO_2$ kwa kujenga mfumo wa dohani wa chepechepe ya gesi ya kuondoa salfa.[243]

Teknolojia ya FGD hupunguza moshi wa $_{SO2}$ pakubwa, lakini inaweza kuwa na athari zingine ambazo hazijazingatiwa katika ESIA ya 2016.

Katika mchakato wa FGD, moshi wa $SO_2$ utokanao na uchomaji wa makaa huchanganyika na kalsiamu au alikali tenganishi yenye sodiamu na hubadili $SO_2$ na kuifanya kitu kigumu.[244] Kiwanda cha umeme cha Lamu kitatumia mfumo wa maji ya bahari.[245] Viwanda vinavyotumia mfumo huo, maji ya bahari – ambayo kiwanda kitatumia kwa ajili ya kutia baridi – hutumika kama kutenganishi badala ya kemikali zingine za alikali.[246]

Miongozo ya IFC ya Mazingira, Afya na Usalama imesema kwamba mifumo ya maji ya bahari ya FGD ina ufanisi wa hadi asilimia 90% kwa kutoa $SO_2$.[247] Hata hivyo, miongozo hii inatambua kuwa "athari katika mazingira ya baharini sharti ichunguzwe kwa makini (k.m. kupunguza PH, pembejeo za chuma zito zilizobaki, jivu lisilodhibitika, joto la salfeti, oksijeni iliyoyeyushwa, na

---

[237] *Id*.
[238] "Scientific Evidence of Health Effects from Coal Use in Energy Generation," 5.
[239] WHO Guidelines, 18.
[240] Muhammad Ehsan Munawer, "Human health and environmental impacts of coal combustion and post-combustion wastes," 17 *Journal of Sustainable Mining* 87, 88 (22 Dec. 2017).
[241] EHS Guidelines on Thermal Power Plants, 4.
[242] Wingi wa salfa wa zaidi ya asilimia 1% huchukuliwa ni wa kiwamgo cha chini, lakini wingi wa asilimia 1.3% ni wa wastani. Wingi wa salfa wa zaidi ya asilimia 3% ni wa juu. Stanley P. Schweinfurth, "An Introduction to Coal Quality," The National Coal Resource Assessment Overview, 2 (2009). Kwa msingi huu, makaa yaliyochomwa katika kiwanda cha Lamu yatakuwa na salfa baini ya kiwango cha chini na wastani.
[243] 2016 ESIA, Sura 8, §8.2.2.
[244] U.S. Environmental Protection Agency, "Air Pollution Control Technology Fact Sheet," 3, https://www3.epa.gov/ttncatc1/dir1/ffdg.pdf.
[245] 2016 ESIA, Sura 4, §4.4.
[246] Katsuo Oikawa et. al, "Seawater flue gas desulfurization: Its technical implications and performance results," 22 *Environmental Progress* 67, 67 (20 Apr. 2004).
[247] EHS Guidelines on Thermal Power Plants, 4.

mahitaji ya oksijeni ya kemikali).[248] ESIA haibainishi athari hizi mbalimbali zinazohusiana na mfumo wake wa FGD. Taarifa zaidi inahitajika ili kufahamu kama teknolojia za kiwanda cha Lamu za kupunguza $SO_2$ zitaathiri viumbehai vya mikoko ya pwani.

Isitoshe, utafiti wa majuzi uligundua kuwa wingi wa zebaki karibu na milango ya maji ya bahari katika mfumo wa FGD uko juu ulinganishwapo na ule wa kituo upimaji kilichoko kilomita 2.5 na kilomita 8 kutoka kiwandani, mtawalia.[249] Fauka ya hayo, kulionekana uhamishaji wa zebaki kutoka majini kuingia hewani.[250] Utafiti ulihitimisha, "Uchafuzi wa Hg katika mazingira ya bahari sharti … uwe wa kutia hofu na kuwe na ufuatiliaji wa muda mrefu.[251] ESIA haitoi maelezo kuhusu jambo hili. Japo inatambua zebaki ni tokeo la uchomaji makaa, inabainisha kuwa mifumo ya moshi (pamoja na FGD, vitenganishi umeme, na lundo la moshi) itatosha kuzuia makali ya moshi wenye zebaki.[252]

Kwa mujibu wa matokeo haya, japo teknolojia ya FGD huenda ikapunguza makali ya moshi wa SO2 kutoka kiwanda cha umeme wa makaa kwa ufanisi, huenda ikaharibu zaidi. Tathmini zaidi za athari zinahitajika ili kufahamu upeo wa athari hizi katika muktadha wa Lamu.

*Chembechembe*

Chembechembe hewani (PM) zina chembechembe ndogo za uchafuzi uliochanganyika na maji. PM zenye upana wa chini ya au kama 2.5mm (PM2.5) husababisha matatizo ya afya miongoni mwa binadamu. Viwanda vya umeme vya mafua ya visukuku hutoa PM2.5 kupitia njia mbili: hutoa PM2.5 moja kwa moja kama tokeo la uchomaji na pia $NO_x$ na $SO_x$, ambazo huchanganyika na kemikali zingine hewani kutengeneza aina ya PM2.5.[253] Aina hii ya mchango inaitwa uundaji wa upili wa chembechembe.[254]

Uundaji wa upili wa chembechembe ndio mchango mkubwa zaidi wa viwanda vya umeme wa makaa katika uchaguzi wa PM2.5, unaosababisha zaidi ya asilimia 90% ya watu kufikiwa na chembechembe. Mtaalamu wa uchafuzi wa hewa aliyepima hali ya hewa katika jaribio la kiwanda cha Lamu aliona kwamba uchafuzi wa hewa uliofanywa katika jaribio la kiwanda cha Lamu ulishindwa kukisia vilivyo kiwango cha athari za uchafuzi wa chembechembe za upili, kwa sababu kipimo cha PM2.5 hakikuzingatiwa katika jaribio.[255] Kwa sababu utengenezaji wa chembechembe za upili ulipunguzwa na ESIA, wingi wa msingi wa PM2.5 kutoka moshi wa kiwanda cha umeme kinachokusudiwa huenda umewekwa katika kiwango cha chini.

---

[248] *Id*.
[249] Liu et. al, "Mercury distribution in seawater discharged from a coal-fired power plant equipped with a seawater flue gas desulfurization system," 18 *Environmental Science and Pollution Research International* 1324, 1324 (Sept. 2011).
[250] *Id*. at 1331.
[251] *Id*.
[252] 2016 ESIA, Sura 8, §8.10.3.1.
[253] Jonathan J. Buonocore et. al, "Using the Community Multiscale Air Quality (CMAQ) model to estimate public health impacts of $PM_{2.5}$ from individual power plants," 68 *Environment International* 200, 200 (2014).
[254] Sander, S.P., Seinfeld J.H., 1976. Chemical kinetics of homogeneous atmospheric oxidation of sulfur dioxide Environmental Science and Technology 10, 1114–1123. See also Richards L.W., 1983. Comments on the oxidation of NO2 to nitrate: day and night Atmospheric Environment, 17, 397–402.
[255] Lauri Myllyvirta, *Save Lamu & Ors v National Environment Management Authority & Anor* (2016) NET Appeal 196/2016.

Moshi wa $PM_{2.5}$ unahusishwa na athari nyingi za afya, pamoja na " magonjwa ya kifua, saratani ya mapafu, na maradhi mengine ya kupumua na matokeo yake."[256] Kwa hakika takribani asilimia tatu ya vifo vinavyohusiana na hali ya moyo na mapafu, na asilimia tano ya vifo kutokana na saratani ya mapafu husababishwa na chembechembe hewani duniani. .[257] $PM_{2.5}$ ina athari kubwa kutokana na hatari za muda mfupi na za muda mrefu.[258] Utafiti wa majuzi ulionyesha kuwa $PM_{2.5}$ hewani ilikuwa ya kiwango cha tano katika katika hatari za maisha mnamo 2015 na ilihusishwa na vifo vya watu takribani milioni 4.2 duniani.[259]

ESIA ya 2016 inasema kwamba Vitenganishi vya Umeme (ESO) vitatumika ili kushika chembechembe kutoka dohani na vipokea moshi, bila kubainisha teknolojia mahususi itakatotumika.[260] Vitenganishi vya umeme vinaweza kuwa na ufanisi katika kupunguza chembechembe chafuzi, hata vikiwa vidogo kiasi gani.[261] Hata hivyo, ijapokuwa ESP zingine zina ufanisi wa hadi asilimia 99.5% katika kutoa chembechembe kwa jumla, hazina ufanisi mkubwa katika kuondoa chembechembe za kiwango cha PM2.5 na ndogo zaidi, ambazo ni hatarishi zaidi kwa afya ya binadamu.[262] Kwa bababu ya ukosefu wa maelezo ya kina katika ESIA ya 2016, haijulikani ufanisi wa ESPs katika kiwanda cha makaa cha Lamu utakuwa wa kiwango gani.

Hatimaye, mtalaamu wa uchafuzi wa hewa anashauri kuwa, kinyume na mkabala wa majaribio uliotumika na ESIA, uhatarishi mwingi wa watu utatokea zaidi katika eneo la umbali wa kilomita 100km kwenye vituo kama vile Garissa na Voi.[263] Tafiti zilizofanywa katika viwanda vingine kwa kutumia majaribio kama hayo ya ESIA zilibanisha kuwa katika vyanzo vingi, umbali wa kilomita elfu moja kutoka eneo la kiwanda ulihitajika ili kupata asilimia 50% ya hatari ya uchafuzi wa PM2.5 kutokana na moshi.[264] Eneo la kilomita 50km x 50km, kama katika jaribio la ESIA ya Lamu, halitoshi kamwe, kwa sababu linawakilisha asilimia 0.1% pekee ya eneo la umbali wa kilomita 1000km.

*Zebaki*

Mwako wa makaa unachangia asilimia 24% ya zebaki ya angani kimataifa. Jambo hili linaufanya mwako wa makaa kuwa chanzo cha pili cha shughuli za binadamu zinazozalisha zebaki katika

[256] Sarah Penney et. al, "Estimating the Health Impacts of Coal-Fired Power Plants Receiving International Financing," Environmental Defense Fund, 2 (2009).
[257] World Health Organization, "Health Effects of Particulate Matter: Policy implications for countries in eastern Europe, Caucasus, and central Asia" (2013) http://www.euro.who.int/__data/assets/pdf_file/0006/189051/Health-effects-of-particulate-matter-final-Eng.pdf.
[258] WHO Guidelines, 9.
[259] Aaron J. Cohen et. al, "Estimates and 25-year trends of the global burden of disease attributable to ambient air pollution: an analysis of data from the Global Burden of Diseases Study 2015," 389 *The Lancet* 1907, 1907 (13 May 2017).
[260] 2016 ESIA, Sura 4, §4.3.
[261] David Hosansky, "Electrostatic Precipitator," *Green Technology: An A-to-Z Guide*, ed. Dustin Mulvaney and Paul Robbins at 154-155.
[262] Hu Bin et. al, "$PM_{2.5}$ and $SO_3$ collaborative removal in electrostatic precipitator," 318 *Powder Technology* 484, 484 (1 Jun. 2017).
[263] Lauri Myllyvirta and Clifford Chuwah, *Assessing the Air Quality, Toxic and Health impacts of the Lamu Coal-Fired Power Plant* (Greenpeace, 2017) http://accountabilitycounsel.org/wp-content/uploads/2017/11/FINAL-Air-Quality-toxic-and-health-impacts-modelling-study-of-the-Lamu-Coal-Plant.pdf.
[264] Zhou Y et al 2006. The influence of geographic location on population exposure to emissions from power plants throughout China. Environment International 32, 365–373.

uchimbaji mdogo wa dhahabu.[265] "Makaa hayana viwango vya juu vya zebaki. Lakini, mchanganyiko mkubwa wa makaa yanayochomwa na sehemu kubwa ya zebaki iliyopo katika makaa na inayotolewa angani inazalisha kiwango kikubwa kutokana na hali hii."[266]

Zebaki inahusishwa na athari mbaya ya afya kwa binadamu, ikiwa ni pamoja na athari za neva, kama vile "kupoteza kumbukumbu, hisia mbaya, huzuni kubwa, hasira, kukasirika ovyo / ghadhabu / ukatili, kujidunisha, mawazo ya kujiua, na ukosefu wa nguvu ili kuzuia wasiwasi au shauku au kupinga ushurutishwaji.[267] " Pia huathiri afya ya figo, mfumo wa mishipa ya moyo , na kusababisha utasa.[268]

Njia ya msingi ambayo wanadamu hupata zebaki ni kula samaki.[269] Hii ni shida kubwa kwani - kama ESIA inavyokiri - uvuvi wa bahari ni shughuli ya pili kwa ukubwa katika uchumi wa Lamu; asilimia 75% ya samaki ni wa mwitu - waliovuliwa kutoka mazingira ya karibu na bahari.[270] Takwimu moja ya kutisha juu ya nguvu za zebaki ni kwamba, "tone moja, 1/70 ya kijiko cha zebaki inaweza kuharibu ziwa la ekari 25 hivi kwamba samaki wanakuwa hatarini wanapokula."[271] Ingawa mazingira ya baharini yaliyo karibu na mradi wa Lamu ni tofauti na ziwa lisilovuja, na zebaki itasambazaa maeneo mbalimbali, athari za zebaki katika eneo la mradi zinapaswa kuchambuliwa zaidi kutokana na athari zake katika uvuvi na afya ya binadamu.

Zebaki huzalishwa na mwako wa makaa kama mvuke (asilimia 90% ya uzalishaji wa zebaki) na majivu ya makaa (10% ya uzalishaji wa zebaki).[272] Ingawa zebaki ya majivu ya makaa inaweza kuondolewa kwa kutumia vifaa vya kudhibiti chembe, zebaki ya mvuke ni ngumu kuondolewa.[273]

Miongozo ya IFC inapendekeza kupunguza uzalishaji wa zebaki kwa kutumia teknolojia ya kupunguza ESPs na FGD.[274] Hata hivyo, teknolojia hizi haziwezi kupunguza uzalishaji wa zebaki hatari: "ESPs haiwezi kuwa kifaa mwafaka cha kudhibiti isipokuwa [zebaki] iwe imetoneshwa kuwa chembechembe wakati ama kabla ya kutumia kifaa hicho."[275] ESIA 2016 haina taarifa yoyote kufafanua kama zebaki kutoka kiwanda cha Lamu itatoneshwa na kuwa chembechembe kabla ya kufika kiwanda cha ESPs. Teknolojia zingine, kama "kitambaa cha

[265] UN Environment Programme, "Global Mercury Assessment," 9 (2013).
[266] *Id*. at 6.
[267] Ki-Hyun Kim et. al, "A review on the distribution of Hg in the environment and its human health impacts," 306 *Journal of Hazardous Materials* 376, 381 (2016).
[268] *Id*. at 381-82.
[269] V.M. Fthenakis et. al, "An assessment of mercury emissions and health risks from a coal-fired power plant," 44 *Journal of Hazardous Materials* 267, 279 (1995).
[270] 2016 ESIA, Chapter 5, §5.11.7.3.
[271] Patricia Glick, "The Toll from Coal: Power Plants, Emissions, Wildlife, and Human Health," 21 *Bulletin of Science, Health, and Society* 482, 487 (Dec. 2001).
[272] "An assessment of mercury emissions and health risks from a coal-fired power plant," 271.
[273] *Id*.
[274] EHS Guidelines on Thermal Power Plants, 6.
[275] "An assessment of mercury emissions and health risks from a coal-fired power plant," 272.

kuchungia, " zina ufanisi zaidi.[276] ESIA ya kiwanda cha Lamu haitoi taarifa yoyote ya teknolojia ya kitambaa cha kuchungia.

Zaidi ya hayo, FGDs ya maji ya bahari (aina ya mfumo wa kuondoa salfa uliopendekezwa kwa kiwanda cha Lamu) imeonyeshwa kutoa viwango vya juu cha zebaki chimbukoni, kama ilivyojadiliwa hapo juu. ESIA ya 2016 inashindwa kushughulikia athari hii.

Kutokana na hatari mbaya za afya zinazohusiana na uzalishaji wa zebaki, habari zaidi juu ya upunguzaji wake ni muhimu.

*Utoaji wa taka kutoka yadi ya makaa haujatathminiwa vizuri*

Pamoja na hatari zingine zinazotokana na hifadhi ya majivu ya makaa (iliyojadiliwa katika sehemu ya III.D hapo juu), ESIA ya 2016 inashindwa kutathmini kiasi au athari zinazoweza kutokana na taka ya makaa na majivu ikieleza tu kwamba "hakuna taarifa ya kutosha wala data ya kuaminika" ili kujua athari kamili.[277] Kutokana na taarifa ya ESIA kwamba kiwango cha makaa cha kuhifadhiwa katika eneo la mradi (hadi 420,000 za tani),[278] uamuzi wa kukosa kukadiria kiasi cha utoaji taka hauthibitiki.[279]

*Mvua ya asidi*

ESIA inakubali kuwa kiwanda cha nguvu za umeme cha Lamu pia kinaweza kudhuru mazingira kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja kupitia mvua ya asidi.[280] Kwa kweli, tafiti nyingi zimethibitisha kwamba uzalishaji wa Okside ya Nitrojeni na Salfa Dioksidi($NO_x$ na $SO_2$ ) kutoka kwa kiwanda cha makaa unachangia pakubwa katika mvua ya asidi.[281] Ingawa ESIA inabainisha kwamba mvua ya asidi ni tishio kwa mimea na mfumo wa ekolojia ya majini, haizingatii athari kwenye Lamu Old Town,eneo ambalo ni Turathi ya Kimataifa ya UNESCO.

"Athari ya kuacha asidi kwenye minara ya wa mawe iliyojengwa kwa marumaru na chokaa na vifaa vya ujenzi vyenye kiasi kikubwa cha kaboneti imeshuhudiwa kwa zaidi ya karne."[282] Asidi ya salfa na nitriki huchanganyika na kalsite katika vifaa hivi, na kuviyeyusha.[283]

---

[276] U.S. Environmental Protection Agency, “Control of Mercury Emissions from Coal Fired Electric Utility Boilers: An Update,” Air Pollution Prevention and Control Division, National Risk Management Research Laboratory White Paper, 5 (18 Feb. 2005).
[277] 2016 ESIA, Kiambatisho 4: Climate Change and GHG Specialist Study, 49.
[278] 2016 ESIA, Sura 4, §4 katika 15.
[279] *Tazama* pia Taarifa ya shahidi Dr. David Obura katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environment Tribunal), Nairobi, imeambatwa katika Nyongeza 3.
[280] 2016 ESIA, Sura 8, §8.10.2.4.
[281] Anita Singh na Madhoolika Agrawal, “Acid rain and its ecological consequences,” 29 *Journal of Environmental Biology* 15, 15 (Jan. 2008).
[282] *Id*. katika 21.
[283] U.S. Geological Survey, “How does acid precipitation affect marble and limestone buildings?” https://www.usgs.gov/faqs/how-does-acid-precipitation-affect-marble-and-limestone-buildings?qt-news_science_products=0#qt-news_science_products.

Majengo ya kihistoria ya Lamu Old Town itaathirika zaidi: vifaa vya ujenzi vilivyotumika katika majengo mengi hujumuisha chokaa na matumbawe.[284] Chokaa ina kalsiamu na haidrojeni,[285] wakati matumbawe yana mabaki ya kalsiamu kaboneti chache iliyotokana na maotea.[286] Matokeo yake ni kwamba vifaa vya ujenzi vya chokaa na matumbawe vina hatari kubwa ya kuharibiwa kutokana na mvua ya asidi.

Licha ya hayo, ESIA haijataja njia zozote maalumu za kupunguza madhara ya mvua ya asidi katika mji wa Lamu Old Town.

Kwa sababu zote zilizotajwa hapo juu, uchambuzi wa athari za uchafuzi wa hewa katika ESIA hautoshi kukidhi majukumu magumu ya kutambua hatari za uchafuzi, uzuiaji na upunguzaji kama ilivyoagizwa na IFC PS 3, 4 na 6.

### 5. *Tathmini ya athari ya mabadiliko ya hali ya anga*

Mbali na majukumu ya kupambana na uchafuzi ambao tayari umejadiliwa, IFC PS 3 pia inahitaji mteja kuzingatia njia mbadala na kutekeleza mbinu zinazowezekana na za gharama ya chini zinazoweza kupunguza uzalishaji wa gesi (GHG) katika awamu za uandaaji na uendeshaji wa mradi.[287]

Ukame wa hivi majuzi uliotokea nchini Kenya ni dhihirisho la uathirikaje wa mabadiliko ya hali ya anga nchini. Watu wa Lamu wanahofia kuathirika zaidi:

> *"Sisi tunaathirika sana na hatari za hali ya anga kutokana na kwamba tegemeo letu ni rasilmali asili kwa ajili ya chakula, mafuta, na makazi. Hivi sasa, maeneo yetu nchini Kenya ni mojawapo ya yale yanayoathirika kutokana na ukame unaochochewa na mabadiliko ya hali ya anga kama inavyoaminiwa na wataalamu. Tunajitahidi kukabiliana na hali hii mbaya. Kwa hivyo, tunapingana na ujenzi wa kiwanda cha makaa huko Lamu kwa sababu tunaamini makaa yatadhuru hali yetu zaidi. "*[288]

Ripoti ya Mabadiliko ya Hali ya Anga na Ripoti ya Kitaalamu ya GHG inasema kwamba Kiwanda cha makaa cha Lamu kitaongeza uchafu wa GHG nchini kwa baina ya asilimia 6% hadi asilimia 10%.[289] Taarifa ya Miradi ya Kenya ya Mchango Fafanuzi Inayokusudiwa Kitaifa, ya 2015, inakisia kwamba moshi utaongezeka kitaifa kwa takribani asilimia 3.4% kila mwaka hadi 2030,[290] kwa hivyo, kiwanda hiki peke yake kitachangia takribani maradufu ya uzalishaji mwingine pamoja: chaguo lisilofaa wakati nchi inahitajika, na imejitolea, kupunguza uzalishaji wa GHG kwa jumla na ukuaji wa makadirio katika uzalishaji wake. Tokeo hili ni kinyume na

---

284 UNESCO, "Lamu Old Town" https://whc.unesco.org/en/list/1055.
285 "Calcium Hydroxide," Encyclopaedia Britannica https://www.britannica.com/science/calcium-hydroxide.
286 National Oceanic and Atmospheric Administration, "How Do Corals Grow? What Forms Do They Take?" (6 Jul. 2017) https://oceanservice.noaa.gov/education/kits/corals/coral03_growth.html.
287 IFC PS 3, aya. 7.
288 BCP, §9.1.7.
289 2016 ESIA Kiambatisho 4, §7.5.
290 Ministry of Environment and Natural Resources, *Kenya's Intended Nationally Determined Contribution* (23 Jul. 2015) http://www.environment.go.ke/wp-ontent/uploads/2015/07/Kenya_INDC_20150723.pdf.

mkondo wa maendeleo wa kaboni ndogo na maendeleo endelevu uliofafanuliwa katika Mpango wa Kitaifa ya Mabadiliko ya Hali ya Anga na unakiuka maamuzi ya Kenya chini ya Mkataba wa Paris.[291]

Fauka ya hayo, ni muhimu kutambua kwamba Ripoti ya Mabadiliko ya Hali ya Anga na Ripoti ya Kitaalamu ya GHG iliandaliwa "baada ya kukamilika kwa ESIA",[292] na kwa hivyo matokeo yake ni kwamba, "ni tathmini za nyaraka tu zilizowezekana.[293]

Ripoti ya Mabadiliko ya Hali ya Anga na Ripoti Kitaalamu ya GHG ina vipengele viwili. Hata hivyo hakuna kinachozungumzia kwa kina athari za mabadiliko ya hali ya anga kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha makaa ikilinganishwa na ujenzi mbadala wenye uchafuzi wa chini:

- Kipengele cha kwanza - tathmini ya hatari ya hali ya anga - ni tathmini ya hatari zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya anga kwa mradi,[294] kinyume na hatari za hali ya anga zinazofanywa na mradi huo.
- Kipengele cha pili - tathmini ya GHG – mna mapendekezo machache sana kuhusu namna *kiwanda cha makaa* kitakavyopunguza mkondo wa GHG, kama "sifa za ujenzi wa kijani" katika muundo wa ofisi na malazi.[295] Hata hivyo, kipengele hiki hakina mapendekezo sahihi kuhusu chanzo cha uzalishaji wa GHG: yaani, mwako wa makaa. Hakijumuishi mapendekezo ya mwako ulio na ufanisi zaidi.[296] Pia, hakijajumuisha tathmini mbadala za nishati au hali isiyo ya mradi. Aidha, kipengele hiki hakijafafanua jinsi uzalishaji wa GHG kutoka kwa kiwanda cha makaa hatimaye utachangia mabadiliko ya hali ya anga katika eneo hilo.[297]

Hatimaye, ESIA inashindwa kutambua kwa usahihi au kupunguza makali ya athari za mabadiliko ya hali ya baada ya kujengwa kiwanda cha makaa kilichopendekezwa.

### E. Upeo wa watu kuhamishwa na uchumi kubadilishwa umesitiriwa au kupuuzwa

Pamoja na hatari kubwa za kimazingira zilizojadiliwa hapo juu, huenda maelfu ya watu, ikiwa ni pamoja na wanachama wa jamii asili, wakahamishwa kutoka mashamba yao na rasilimali zingine za asili kutokana na kiwanda cha makaa cha Lamu na miundombinu inayohusiana nacho. Wafugaji wa nyuki, wawindaji na wakusanyaji, wavuvi, waendeshaji wa utalii na wavunaji wa mikoko pia wanakabiliwa na athari mbaya za maisha kutokana na mipaka ya upatikanaji wa rasilimali zilizopo, pamoja na mabadiliko makubwa ya mazingira na utamaduni wa eneo pana. Baadhi pia watapoteza makazi ya muda wakati wa kutumia ardhi.

---

[291] Tazama pia barua za Maseneta wa Marekani kwa Rais wa African Development Bank Group na Katibu Mtendaji za Mei 28, 2018, zimeambatwa katika Nyongeza 5.
[292] 2016 ESIA Kiambatisho 4, §2.1.
[293] 2016 ESIA Kiambatisho 4, §2.3.
[294] 2016 ESIA Kiambatisho 4, §1.1.2 ("This Climate Change Specialist Study has the following objectives: Undertake a high level assessment of the physical risks facing the development, such as high temperatures, floods, strong winds, monsoons etc, and identify adaptation measures that could reduce the risk or take advantage of opportunities") na §2.1.
[295] 2016 ESIA Kiambatisho 4, §8.
[296] 2016 ESIA Kiambatisho 4, §§1.1.2, 3.1.1 na 8.
[297] *Id. Tazama pia* 2016 ESIA Kiambatisho 4, §3.3.

Licha ya ukali wa athari hizi, cha kushangaza ni kwamba ni taarifa chache tu zinazopatikana kuhusiana na upeo wa uhamisho na mipango ya hatua za makao mapya. ESIA ya 2016 inashindwa kuchambua masuala ya makao mapya kwa undani, na Mpango wa Utekelezaji wa Makao Mapya (*Resettlement Action Plan -RAP*) bado haujatolewa. Kufikia sasa, zaidi ya miaka miwili baada ya kutolewa kwa ESIA, RAP kamili haijatolewa (ni muhtasari usiokamilika uliolenga wanajamii unapatikana). Bila taarifa kamili jamii zilizoathirika hazina ufahamu wa kina kuhusu athari za uhamisho zinazotokana na mradi (ikiwa ni pamoja na taarifa sahihi ya kiasi cha ardhi inayonyakuliwa na idadi ya familia zitakaoathirika) na hatua zilizopendekezwa za kupunguza makali pamoja na fidia.  Ingawa muhtasari wa RAP unapatikana,[298] waraka huo usiokuwa na tarehe una upungufu, ni vigumu kuuelewa na hautoshi kutathmini upeo kamili wa uhamisho na hatua zilizopangwa za kupunguza makali na kutoa fidia. Upungufu huu unazua wasiwasi mkubwa na hofu kwa wale waliohamishwa, baadhi yao wakiwa wameacha kuimarisha mashamba yao bila kulipwa fidia, kwa sababu hakuna matumaini ya baadaye.[299] Pia, upungufu huo unawaruhusu wahuni kudai ardhi (ikiwa ni pamoja na ardhi iliyoachwa na wakulima walioathirika) kwa matumaini kwamba watafidiwa. Wakazi wanasema hivi:[300]

> "*Ukosefu wa RAP ulisababisha wasiwasi miongoni mwa wanajamii, hasa kwa sababu ardhi haina hatimiliki, badala yake, ni ardhi ambayo imekuwa makazi ya wanajamii kwa vizazi. Tangu kiwanda cha  makaa kimekuwa katika vyombo vya habari kwa miaka miwili au zaidi, watu wamekuja Kwasasi na kuchukua au kununua ardhi. Hilo lina maana kuwa wamiliki wa awali ni wachache na wengi wa wamiliki ni wapya, kwa kuzingatia mradi uliopendekezwa, wanashilikia ardhi na kwa hivyo kuzua mgogoro wa maslahi juu ya mradi. Hali hiyo inaendelea kuzua wasiwasi miongoni mwa wanajamii. Hii ni kutokana na ukosefu wa uwazi na kutokuwa na RAP kwa ajili ya eneo.* "

Kwa mujibu wa utafiti wetu wenyewe, tunaamini kwamba athari za makazi mapya kutoka kwa kiwanda cha makaa cha Lamu ziko katika makundi manne, yote yakijumuisha wanachama wa jamii za asili:

1. Uhamisho wa wakulima takribani 675 kutoka mashamba ya eneo la mradi;

2. Uhamisho wa wawindaji, wakusanyaji, wafugaji wa nyuki na wavunaji wa mikoko na watumiaji wengine wa rasilimali kutoka kwenye eneo la mradi;

3. Uhamisho wa wakulima zaidi ya 109 kutoka mashamba yaliyopitiwa  na barabara  ya kufikia eneo la mradi;

---

298 Full Resettlement Action Plan Summary - Lamu Coal Project (hamna tarehe), https://www.afdb.org/fileadmin/uploads/afdb/Documents/Environmental-and-Social-Assessments/Kenya_-_Lamu_Coal_Power_Project_%E2%80%93_RAP_Summary.pdf [RAP Summary].

299 Tazama pia Daily Nation "At what cost will Lamu coal power plant be to Man and sea?" (9 April 2018), where a local farmer explains "Five acres of my land is up for sale to Amu Power and I am anxiously waiting for them to finalise the process … As long as the sale hangs over it, I cannot farm as I have no idea when they will come calling; so I have not grown anything on it for over four years, and I am forced to rely on the small income I make from selling coconuts." https://www.nation.co.ke/news/In-Lamu--a-coal-power-plant-faces-opposition/1056-4378174-dajthdz/index.html.

300 BCP, §9.1.5.

4. Uhamisho wa kiuchumi miongoni mwa wavuvi na waendeshaji wa shughuli za utalii kutokana na uharibifu wa mazingira, vikwazo vya baharini na vingine vinavyoathiri ubora wa visiwa vya Lamu.

**Kielelezo 9: Kuhamishwa kutoka kwenye makazi na makazi ya msimu**

Mohamad Shee, Mwenyekiti wa Kundi la *Kwasasi Mvunjeni Farmers Self-Help* ameonyeshwa hapa na makazi ya muda ambapo anakaa wakati analima ardhi yake Kwasasi.





*Makazi mengine ya muda mfupi yanayotumiwa na mwanachama wa Kundi la Kwasasi la Mvunjeni Farmers Self-Help.*

IFC PS 5 ( makao mapya ya lazima) inatumika katika sehemu zote za madhara haya. Uhamisho wa kulazimishwa, katika muktadha huu, unamaanisha uhamisho wa makao (kuhamishwa au kupoteza makazi) na pia uhamisho wa kiuchumi (kupoteza rasilmali au kufikia rasilmali kunakosababisha kupoteza vyanzo vya mapato au njia zingine za maisha) kutokana na upatikanaji wa ardhi ya mradi na / au vikwazo vya matumizi ya ardhi au rasilimali zingine (ikiwa ni pamoja na rasilimali za baharini).[301] Katika kutambua athari kali za uhamisho kwa jamii, IFC PS 5 inasisitiza kuwa uhamisho lazima uepukwe. Hata hivyo, ambapo uhamisho huo hauwezi kuepukika, unapaswa kupunguzwa na hatua sahihi za kutuliza makali yake lazima ziandaliwe na kutekelezwa kwa uangalifu. Hili linafaa kufanyika kwa mashauriano yenye maana na ushiriki wa wale walioathirika.[302] Hatari za uhamishwaji zinapaswa kutambuliwa kama sehemu ya tathmini ya athari za E&S chini ya IFC PS 1,[303] na hatua za kina za kupunguza makali lazima ziwekwe kwa njia ya maandishi rasmi (na kushauriwa) katika RAP au Mpango wa Kuimarisha Riziki (*Livelihood Restoration Plan*).[304] Mteja hajaepushwa na majukumu hayo hata kama

[301] IFC PS 5, aya. 1 na 5.
[302] IFC PS 5, aya. 2.
[303] IFC PS 5, aya. 4.
[304] IFC PS 5, aya. 14.

mchakato wa uhamisho unasimamiwa na serikali.[305] Kinyume chake, ikiwa hatua za serikali za uhamisho hazitimizi masharti ya PS 5, mteja hana budi kutayarisha Mpango wa Nyongeza wa Uhamishaji (*Supplemental Resettlement Plan*) ili kuziba mapengo hayo.[306]

ESIA ya 2016 haielezi kikamilifu madhara ya mradi huo. Inaonyesha kwamba Mpango wa Utekelezaji wa Uhamisho (RAP) utalenga jamii za wakulima huku ikipuuza jamii zingine ambazo zitahamishwa kiuchumi. Pia ESIA imeweka kiwango cha uhamisho kuwa kidogo kuliko kilivyo, huku ikielezea kuwa patahitajika ekari 880 za ardhi.[307] Takwimu hiyo inaenda kinyume na notisi na nyaraka zingine za umma zinazotolewa na mpendekezaji wa mradi pamoja na Serikali ya Kenya. Nyaraka hizi zinatofautiana kwa takribani ekari 100. Kwa mfano:

| **Tarehe** | **Waraka** | **Eneo la Mradi** |
|---|---|---|
| 02/11/2015 | Taifa Leo - Taarifa ya Utekelezaji iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Ardhi | Ekari 351.8 ha (869.31 ) |
| 29/04/2016 | Gazeti la Kenya – Ilani ya Unyakuzi wa Ardhi iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Ardhi | Ekari 387.363 ha (957.194 ) |
| 10/07/2016 | EPR - Kiambatisho 8.11.6 | Ekari 975 |
| 10/07/2016 | EPR – EPR - Kiambatisho 4 na Kiambatisho 12.2.3 | Ekari 880 |
| 28/09/2016 | Maombi ya Tume ya Udhibiti wa Nishati ( Energy Regulatory Authority) iliyotolewa na Amu Power | Ekari 865 |
| Agosti 2017 | Muhtasari wa ESIA | Ekari 975 |
| Haina Tarehe | Muhtasari wa RAP (Eneo la AfDB) | Ekari 975 |

Isitoshe, ESIA haitoi taarifa zaidi kuhusu idadi ya watu ambao watahamishwa, vigezo vya ustahiki au mbinu za fidia. Tathmini yake ya maeneo mbadala haitaji makazi mapya hasa, au athari za kiuchumi baada ya uhamisho. Badala yake inasisitiza gharama za kila eneo.[308]

---

[305] IFC PS 5, aya. 30-31.
[306] IFC PS 5, aya. 31.
[307] 2016 ESIA Sura 9: Overview of the SEP, GM and RAP, §9.4 at 8.
[308] 2016 ESIA Sura ya 6: Project Alternatives, §6.1. Sehemu hii pia inataja athari za vumbi ya makaa kama sababu kikuu (labda ya pekee) ya kutojenga kiwanda karibu na bandari ya Mombasa, lakini haitoi tathmini linganishi ya uchafuzi wa hewa na athari zake kwa kisiwa cha Manda na maeneo jirani. .

Aghalabu, uandaaji na uchapishaji wa Mpango wa Kuimarisha Riziki ( *Livelihood Restoration Plan - RAP*) huweza kuondoa upungufu huu. Hata hivyo, sio katika hali hii. Kwa mujibu wa ufahamu wetu, hakuna Mpango wa Kuimarisha Riziki (RAP)  uliowahi kuchapishwa au kushirikisha watu walioathirika. Badala yake, Muhtasari wa RAP unapatikana mtandaoni (haijulikani umesambazwa kwa kiasi gani). Ingawa muhtasari wa RAP una taarifa zaidi kuliko ESIA ya 2016, na unatambua athari nyingi za uhamishwaji, bado una upungufu wa taarifa muhimu, ikiwa ni pamoja na:

- Haufafanui vigezo vitakavyoyawezesha kustahiki kwa makundi mbalimbali ya watu waliohamishwa na mradi huo.[309] Orodha rasmi ya wenyeji wanaomiliki ardhi na watumiaji wa ardhi ambao watapata fidia bado haijulikani, miaka minne baada ya kufanyika kwa majadiliano kuhusu mradi huu.  Hasa, bado haijulikani vile watakavyotendewa wakulima ambao hawana hatimiliki lakini wamekuwa wakilima na wakitumia kitamaduni hiyo ardhi  iliyoko katika eneo linalokusudiwa kujengwa mradi. Madhara ya kutokuwa na uhakika huu ni kali mno. Tunaelewa kwamba wakulima wanaotegemea uthibitisho wa Serikali wa makazi mapya na fidia bado hawajalipwa wala hawajaweza kukuza mimea kwenye eneo lililopangwa la mradi.[310] Hatma ya wakulima waliohamishwa na barabara ya kufikia kiwanja bado haijulikani, kwani wakulima hawa hawajashauriwa kabisa kuhusu uchukuaji wala fidia yoyote iliyopendekezwa.[311] Wahuni walowezi wanatumia fursa ya hali hii kunyakua ardhi kwa matumaini ya kupokea fidia, na kwa njia kuwahamisha zaidi wamiliki wenye haki / watumiaji wa ardhi;

- Hautambui kwamba baadhi ya watu walioathirika waliishi kwa msimu kwenye ardhi katika makazi za muda;[312]

- Hautambui kwamba wakulima walilima ardhi kwa kutumia mbinu za mzunguko, ambapo ardhi inaachwa kwa muda ipumzike na ipate afueni kabla ya kutumiwa tena.  Jambo hili linasababisha hatari kutokana na dhana kwamba ardhi iliyoachwa ipumzike inaweza kuchukuliwa kama ardhi isiyokuwa na wamiliki. Pia huongeza athari za uhamisho, kwa sababu sio wakulima peke yao wanapoteza mashamba, bali pia mfumo wao wa kilimo cha mzunguko unavurugwa kabisa. Hili linapunguza uzalishaji wa eneo pana;

- Umepunguza upeo wa uhamisho miongoni mwa wavuvi. Muhtasari huu unakisia hesabu ya watu waliohamishwa kutoka eneo la uvuvi kwamba ni takribani  "3BMUs" (vitengo vya usimamizi wa ufukoni), ambao ni jumla ya wavuvi 124.[313] Hautoi ramani au hoja inayofaa ili kuunga mkono takwimu hii. Tunaamini kwamba muhtasari unapunguza idadi ya wavuvi ambao wataathirika. Uvuvi wa bahari unachukua nafasi ya pili katika  ukubwa wa uchumi wa Lamu, baada ya utalii. Tunaamini kuwa angalau BMU tisa zitaathiriwa moja kwa moja, kwani wavuvi wanategemea maji yaliyo karibu na eneo la mradi.[314] Tunakadiria kuwa angalau wavuvi 4,700 wenye ujuzi wataathiriwa moja kwa moja na

---

309 RAP Muhtasari, §9.
310 "Kenyans at loggerheads over coal plant at world heritage site," Reuters (5 Jan. 2017), *inapatitikana* http://www.reuters.com/article/us-kenya-coal-idUSKBN14P1U5.
311 *Tazama* Sehemu   III.B.2 hapo juu.
312 RAP Muhtasari, §2.
313 RAP Muhtasari, §2.
314 BCP, §9.1.7.

kwa njia zingine kutokana na kiwanda cha makaa. Wavuvi hawa wanatumia maji ndani na karibu na Kisiwa cha Manda na wataathirika kutokana na kuzorota kwa mazingira ya baharini, vikwazo vya uvuvi na upatikanaji wa njia za meli. Uamuzi wa hivi karibuni wa Mahakama Kuu ya Kenya, kuhusu maendeleo ya bandari ya Lamu na LAPSSET kwa jumla, unaunga mkono malalamishi yetu: Mahakama Kuu ya Kenya iligundua kwamba wavuvi wa jadi kama 4,700 wataathiriwa sana na mradi wa bandari kutokana na ujenzi wake, madhara ya uzoaji, kukosa njia za kufikia baharini, na uharibifu wa miamba ya matumbawe na misitu ya mikoko.[315] Pia iligundua kuwa maslahi yao katika maeneo yao ya jadi ya uvuvi ni umiliki wa rasilmali kisheria, na hasara yoyote inapaswa kuambatana na fidia ya kifedha pamoja na msaada wa kuimarisha riziki.[316] Tunaamini kwamba athari zinazosababishwa na kiwanda cha makaa zitakuwa za kiwango sawa;

- Hautambui athari mbaya za riziki kwa watu wanaofanya kazi katika sekta ya utalii. Utalii unachangia pakubwa zaidi katika uchumi wa Lamu, mahali ambapo ni Turathi ya Dunia. Wafanya kazi katika sekta ya utalii wamekabiliwa na taathira kubwa katika maisha yao kwa sababu ya mabadiliko makubwa ya utamaduni na mazingira ya Lamu. Madhara ya rasilimali za matumbawe na baharini, pamoja na athari za usanifu na utamaduni wa Lamu Old Town, zitaathiri vibaya sekta ya utalii; na
- Haitambui kikamilifu madhara ambayo watapata watu asilia na jamii zingine zilizohatarishwa, kama ilivyojadiliwa zaidi katika kifungu kidogo cha III.F hapo chini. Waorma, Wasanye na Waswahili hawatambuliwi kabisa. Hakuna ithibati ya kibali kwamba jamii asilia zimeipa FPIC matumizi ya ardhi yao ya kitamaduni ambayo wanaitumia wao.[317]

[315] *Mohamed Ali Baadi and others v. the Attorney-General and others* (No. 22 of 2012) High Court of Kenya (Judgment dated 30 Apr. 2018), paras. 291-304 https://www.elaw.org/ke_LAPSSET_Summary_30April2018 (judgment under appeal).
[316] *Id.*
[317] See IFC PS 7, para. 15: “If such relocation is unavoidable the client will not proceed with the project unless FPIC has been obtained as described above.”

**Kielelezo 10: Mashua za Jadi**



*Uvuvi na mashua za jadi zinafanikisha utamaduni na uchumi wa Lamu, na kuendeleza shughuli zake mbili muhimu za kiuchumi: uvuvi na utalii.*

Aidha, ESIA ya 2016 na muhtasari wa RAP hazionyeshi kuwa watu waliohamishwa watapata aina na ubora wa faida za uhamisho zinazohitajika na sera ya IFC. Muhtasari wa RAP unalenga fidia, kwa njia ya fedha, hasara maalumu (hesabu iliyotumiwa haiko bayana) – badala ya kuzingatia mambo muhimu yanayorejesha riziki. Mpango wa RAP au Mpango wa Kurejeshoa Riziki, unaohitajika na IFC PS 5, unapaswa kufikia hali zote mbili.[318]

Kwa mfano, muhtasari wa RAP unasema kuwa wachuuzi wa mikoko watalipwa fidia kuktokana na kupoteza riziki kwa muda wa mwaka mmoja wakati wanapojifahamisha na vyanzo vingine vya mapato,[319] bila kuahidi msaada wowote au kuungwa mkono ili kujiruzuku kupitia njia hizi mpya.

Vilevile, muhtasari wa RAP unasema kwamba wavuvi ambao watapoteza misingi yao ya uvuvi watafidiwa kwa mwaka mmoja kwa kupoteza riziki wakitafuta vyanzo vingine vya kujiruzuku. Pia watapewa vifaa vya kisasa vya uvuvi na dau ili kuwawezesha kuvua samaki mbali na

[318] IFC PS 5, aya. 9, 20-22 (watu kuhamishwa) na 25, 27-28 (kuhamishwa kiuchumi).
[319] RAP Muhtasari, §10.

pwani.[320] Waraka huo hauna uchambuzi wa kina wa uvuvi wa mbali na pwani kuhusu jinsi uchukuaji, uteuzi, na usambazaji wa vifaa vya kisasa vya uvuvi na dau utafanyika. Pia, waraka haujataja umuhimu wa kutoa mafunzo mwafaka na maandalizi ili kuwafanya wavuvi hao kufanikisha mababadiliko hayo. Wala hakuna uchambuzi wa kina wa uvuvi wa mbali na pwani, na kama fidia ya mwaka mmoja itatosha kuziwezesha familia hizo kuendeleza riziki zao na pia kuruhusu wale wavuvi kuwekeza katika uvuvi wa mbali na pwani.

Miongoni mwa wa Aweer (watumiaji asilia wa eneo linalokusudiwa mradi), muhtasari wa RAP unasema kwamba,"watazingatiwa ili kupata kazi zisizohitaji ujuzi katika mradi wa kiwanda wakati wa awamu ya ujenzi na undeshaji."[321] Jibu hili halifai kabisa kwa jamii za asilia ambazo zinakabiliwa na vitisho mbalimbali dhidi ya urithi wao wa kitamaduni, pamoja na athari za riziki kutokana na mradi.

Tukizingatia ukweli kwamba uhamisho tayari unaendelea, bila RAP na IPP kamili na kamilifu zilizoshauriana, maendeleo ya kiwanda cha makaa cha Lamu tayari yanavunja masharti ya IFC PS 5.

### F. Tathmini za athari hadi leo zinapuuza watu asilia na makundi mengine yaliyohatarishwa

Katika IFC PS, kuna kanuni za kutambua na kuzingatia maslahi maalumu ya athari kwa watu asilia. Pia, IFC PS 7 (watu asilia) inawajibisha watekelezaji wa mradi unaoathiri vibaya jamii asilia, ikiwa ni pamoja na:

- Majukumu ya kutekeleza mchakato wa Mashauriano na Ushiriki wenye Ufahamu (ICP), unaojumuisha mashirika ya jamii asilia (kwa mfano, baraza la wazee au baraza la vijiji), na wanajamii wenyewe, na kuruhusu muda wa kutosha ili waweze kufanya maamuzi.[322]

- Majukumu ya kuepuka na kupunguza athari mbaya kama hizo, ikiwa ni pamoja na jitihada za kuepuka na vinginevyo kupunguza eneo la ardhi iliyopendekezwa kwa mradi huo na kuepuka, ama labda kupunguza madhara kwa maliasili;[323] na

- Kanuni za ziada za uhamishaji, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya kuunda Mpango wa Watu Asilia (*Indigenous Peoples' Plan- IPP*), kutoa fidia sahihi ya utamaduni na fursa za maendeleo endelevu, na, kukiwa na kuhamishwa au athari mbaya juu ya turathi muhimu za kitamaduni, kufuata kanuni ya Mwafaka Huru, wa Awali na wenye Ufahamu (FPIC).[324]

[320] RAP Muhtasari, §10.
[321] RAP Muhtasari, §10.
[322] IFC PS 5, aya. 9, 10.
[323] IFC PS 5, aya. 14.
[324] IFC PS 5, aya. 9, 14-15.

Kaunti ya Lamu ni makazi ya jamii asilia ambazo zimetengeneza njia maalumu za kujiruzuku kwa muda wa karne nyingi kwa kutumia mazingira ya baharini, pwani, misitu na nyasi. Jamii asilia za Kaunti ya Lamu ni pamoja na Wabajuni, Waswahili, Wasanye, WaAweer (wanaojulikana pia kama Waboni), Waorma, na pamoja na Wagiriama, Wamijikenda, na Wakore Maasai, miongoni mwa wengine.[325] Wabajuni (wanakadiriwa kuwa ni idadi ya watu 25,000)[326] ni wavuvi, watengenezaji mashua, wakulima na wachuuzi wa mikoko na kwa kawaida huishi kando ya pwani ya bara na kwenye visiwa vya Lamu.[327] Wasanye (wanakadiriwa kuwa ni idadi ya watu 500)[328] na WaAweer (wanakadiriwa kuwa ni idadi ya watu 2,500)[329] ni wawindaji na wakusanyaji wanaoishi misituni na hutafuta chakula chao nyikani na kwenye miamba ya mikoko tangu jadi. Wasanye wanazungumza lugha ya kidoko, inayosemekana kuwa mojawapo ya lugha za kale zaidi kwenye bara la Afrika.[330] WaOrma ni nusu wachungaji na wahamaji (hukadiriwa ni idadi ya watu 7,000).[331] Maeneo yao yanajumuisha kaunti tatu zikiwa pamoja na Lamu, Tana River, na Garissa, wakifuata malisho ya ng'ombe zao, mbuzi, kondoo na ngamia, wanyama ambao ni kipengele muhimu cha uchumi wa kikanda.[332] Jamii za Lamu ambazo zinajitambulisha kama Waswahili[333] ni WaSiyu, WaPate, na Wa-Amu (watu wa Siyu, Pate na Lamu). WaSiyu na WaPate wengi ni wakulima il hali Wa-Amu, wanaoishi katika mji mkubwa zaidi katika kaunti, ni wafanyabiashara, wakulima, na wavuvi.

Jamii hizi zote zinafuata imani ya Kiisalamu.[334] Wana michakato ya maamuzi mbalimbali ya kijadi.[335] Jamii zote inakabiliwa na uhamisho kutoka eneo la mradi, athari mbaya kwa riziki zao, athari juu ya turathi zao za kitamaduni, na ukosaji wa kufikia ardhi na rasilimali asilia katika au karibu na eneo la mradi.

Wabajuni wataathirika zaidi kwa kupoteza maeneo asilia ya uvuvi na mikoko. Madhara kutoka kwa kiwanda cha makaa yatazidisha hasara ambayo tayari imefanyika kutokana na ujenzi wa bandari ya Lamu.

---

[325] *Tazama* pia Kanyinke Sena, *Report on Expert Mission by a Member of the UN Permanent Forum On Indigenous Issues: Lamu Port-South Sudan-Ethiopia Transport Corridor (LAPSSET) and Indigenous Peoples in Kenya* attached in Annex 7.
[326] Kanyinke Sena, p. 9.
[327] Ijapokuwa Wabajuni katika maandishi mengi husemekana ni Wabantu wa jamii ya “Waswahili”, katika Lamu, Waswahili ambao ni wenyeji wa visiwa vya Lamu Mashariki hujiita “Wabajuni”, ilhali wale wa visiwa vya Lamu Magharibi hujiita “Waswahili.”. Jina “Swahili” lina mzizi wa neno la Kiarabu “Sawahel”, lenye maana ya pwani, na lilitumiwa na Waarabu kuziita jamii asilia za pwani ya Afrika Mashariki walizozikuta kutoka Somalia hadi Msumbiji: BCP, §§3.0 na 4.1.
[328] Kanyinke Sena, uk. 9.
[329] Kanyinke Sena, uk. 9.
[330] BCP, §4.3.
[331] Kanyinke Sena, uk. 9.
[332] BCP, §1.0.
[333] Jina “Swahili” lina mzizi wa neno la Kiarabu “Sawahel”, lenye maana ya pwani, na lilitumiwa na Waarabu kuziita jamii asilia za pwani ya Afrika Mashariki walizozikuta kutoka Somalia hadi Msumbiji: BCP, §3.0.
[334] BCP, §4.0.
[335] BCP, §7.0.

*"Miradi ya bandari na ya makaa itaathiri maeneo yetu ya uvuvi, ikiwa ni pamoja na maeneo jirani ya Manda na kwenye vituo vya Manda ikiwa ni pamoja na Dodori na Hori za Ndununi. Maeneo haya ni muhimu kwetu kwa uvuvi na samaki wa aina zote."*[336]

*"Tunashangazwa kuwa mazingira yetu ya pwani yataathiriwa sana na tutapoteza rasilimali zetu asilia, ambazo tunatumia kupata riziki zetu."*[337]

Jamii ya Wabajuni "wana maeneo ya kijamaa ya kilimo kwenye ardhi ya bara ambako tunaishi kimsimu. Wakati wa kupanda, tunasafiri hadi bara na kupanda mahindi, ufuta na mtama, kati ya mazao mengine."[338] Wanajamii wa Kundi la Kwasasi Mvunjeni Farmers Self-Help waliohamishwa kutokana na barabara ya ufikiaji eneo la mradi, wanajumuisha wanajamii wa Wabajuni, na jamii za WaAweer na Wagiriama.

Eneo asilia la WaAweer liko katika eneo la misitu kaskazini mashariki mwa Kaunti ya Lamu. WaAweer wataathirika sana kutokana na uharibifu wa misitu inayohusishwa na kiwanda cha makaa na miundombinu yake,[339] pamoja na uhamisho kutoka maeneo ya uwindaji asilia na ukusanyaji.

*"Eneo hili limekuwa makazi yetu tangu zamani. Kwa miaka mingi, tumekuwa wawindaji wa wanyama wadogo na tumeishi kwa matunda ya mwitu, mizizi na kukusanya asali kutoka misituni. Pia tunazingatia misitu sana kwa kuwa tuna maeneo mengi matakatifu humo ndani. "*[340]

WaOrma ni nusu wachungaji na wahamaji, ambao huhamisha ng'ombe wao kote katika nyika ya Lamu kutafuta malisho mazuri.

*"Tunatambua maeneo ya misitu na nyika katika sehemu ya magaharibi ya Kaunti kama ardhi ya ufugaji wa jadi. Kutoka Witu, tunahamia Kaskazini kuelekea maeneo ya misitu na kusini mwa nyanda za Mto Tana. Wakati wa msimu wa ukavu, tunaleta ng'ombe wetu kwenye nyanda za mto Tana na baada ya masika, tunawahamisha kwenye maeneo ya nyika hadi Voi."*[341]

Wasanye hutumia misitu kukusanya asali, matunda, na mizizi. Wao pia ni wakulima wadogo wadogo wa kupanda mahindi, mbegu za ufuta na mhogo. Kijadi, waliishi katika misitu ya kusini na ukanda wa mbuga za Lamu, kati ya Kisiwa cha Lamu na mji wa Witu ulioko bara. Hata hivyo, wamekuwa wakihamishwa kwa nguvu na miradi ya serikali, wakiachwa kutawanyika katika maeneo ya mijini na vijiji vidogo bila usalama wa ardhi.[342]

Waswahili pia ni wakulima, wavuvi na wafugaji, pamoja na wafanyibiashara wa bidhaa za kilimo zinazozalishwa na makundi mengine:

---

[336] BCP, §6.1.
[337] BCP, §6.2.
[338] *Id.*
[339] Kanyinke Sena, uk. 11.
[340] BCP, §4.4.
[341] BCP, §4.2.
[342] BCP, §4.3.

*"Sisi pia tulifanya biashara kwa ajili ya kupata mazao ya kilimo na mifugo kutoka kwa majirani zetu, hususan Wabajuni na WaOrma na kuuuza bidhaa zao katika miduara yetu ya kikanda na kimataifa. Wabajuni wamefanya biashara na sisi kutuuzia nafaka zao za ziada kutoka mashamba yao kwenye bara na WaOrma wametuuzia ng'ombe wao, ambao tumewauza kwa mataifa ya Uarabuni. Pia tunategemea wavuvi na wachuuzi wa mikoko kutoka Visiwa vya Bajuni kwa rasilimali zetu za baharini na vifaa vya ujenzi na kwa biashara katika masoko yetu ya kikanda. Wawindaji na wakusanyaji misituni pia wana jukumu la kustawisha uchumi wetu wa kikanda kwa kusambaza asali na mikeka kwa wakazi wetu wa miji."*[343]

*"Wengi wetu katika Lamu tunategemea mazingira kwa riziki zetu za maisha. Mababu zetu tangu jadi pia walitegemea maliasili ya eneo hili kwa ajili ya kujiruzuku. Mazingira haya yamekuwa ya kuaminika katika kutupatia sisi huduma hizi. Katika jamii yetu ya Lamu, tuna makundi kadha ya riziki yaliyoungana na kuingiliana. Makundi ya kikabila ndani ya Lamu mara nyingi hushirikiana katika kujiruzuku - na kwa sababu ya hili, jamii huishi kwa amani kwa sababu zinaingiliana ili kujiruzuku.*[344]

Kupotea kwa riziki hakutakuwa na athari za kiuchumi peke yake, bali pia kutapotea maarifa ya jadi na turathi za kitamaduni. Endapo mbinu za jadi hazifanyishwi kazi, hupotea.

"*Kilimo si riziki yetu tu – pia tuna mila na desturi za kitamaduni na kiroho ambazo zimejumuishwa na kilimo chetu. Sisi, Wabajuni, tuna nyimbo za jadi tunazoimba wakati wa maandalizi ya ardhi wakati wa kupanda na wa kuvuna. Tuna mtu anayeongoza kilimo ambaye huchaguliwa miongoni mwetu kwa sababu ya ujuzi, uzoefu, na wajibu wake. Tunapewa ushauri na mwanajadi anayeitwa mwalimu, juu ya wapi pazuri pa kilimo, ikiwa ni pamoja na ubora wa udongo, katika tamaduni inayoitwa "kushikamwitu." Sadaka ya tamaduni"pia hutolewa kwa ajili ya kilimo, na mwalimu huamua aina bora ya mbuzi, siku na wakati wa sadaka (inayoitwa "kuvuwadha"). Mila zingine za jamii za kuandaa ardhi ya kilimo ni pamoja na "Kusonga" na kukariri kwa Qur'ani Tukufu (Sura Ya Yasin) na sala ili kuhamasisha mafanikio, pamoja na sadaka kwa Mungu kwa kutambua baraka za mavuno mazuri (inayoitwa " Kudarawa). "*[345]

*"Kama wakulima, tunahatarishwa kwa sababu wengi wetu hatuna hatimiliki kuonyesha umiliki wa ardhi yetu. Pia tuna wasiwasi kwa sababu haturuhusiwi kuingia msitu ili kupata matunda ya mwitu yaliyopo kama dhichakwi, pepeta, mabonge, tundukuwa, kungu, makoma, maganda ya kamwa, kunazi, na matongaandukwaju. Tunahofu kubwa kwa sababu ya Bandari la Lamu na miundombinu zingine za LAPSSET. Tuna wasiwasi kwamba ardhi zetu za kilimo cha jadi zitachukuliwa, kwamba rasilimali zetu za asili zitaharibiwa kutokana na idadi ya watu wanaoishi katika kaunti na pia mbinu zetu za uhifadhi wa jadi hazitaheshimiwa."*[346]

[343] BCP, §4.5.
[344] BCP, §6.0.
[345] BCP, §6.5.
[346] BCP, §6.5.

Jamii hizi pia zinaogopa kupoteza uwezo wa kufikia maeneo muhimu ya kitamaduni. Wasanye "tayari wamepoteza baadhi ya makaburi ya baba zetu na tuna hofu kwamba tutaendelea kupoteza maeneo zaidi."[347]

Hatimaye, makundi yanaogopa madhara yanayohusiana na uhamiaji wa watu, ikiwa ni pamoja na uharibifu wa mazingira, uharibifu wa maadili na utamaduni, na wanajamii kuwekwa pembezoni zaidi.[348]

> *"Ongezeko la idadi ya watu kutokana na jengo la bandari na miundombinu zingine litasababisha uharibifu mkubwa wa rasilimali zetu za asili kama mikoko, ambayo hutumiwa kujenga nyumba na hii pia itaathiri mazingira ya baharini kama maeneo ya uzalishaji samaki na kulinda pwani dhidi ya mafuriko. Maeneo ya misitu pia yatahatarishwa kutokana na ongezeko la idadi ya watu na vipengele vingine vya LAPSSET na kiwanda cha makaa ambacho kinahitaji sehemu kubwa ya ardhi kujengwa. Tunaogopa kwamba rasilimali zetu zitazoroteshwa na tutapoteza riziki na turathi.*[349]

> *"Tunahofia kwamba kutokana na idadi kubwa ya watu wapya wanaohamia Lamu kutafuta ajira, tutalazimishwa kuhama ili tuwape nafasi. Tamaduni zetu za maisha zitapotea milele tunapohamia mijini na vijijni kutafuta makazi. Tutapoteza njia zetu za maisha na rasilimali asilia tunazotumia kwa riziki zetu.*[350]

> *"Tunahatarishwa wakati tunapozungumzia uandaaji wa miradi kwa sababu sisi (Wasanye) hatuna uwakilishi wowote wa kisiasa katika Kaunti, wala nchi. Sisi jamii ya WaAweer tuna mwakilishi mmoja aliyechaguliwa katika Bunge la Kaunti, lakini hii haitoshi kulinda uhatarishwaji wetu dhidi ya ujenzi wa viwanda ambavyo huchukua ardhi zetu. Kwa jumla, tuna elimu ya chini sana. Wengi wetu hatukumaliza elimu ya msingi na tunajitahidi kupeleka watoto wetu shuleni. Kwa sababu ya kiwango chetu cha elimu, wanabiashara, wajenzi na maafisa wa serikali hunufaika kutokana na hali zetu. Sisi, Wasanye hatuna hata hatimiliki moja katika jamii nzima. Na sisi, WaAweer, pia tunakabiliwa na matatizo ya usalama wa ardhi.*[351]

Katika ESIA ya 2016 hakuna tathmini yoyote ya kina kuhusu tabia za kikabila au kiuchumi za jamii zilizoathiriwa. Hakuna ithibati ya watu wa asili isipokuwa kuwataja kwa kifupi jamii za WaAweer (Waboni) na Wabajuni.[352] Kwa kweli, ESIA haizingatii hatari ya kijamii, wala haitaji kuhatarishwa na uzingatiaji wa watu asilia unaoagizwa na IFC PS 1 na 7. Wala hatuna ufahamu wowote wa mashauriano maalumu ya jamii za asili zilizoathiriwa. Hakuna ushahidi kwamba mashauriano yenye maana, bila hata FPIC, yamefanyika miongoni mwa jamii hizi. Hakuna Mpango wa Watu Asilia katika mradi huu.

Mteja pia anatakiwa kutambua watu binafsi na vikundi ambavyo vinaweza kuathiriwa na mradi moja kwa moja, kwa njia tofauti, au kwa kiasi kikubwa, kwa sababu ya hali yao ya

[347] BCP, §6.3.
[348] *Tazama* pia Kanyinke Sena, uk. 11-13.
[349] BCP, §6.2.
[350] BCP, §6.4.
[351] BCP, §6.4.
[352] 2016 ESIA, Sura 8, §§8.11.7 na 8.14.1

kuhatarishwa.[353] ESIA inarejelea tu kwa kifupi madhara yanayoweza kuwapata wanawake wakati wa uhamisho na  wa makazi mapya, bila mipango ya kupunguza makali ya tatizo hilo.[354]

Muhtasari wa RAP pia haujachambua na kushughulikia maswala haya kikamilifu. Ingawa jamii za WaAweer na Wabajuni zimetambuliwa kwa kifupi katika muhtasari RAP, hakuna hatua za kutosha zilizowekwa ili kuwalinda kutokana na madhara mabaya za mradi huu. Kwa mfano, muhtasari wa RAP unakubali kwamba WaAweer watapoteza ardhi yao ambayo wanaitumia katika uwindaji, ukusanyaji na ufugaji wa nyuki, lakini hauelezi ni wangapi walioathiriwa au matokeo ya mashauriano yoyote.  Zaidi ya hayo, kama ilivyojadiliwa hapo juu, muhtasari wa RAP unasema kuwa WaAweer "watazingatiwa kwa fursa za kazi zisizo na ujuzi katika mradi wakati wa awamu ya ujenzi na uendeshaji."[355] Haya ni majibu yasiyofaa kabisa kwa jamii asilia ambayo inahatarishwa kupitia turathi zake za kitamaduni pamoja na riziki zake na mazingira. Pia kwa kifupi muhtasari unaelezea athari kwa Wabajuni, bila kutaja athari hizo kwa kina  au jinsi zitakavyopunguzwa makali.[356] Hakuna marejeleo ya jamii zingine asilia. Watu wawili, kwa jumla, ndio waliotambuliwa kuwa  wamehatarishwa kwa msingi wa ujane. Hatua pekee za kupunguza makali  na fidia ambazo zimetambuliwa kwa waliohatarishwa na vikundi asilia ni:[357]

- Kwa wajane wawili walioathirika, Kamati ya Usimamizi wa Mradi wa Makazi Mapya, kupitia jamii itawapa msaada zaidi ili kuhakikisha kuwa wana akaunti za benki, wanafahamishwa wakati fedha za fidia zitawekwa kwenye akaunti zao na watahamasishwa jinsi wanavyopaswa kuwekeza fedha ili kuwa na chanzo cha riziki. Wanapaswa pia kujulishwa fursa yoyote ya ajira au biashara zinazotokana na mradi huo.
- Jamii ya WaAweer ambayo imetegemea eneo la mradi kwa uwindaji na shughuli zingine za uendeshaji, itazingatiwa kwenye fursa za ajira zisizo na ujuzi katika mradi wakati wa awamu ya ujenzi na uendeshaji, bila kutafakari kama kazi hizi zinazingatiwa kuwa sawa kitamaduni na jamii zilizoathirika.

Hatua hizi hazitoshi kabisa kulinda jamii asilia na makundi mengine yanayoathirika kutokana na madhara makubwa ya ujenzi wa kiwanda cha makaa cha Lamu. Kinyume chake, kuhatarishwa na kutengwa kwa watu asilia kunazidishwa na namna wanavyopuuzwa na waendelezaji mradi.

### G. Turathi za kipekee za kitamaduni zinatishwa

Mbali na vitisho maalumu vinavyowakabili watu asilia, jamii ya Lamu inakabiliwa na athari mbaya juu ya turathi zake za kitamaduni zenye thamani. Lamu Old Town ni mfano bora wa

[353] IFC PS 1, aya. 12. Hadhi hii ya pembezoni ama iliyohatarishwa huenda ikatokana na tofauti za rangi, jinsia, lugha, dini, maoni ya kisiasa au kitu kingine, chanzo cha kitaifa au kijamii, rasilmali, uzawa, or hali nyingine. Mteja anapaswa pia kuchunguza hali kama jinsia, umri, kabila, utamaduni, afya, elimu, ulemavu wa mwili au akili, umasikini au hali duni ya kiuchumi, na utegemezi wa maliasili maalumu: angalizo 18.

[354] 2016 ESIA, Sura 8.11.6.

[355] Muhtasari  RAP, §10. *Tazama pia* §5.12.5  ambapo muhtasari wa RAP unatambua kwa kifupi kwamba " "Ardhi ambapo mradi unakusudiwa kujengwa ilikuwa ardhi ya jamii na kipande hicho kilikuwa cha vizazi vya kale. Jamii ya Wabajuni kutoka visiwani ilitumia kipande hiki kwa ajili ya kilimo na Waaweer walikitumia kuwekea mizinga ya nyuki."

[356] Muhtasari RAP, §2. *Tazama pia*  §5.12.5.

[357] Muhtasari RAP, §10.

juhudi za kuhifadhi makazi ya Waswahili na ni kituo kikuu cha elimu katika utamaduni wa Kiislam na Kiswahili katika Afrika Mashariki. Hadi sasa, Lamu Old Town ni jamii ya kihafidhina na iliyohifadhiwa, kudumisha utimilifu wake wa kijamii na utamaduni, pamoja na usanifu wake halisi na kazi muhimu za kidini. Kwa sababu hizi, Lamu Old Town ilijumuishwa kwenye Orodha ya Turathi za Dunia mwaka 2001 kama mali ya kitamaduni ya Thamani Bora ya Ulimwengu.[358]

UNESCO ina hofu kubwa kwa turathi hii ya kitamaduni, maendeleo ya LAPSSET pamoja na kiwanda cha makaa. Hofu hizo zimesababisha ufuatiliaji kadha na mapendekezo mbalimbali, mengi ambayo hayajatekelezwa.[359] Tathmini ya Athari ya Turathi, iliyotajwa na UNESCO lakini haipatikani kwa wakati huu, inaelezea matatizo kadha muhimu:[360]

> *"Ijapokuwa Kisiwa cha Lamu na rasilmali ya Turathi za Dunia haziko chini ya mradi wa [LAPSSET], na huenda zisiathirike moja kwa moja, na madhara katika maeneo ya rasilmali ya Turathi ya Dunia zaidi ni ya pembeni, kuna madhara mengi yatakayotokea katika mazingira ya rasilmali za Turathi ya Dunia - mazingira ya kitamaduni ya Lamu – na madhara mabaya jumulifu ya turathi asilia katika utamaduni wa eneo hili ambayo yatakuwa na athari kubwa za kudumu. "*

> *"Kuna ... uwezekano wa sio tu kudunisha jamii lakini kuvunja kabisa utamaduni na maisha ya kitamaduni yaliyokuzwa na kuimarishwa kwa karne na upotezaji wa turathi. Maadili ya kitamaduni, mizizi, uhuru wa usafiri na utozingatiaji wa hisia za ushirikiano kijamii kwa maadili ya kimsingi unahatarishwa. Aidha, uhusiano unaohusishwa na maeneo muhimu ya elimuya kale inayohimili historia na ujitambulishaji wa mahali na ukuaji, una uwezekano wa kupotea milele.*

---

[358] UNESCO "Lamu Old Town" https://whc.unesco.org/en/list/1055/.

[359] Ripoti ya UNESCO, *Report Of The World Heritage Centre/ICOMOS/ICCROM Advisory Mission To Nairobi Concerning Lamu Old Town, Kenya* (Apr. 2018), https://whc.unesco.org/document/167872 ["UNESCO Report (2018)"]; UNESCO, *Report on the Reactive Monitoring Mission to Lamu Old Town Kenya* (Feb. 2015), http://whc.unesco.org/document/135436 ["UNESCO Report (2015)"].


[360] Ripoti ya UNESCO (2018), 3.4.1, uk. 26.

**Mchoro 11: Lamu Old Town**



*Eneo la Umma Katika Lamu Old Town*





*Ngome ya Lamu*





*Mifano ya milango na njia za kupitia Mjini Lamu Old Town*

Kuhusu hasa kiwanda cha makaa, UNESCO inataja hatari za kitamaduni zifuatazo:[361]

- Kupoteza mila na desturi zinazohusiana na riziki zitokanazo na uvuvi;
- Tishio kwa majengo ya mawe maridadi katika Lamu Old Town na mahali kwingine kutokana na uchafuzi wa hewa;
- Athari za ongezeko la watu (ikiwa ni pamoja na maendeleo yasiyodhibitiwa, ukosefu wa usalama, hali ya afya) na mabadiliko ya tabia za Uswahilini miongoni mwa wanajamii; na
- Athari za ujumi kutokana na miundombinu ya kiwanda cha makaa.

UNESCO inasema kwamba ESIA ya 2016 haishughulikii hatari hizi kikamilifu. ESIA ya 2016 inapendekeza mfululizo wa sheria na kanuni juu ya wafanyakazi na makandarasi, kwa mfano kutoa taarifa kuhusu "mapato ya bahati" na mavazi ya heshima. Hata hivyo, kanuni hizi hazilingani na athari kubwa kwa turathi za kitamaduni zinazotokana na mradi huu.[362] ESIA ya 2016 inashindwa kushughulikia maswali muhimu zaidi kama vile makazi ya wafanyikazi na idadi ya watu na aina ya wafanyikazi (ikiwa ni pamoja na umri na kabila). Kama UNESCO inavyosema, "[ESIA] haiweki wazi taarifa ifaayo kuhusu madhara ya idadi ya watu na mabadiliko ya tabia za Uswahilini. ... Ni maisha ya kila siku ya kijamii na ya kitamaduni yatakayoathiriwa sana, na suala hili linahitaji kuchunguzwa na  na kueleweka vizuri kabla ya hatua za kupunguza makali ya madhara kutengenezwa.[363] "ESIA 2016 pia  haishughulikii athari za uchafuzi - ikiwa ni pamoja na mvua ya asidi - kwenye maeneo muhimu ya kitamaduni.[364]

Aidha, ESIA haishughulikii  uwezekano wa madhara  kwenye maeneo ya kihistoria yaliyo karibu na kiwanda cha makaa, ikiwa ni pamoja na misikiti miwili, inayojulikana kama maeneo ya kihistoria kutokana na ramani ya rasilimali ya jamii ya Save Lamu (angalia Kielelezo 7 hapo juu). Maeneo mengine ni makaburi na visima, yanayoweza kuharibiwa wakati wa ujenzi. Aina hizi za maeneo, hasa misikiti ya kihistoria, ni mifano mwafaka na njia za kuhifadhi utamaduni na

[361] Ripoti ya  UNESCO  (2018), uk. 27-29.
[362] 2016 ESIA, Sura 8, §§ 8.12 na 8.14.
[363] Ripoti ya UNESCO (2018), uk. 29.
[364] Tazama pia Sehemu III.D.4 hapo juu.

utambulisho wa jamii zetu. Uwepo wa aina hizi za maeneo pia husaidia jamii wakati wanafanya madai ya ardhi na / au kuthibitisha muda gani wamekaa katika eneo fulani.

Tathmini hii ya juu juu na isiyokuwa na kina juu ya athari za turathi za kitamaduni inakiuka kanuni zaa IFC PS 1 na 8 ( turathi za kitamaduni). Utamaduni maalumu, wa kihafidhina na uliohifadhiwa na Lamu Old Town na mazingira yake, kama maeneo ya turathi ya kitamaduni inayotambulika kimataifa, ni "turathi muhimu ya kitamaduni" kwa minajili ya IFC PS 8.[365] Kwa hivyo, mteja anahitajika kuepuka athari juu ya turathi hizi muhimu za kitamaduni. Katika mazingira ya kipekee ambapo madhara hayawezi kuepukika, mteja lazima aonyeshe matokeo yatakayopatikana na mchakato mzuri wa kujadiliana na jamii zilizoathirika na kuhifadhiwa katika nyaraka.[366] Mteja lazima pia abaki na wataalamu wa nje ili wasaidie katika tathmini ya ulinzi wa turathi muhimu za kitamaduni. ESIA 2016 haitoi ushahidi kwamba mahitaji hayo yametekelezwa.

## H. Tathmini mbadala inategemea dhana potovu na mantiki isiyofaa

### *1. ESIA haitoi mantiki ya kutosha kwa kukataa vyanzo bora vya nishati mbadala*

Kama ilivyojadiliwa kwa urefu katika malalamishi haya, inajulikana wazi kuwa viwanda vya makaa ni hatari kwa afya ya binadamu na hatari zingine zinazohusiana na hali ya anga. Ni kutokana na sababu hizi ambapo World Bank Group inatoa msaada wa kifedha tu kwa miradi ya umeme wa makaa ya kijani katika hali chache pekee.[367] IFC PS pia inahitaji IFC na mteja wa mradi kuzingatia njia mbadala, ili kuhakikisha kwamba athari mbaya za E&S zimeepukwa.[368] Miongozo ya EHS ya IFH kwa Viwanda vya Joto la Umeme hasa unapendekeza matumizi ya " mafuta safi zaidi inayopatikana kwa urahisi (kwa mfano gesi ya asili ni bora kuliko mafuta, ambayo ni bora kuliko makaa)" ili kupunguza uchafuzi wa hewa.[369] Uchambuzi mbadala uliofanywa kwa kiwanda cha makaa cha Lamu hauwezi kufikia viwango hivi muhimu, kuhakikisha kiwanda cha nishati ya makaa, kinyume na nishati isiyokuwa na athari kubwa - katika hali hii.

Tathmini ya njia mbadala ya kiwanda cha makaa imetegemea hoja zisizofaa ili kukataa vyanzo mbadala, visivyochafua mazingira. Uzingatifu wake wa njia mbadala ni mfupi sana na hauna ufafanuzi wa kuamua kama masuala ya kiuchumi, kiufundi, mazingira na kijamii yalipimwa vizuri. Sehemu hii ya ESIA haitilii maanani mahitaji ya IFC PS ya kuzingatia njia mbadala za mradi. Kwa hakika, inashindwa kuthibitisha uamuzi wa kuchagua chanzo cha nishati yenye uchafuzi wa juu zaidi.

Tathmini ya ESIA ya njia mbadala inasema kwamba kiwanda cha makaa ya umeme kilichaguliwa kuwa ni bora kwa ajili ya mradi uliopendekezwa ili kutimiza haja ya kuwa na "kiwanda cha nishati chenye gharama ya chini."[370] Tathmini inatarajia kuzingatia chaguzi

---

[365] IFC PS 8, aya. 13.
[366] IFC PS 8, aya. 14.
[367] "Toward a Sustainable Energy Future for All: Directions for the World Bank Group's Energy Sector" (2013) http://documents.worldbank.org/curated/en/745601468160524040/pdf/795970SST0SecM00box377380B00PUBLIC0.pdf.
[368] *Tazama* IFC PS 1, angalizo 11 pamoja na majukumu mengine yaliyotambuliwa hapo juu.
[369] EHS Guidelines for Thermal Power Plants, uk. 3.
[370] 2016 ESIA Sura 6, §6.2.9.

zisizochafua, ikiwa ni pamoja na nguvu za jua na nguvu za upepo, lakini tathmini ya gharama na uwezekano wa chaguzi hizi unaegemezwa kwenye hoja zisizofaa na taarifa iliyopitwa na wakati.

Kwa mfano, ESIA inasema kwamba nishati ya jua au nishati ya upepo haziwezi kuhifadhiwa au kutumika kama vianzo vya msingi. Pia inadokeza kwamba hakuna aina yoyote ya uzalishaji wa nguvu ya umeme nchini Kenya inayopaswa kuzidi asilimia 10 ya wastani ya mahitaji ya umeme,[371] "La sivyo, gridi haitakuwa thabiti. "Lakini madai haya si ya kweli.[372] Kulingana na utafiti wa hivi karibuni uliochapishwa na wanasayansi wa Chuo Kikuu cha Stanford, "uchumi wa nishati ya [Upepo, Maji, Jua] unaweza kutumika bila kupoteza uzito zaidi ya miaka [6] kwa gharama nafuu. ... kutopoteza huku kwa uzito kunazidi viwango vya matumizi ya umeme unaoaminika.[373] "Uchunguzi mwingine umegundua kuwa nishati ya jua inaweza kuwa bora kama chanzo cha nishati ya msingi wa gridi kubwa.[374] Denmark imekuwa ikifuatilia angalau asilimia 40 ya umeme wake kutoka kwa upepo tangu 2008.[375] Utafiti mwingine uligundua kwamba nishati za jua na upepo peke yake zinaweza kutegemewa na kuiendesha gridi kubwa ya nishati (kufikia eneo moja ya tano ya Marekani).[376] Vile vile, uchunguzi wa hivi karibuni wa Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, unaonyesha kwamba hakuna haja ya kupunguza upepo na vyanzo vya nishati za jua kwa sehemu ndogo ya nishati ya jumla ya gridi.[377] Ripoti hii imetumia kielelezo cha nishati ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa imani ya utegemezi wa nishati ya upepo na ya jua inayozidi asilimia 10% ya gridi , ikionyesha kwamba haiamini asilimia 10% ni kiwango mwafaka cha kipimo.

Fauka ya hayo, matumizi ya nishati za upepo na jua yanaweza kuwa ya gharama ya chini kuliko ya kiwanda cha makaa kilichopendekezwa. ESIA inasema kuwa kiwanda cha umeme wa makaa kinatumia kiwango cha chini kabisa ya umeme (LCOE), kwa US ¢ 7.52 / kilowati kwa saa (kWh).[378] Hata hivyo, tafiti za hivi karibuni zimegundua kuwa LCOE kutokana na gharama, nishati za jua na upepo iko sawa na au chini ya makadirio haya. Kwa mujibu wa chapisho la mwaka wa 2013 na Maabara ya Taifa ya Lawrence Berkeley, mikataba ya hivi karibuni ya kununua nishati za miradi ya fotovoltaiki nchini Marekani imeshuka sana katika miaka ya hivi karibuni, na karibu dola 25 /megawati kwa saa (MWh) kwa mwaka, wastani kutoka 2008-2013. LCOE mwaka 2013 katika gharama ya matumizi ya nishati, nishati ya jua ilikuwa ya kiwango

[371] *Id.* katika §§ 6.2.7, 6.2.8.

[372] *Id.* katika §6.2.7.

[373] *Tazama* Taarifa ya shahidi Mark Chernaik, iliyoambatwa katika Nyongeza 3.

[374] *Tazama, kwa mfano.*, Jacobson, M. Z., Delucchi, M. A., Cameron, M. A., & Frew, B. A., Proceedings of the National Academy of Sciences 112 (49) "Low-cost solution to the grid reliability problem with 100% penetration of intermittent wind, water, and solar for all purposes" uk. 15060-15065 http://www.pnas.org/content/112/49/15060.full.

[375] Sovacool, B. K., Utilities Policy, 17(3) "The intermittency of wind, solar, and renewable electricity generators: Technical barrier or rhetorical excuse?" (2009) uk. 288-296 https://www.researchgate.net/profile/Benjamin_Sovacool/publication/46495038_The_intermittency_of_wind_solar_and_renewable_electricity_generators_Technical_barrier_or_rhetorical_excuse/links/00b7d526620ca159ea000000.pdf. Renewables also account for just over 40 percent of electricity production in Germany: *see* Reuters "Renewables overtake coal as Germany's main energy source" (3 Jan. 2019) https://www.reuters.com/article/us-germany-power-renewables/renewables-overtake-coal-as-germanys-main-energy-source-idUSKCN1OX0U2:

[376] Budischak, C., Sewell, D., Thomson, H., Mach, L., Veron, D. E., & Kempton, W., Journal of Power Sources, 225 "Cost-minimized combinations of wind power, solar power and electrochemical storage, powering the grid up to 99.9% of the time" pp. 60-74 http://www.edleaver.com/homepage/Archives/2013/06/pdf/CostMinimizedCombinationsOfWindSolarAndElectrochemicalStorage.pdf.

[377] Castellano, et al. "Brighter Africa: The growth potential of the sub-Saharan electricity sector" (2015) p. 29, fn 43.

[378] 2016 ESIA Sura 6, §6.2.9.

cha  chini cha US $ 50-60 / MWh, ambacho ni sawa na US5-6 ¢ / kWh.[379] Makadirio haya ni ya chini sana kuliko makadirio ya 7.52 / kWh LCOE ya kiwanda cha makaa.

Ingawa takwimu za utafiti wa Lawrence Berkeley zinazingatia soko la nishati ya jua nchini Marekani, zinatufanya  kutilia shaka madai ya ESIA kuwa nishati ya kiwanda cha makaa ina LCOE ya chini kwa chaguzi zilizozingatiwa. Kama ESIA inavyoeleza, Ushuru wa Kenya wa "Feed-in- Tariff" wa nishati ya jua na upepo utaongeza, kwa njia isiyo halisi, bei ya vyanzo hivi vya nishati,[380] lakini ushuru huu ni wa muda mfupi, na hautatumika katika miradi mikubwa.[381] Vyanzo vya nishati ya upepo na jua tayari ni nafuu kuliko makaa, na bei  zinaweza kuanguka zaidi, na kufanya chaguo hizi kuwa ndizo bora zaidi kwa Kenya kwa muda mrefu.

Pamoja na vigezo vingine, nishati ya upepo na jua huonekana kuwa nzuri zaidi kuliko ya kiwanda cha makaa, hata kulingana na tathmini ya ESIA yenyewe. Katika kuthibitisha uamuzi wa ujenzi wa kiwanda cha makaa, ESIA inabainisha kuwa ina muda wa ujenzi wa kiwanda wa haraka. Hata hivyo, ESIA inaweka ratiba ya muda wa ujenzi wa kiwanda cha makaa kuwa ni takribani miezi 36, wakati muda wa nishati ya jua na upepo ni chini ya miezi 12 na miezi 24-30, mtawalia.[382]

Kwa jumla, mbinu ya ESIA ya kuorodhesha kwa kifupi mazingatio chanya  na hasi kwa kila "njia mbadala" ilioangaziwa, bila uchambuzi makinifu, haitoi taarifa ya kutosha ili kutupilia mbali mtazami kuwa  nishati mbadala za upepo na jua  zina uchafuzi wa chini  na hatimaye gharama ya chini kwa mahitaji ya nishati ya Kenya. Jamii zetu zinahitaji njia hizo mbadala:

> *"Hatutaki mazingira yetu na riziki zetu kuhatarishwa kwa vile tunategemea sana rasilimali zetu asilia. Kwa hivyo, tunaomba kwamba serikali iweze kuchunguza njia mbadala za nishati safi inayoweza kutumia kwa mara nyingi."*[383]

*2. Tathmini ya maeneo mbadala haitoi sababu za kutosha za kuchagua eneo la mradi*

Tathmini ya maeneo mbadala inazingatia tu gharama na inapuuza masuala ya kijamii na mazingira. Kwa mfano, haitoi fursa ya kuchagua maeneo ya bara ambayo yanaweza kupunguza athari za mazingira ya pwani ya Kenya, pamoja na shinikizo la mazingira na jamii katika eneo la Lamu Old Town (eneo la Turathi ya Dunia). Jambo hililinatajwa  katika sentensi mbili tu pamoja na gharama kubwa bila kuzingatia mambo mengine.[384] ESIA haijadili athari za makazi au za uhamisho katika maeneo yaliyopendekezwa, na hata eneo lililochaguliwa. Jambo hili linafanya ulinganishaji  wa athari za makazi mapya na za maeneo yanayofaa uwe mgumu. ESIA inasema athari za vumbi ya makaa kama sababu ya msingi (labda hiyo tu) kufanya mradi usiwe karibu na bandari ya Mombasa, lakini haitoi tathmini yoyote ya kulinganisha athari za uchafuzi kwa

---

[379] Bolinger, M. "Utility-Scale Solar 2012: An Empirical Analysis of Project Cost, Performance, and Pricing Trends in the United States" (2014) uk. 25 http://escholarship.org/uc/item/3cf3876s.pdf.
[380] Kenya ina ushuru wa "Feed-in-Tariff" kwa ajili ya umeme wa jua na upepo wa US¢11/kWh and US¢12/kWh, mtawalia. ESIA Sura 6, §§ 6.2.7, 6.2.8.
[381] Feed-in-Tariffs Policy on Wind, Biomass, Small Hydro, Geothermal, Biogas and Solar Resources Generated Electricity, Kenyan Ministry of Energy (Dec. 2012), Appendix 2, p. 16, *available at* http://www.erc.go.ke/images/docs/fitpolicy.pdf. The Feed in Tariff does not apply to solar projects larger than 40 MW or wind projects larger than 50 MW.
[382] 2016 ESIA Sura 6, §§6.2.5, 6.2.7, 6.2.8.
[383] BCP, §9.1.2.
[384] 2016 ESIA Sura 6, §6.1.

mazingira au makazi muhimu katika kisiwa cha Manda na maeneo jirani, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bandari ya Lamu.[385] Matokeo ya tathmini inayojumuisha gharama za njia mbadala haitoi kigezo cha kuamua kama athari za makazi mapya au madhara kwa makazi asilia au muhimu yangeepushwa kupitia kuchagua eneo mbadala la mradi. Jambo hili ni kinyume na mahitaji ya IFC PS yanayoagiza wanamradi kuepuka uhamisho wa kilazima na athari kwa mazingira muhimu na asilia kadri iwezekanavyo.

*3. ESIA haitathmini njia mbadala ambayo ni safi kwa vipengele muhimu vya usanifu*

Tathmini ya njia mbadala inaelezea chaguzi mbili za mwako wa mafuta, lakini haitoi uchambuzi wa kuunga mkono uamuzi wa kutumia makaa yaliyotengenezwa na moto,[386] kinyume na teknolojia ya juu zaidi.[387] Ingawa Amu Power na GE tayari wametangaza kwamba teknolojia ya hali ya juu zaidi itatekelezwa, bado kuna shauku kama mpango huo umekamilika. Aidha, hakuna tathmini za E&S zilizochapishwa kutoa maelezo ya teknolojia hiyo au ikiwa hatua za kulazimishwa zitatekelezwa.[388]

Uzingatuaji wa teknolojia mbadala ya mfumo wa baridi na uchanguzi wa njia mbalimbali za usimamizi zinaonekana kufikia maamuzi ya mwisho. Uamuzi wa mfumo wa kuweka baridi moja kwa moja umeelezwa katika sentensi moja tu, inayosema kuwa hili ni chaguo bora zaidi kwa ajili ya kutia baridi katika teknolojia ya juu zaidi ya ya boila,[389] bila kutambua hatari zake kubwa zaidi kwa mazingira ya baharini (kama ilivyoelezwa hapo juu). ESIA inaelezea tu mifumo tofauti ya kutia baridi, lakini haifafanui manufaa na hasara za kila mfumo. Ijapokuwa mfumo mseto wa kutia baridi unaorodheshwa kama njia mojawapo mbadala, ripoti haifafanui wala njia zingine mbadala safi na zisizokuwa na athari kubwa kwa mazingiraza, kama vile vile utiaji baridi kwa unyevunyevu mzunguko[390] au mifumo mingine ya kiwango cha juu.

Njia ya kuhifadhi majivu kavu pia inaelezwa kwa kauli rahisi kwamba kuhifadhi majivu yenye unyevunyevu kunahitaji maji mengi, bila kutambua hatari za uchafuzi wa hewa inayotokana na uhifadhi wa jivu kavu.[391] Taarifa hizi fupi hazitoshi kuchunguza manufaa ya kimazingira na kijamii ya miundo mbadala. Isitoshe, tathmini hizi za juu juu hazina taarifa kuhusu mbinu mbadala za kudhibiti hatari za kimazingira na kijamii.

---

[385] *Id.*

[386] 2016 ESIA Sura 6, §6.4.

[387] *Tazama*, kwa mfano, Poulsen, H. (2006). Advantages of Ultra Super Critical Technology in Power Generation. International Conference on Clean Coal Technologies for our Future CCT2005, Sardinia, Italy 10- 12 May 2005. http://www.bwe.dk/download/articles_pdf/art-cct2005.pdf.

[388] *Tazama* Sehemu III.B.4.

[389] 2016 ESIA, §6.5.3 katika 14.

[390] Utafiti umeonyesha kuwa kutumia upya mfumo wa kutia baridi hutumia maji na kuachilia maji kidogo na kwa hivyo hupunguza kusongwa na kubanwa kwa viumb: Kristin Gerdes and Christopher Nichols, "Water Requirements for Existing and Emerging Thermoelectric Plant Technologies" *National Energy Technology Laboratory* (Aug. 2008) http://www.netl.doe.gov/energyanalyses/pubs/Water%20Benefits%20Primer_09_02_08.pdf; Union of Concerned Scientists, 'Nuclear Power and Water' *UCSUSA* (Dec. 2011) http://www.ucsusa.org/sites/default/files/legacy/assets/documents/nuclear_power/fact-sheet-water-use.pdf; May, J., and Van Rossum, M.K, "The Quick and the Dead: Fish Entrainment, Entrapment, and the Implementation and Application of Section 316(B) of the Clean Water Act" *Vermont Law Review* Vol. 20:376-493 (1995). Recirculating cooling systems are, however, more expensive than once-through cooling systems. It is therefore clear that the project proponent is selecting cheaper alternatives that are less environmentally friendly rather than the most suitable technologies.

[391] 2016 ESIA, §6.6.1 katika 15.

## I. Athari za kijumla za LAPSSET zimepuuzwa

Mbali na athari za moja kwa moja za mradi huu, IFC na wateja wake wanatakiwa kuzingatia "athari za kijumla ambazo hutokea ... kutokana na maendeleo mengine yaliyomo, yaliyopangwa au yanayofafanuliwa wakati mchakato wa utambulisho wa hatari na athari unafanyika.[392] "Vidokezo vya Taratibu za IFC PS hasa vinaonyesha kuwa," mahali ambapo miradi mingi hutokea, au inapangwa katika eneo moja la kijiografia "- kama ilivyo Lamu na katika maendeleo mbalimbali ya LAPSSET -" mteja hana budi kufanya Tathmini ya Jumla *(Cumulative Impact Assessment - CIA)* kama mchakato wa utambuzi wa hatari na athari."[393]

CIA ya 2016 ya ESIA inakubali kwamba miradi kadha "inatarajiwa" katika eneo hilo, ikiwa ni pamoja na vipengele vya mradi wa LAPSSET. Hata hivyo miradi hii haijumuishwi katika CIA kwa madai kwamba, wakati wa utekelezaji wake haijulikani.[394] CIA inajumuishi taarifa ndogo ya miradi mbalimbali ya LAPSSET, lakini madhara ya vipengele vya kando hayajatambuliwa au kutathminiwa, na katika sehemu nyingi LAPSSET uzingatiaji haupo kamwe. Kwa mfano, vipengele vya LAPSSET havizingatiwi katika kupima uwezekano wa ongezeko la idadi ya watu au athari kwa rasilimali za maji, taka, uhamisho wa lazima, miundombinu (inayohitajika kulinda ongezeko la idadi ya watu), huduma za umma, usafirishaji, na trafiki.

Kinyume na hitimisho ya ESIA, vipengele vingi vya LAPSSET vilivyopangwa katika Lamu vilikuwa na muda wa kutosha wakati ESIA ilikuwa inaundwa. Kwa hivyo, vingezingatiwa katika CIA ya kiwanda cha makaa. Kwa kweli, ESIA inataja LAPSSET kama mojawapo ya miradi mikubwa ya nguvu za umeme nchini Kenya ambayo inathibitisha haja ya kuwa na kiwanda cha makaa.[395] Jambo hili linafanya kutozingatiwa kwake katika uchambuzi hasa wa madhara ya jumla kuwa makosa.

Vipengele vya mradi wa LAPSSET vinavyohusika na kaunti ya Lamu sasa viko katika hatua mbalimbali za maendeleo, na baadhi ya vipengele hivyo viko katika maandalizi ya mapema wakati vingine vinajengwa. Kuvunjwa kwa ardhi ili kuanza Bandari ya Lamu kulifanyika mwaka 2012, na tangu wakati huo vituo mbalimbali vya miundombinu vimejengwa. Tovuti ya LAPSSET inaorodhesha hatua za utekelezaji wa vipengele hivi, na maegesho ya kwanza yanatarajiwa kukamilika mwaka 2018 (sasa imesitishwa kidogo hadi Juni 2019[396]) na maegesho mawili ya ziada kufikia mwaka wa 2020.[397] Vipengele vingine vya LAPSSET vilikuwa vimepiga hatua kubwa za upangaji wakati Ripoti ya ESIA ikichapishwa. Kwa mfano, ESIA katika barabara ya Lamu-Garissa, iliyofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), ilikamilishwa mwezi Aprili 2016.[398] Uboreshaji wa uwanja wa Ndege wa Manda tayari

---

[392] IFC PS 1, aya. 8. Tazama pia PS 3, aya. 11.
[393] Angalizo la Mwongozo 1, GN 38.
[394] 2016 ESIA Sura 10: Tathmini ya Jumla ya Athari, §10.1.
[395] 2016 ESIA Sura 3: Umuhimu wa Mradi, §3.3.
[396] Daily Nation "Kenyans to wait longer for first berth at Lamu Port" (1 Oct. 2018) https://www.nation.co.ke/news/Kenyans-to-wait-longer-for-port-berth/1056-4786110-y065hdz/index.html; Daily Nation "Questions persist on Lamu port viability as first ship set to dock (31 Mar. 2019) https://www.nation.co.ke/business/Questions-persist-on-Lamu-port-viability/996-5049626-tfkqaa/.
[397] Mamlaka ya LAPSSET "Bandari ya Lamu" http://www.lapsset.go.ke/projects/lamu-port/ (ilifikiwa mwisho 19 Machi. 2019).
[398] Systra Group *ESIA Study Report: Consultancy Services for Environmental & Social Impact Assessment and Detailed Engineering Design of Lamu-Garissa Road* (Apr. 2016) https://www.nema.go.ke/images/Docs/EIA%20-%201270%20-%201279/ESIA%20_1272%20Lamu-Garissa%20road%20report.pdf.

umekamilika (tangu mwanzo mwaka 2011).[399] Miji ya starehe ya Wilaya ya Lamu iko katika hatua ya maandalizi. Mwaka jana Serikali ya Kenya iliweka saini mkataba wa kazi za mwanzo katika bomba la mafuta ghafi ambalo litamalizika kwenye bandari la Lamu.[400]

Ingawa vipengele hivi vina muda tofauti wa utekelezaji na baadhi ya athari maalumu hazikujulikana wakati ESIA ikitolewa, jambo hili si sababu tosha kwa kutozingatiwa kwake katika CIA. CIA inadai kuwa upeo wake unahusisha muda wote wa kazi ya mradi wa miaka 25.[401] Hata kama baadhi ya vipengele vya LAPSSET viko katika awamu ya mwanzo, vipengele vyote vimeendelea hivi kwamba pana uwezekano wa kutekelezwa katika kipindi cha miaka 25 ijayo. ESIA ilipaswa kuzingatia taarifa yoyote iliyopatikana kuhusu athari za kila kipengele cha LAPSSET kinachpaswa kutekelezwa katika miaka 25 ijayo wakati kiwanda cha makaa kinafanya kazi.

Kila moja ya vipengele vya LAPSSET kina hatari na athari za kipekee, tangu athari za kimazingira zinazohusiana na kazi nyingi za ujenzi katika mji mdogo hadi athari athari za kijamii ambazo zinaambatana na ongezeko kubwa la idadi ya watu. Kwa pamoja, miradi hii ina uwezekano wa kuwa na madhara makubwa kwa watu na mazingira katika kaunti ya Lamu. Hii ndiyo hali ambayo kanuni za CIA ya IFC zilitarajiwa kushughulikia, na ni muhimu kwamba ESIA ya kiwanda cha makaa irekebishwe ili kuzingatia kila sehemu ya mradi wa LAPSSET, na athari zote kijumla. Tathmini hii inapaswa kuzingatia hasa athari za kijamii za kila kipengele, ambazo zinaonekana hasa kuingiliana na zile za kiwanda cha makaa na ni hatari kwa jamii katika eneo hilo ikiwa hazijatambuliwa vyema na kupunguzwa makali.

### J. Watu walioathirika hawatapata manufaa ya mradi-na hili litasababisha wanajamii kutouunga mkono

FC PS inatambua kuwa uungwaji mkono na wanajamii na ugawaji wa manufaa ni muhimu ili kuwa na usimamizi wa kina na kupunguza hatari za E&S na kuongezea manufaa mazuri ya mradi. Kama sera yake, IFC imechukua jukumu la kuchunguza endapo miradi inayohusisha athari mbaya kwa wanajamii inaungwa mkono na wanajamii. Katika miradi inayohusisha athari mbaya kwa wanajamii.[402] IFC PS pia hutarajia kuwa jamii zilizoathirika zinapata manufaa kutokana na mradi:[403] hali ambayo ni ya lazima endapo uungwaji mkono utapatikana.

ESIA inaeleza kuwa madhumuni ya kiwanda cha nishati ya makaa iliyopendekezwa 1,050MW ni kuwapa Wakenya umeme kwa bei nafuu ili kustawisha uchumi na kuwa katika orodha ya "ongezeko kwa gharama nafuu, kuaminika na uendelezaji wa usambazaji wa umeme" kama mojawapo ya athari ya kijamii ya kimsingi.[404] Kama ilivyojadiliwa hapo juu, ESIA haijumuishi

[399] Mamlaka ya LAPSSET "Uwanja wa Ndege " http://www.lapsset.go.ke/projects/airports/ (ilifikiwa mwisho19 Machi. 2019).
[400] LAPSSET Authority "Resort Cities" http://www.lapsset.go.ke/projects/resort-cities/ (ilifikiwa mwisho 19 Machi. 2019) na "Oil Pipelines" http://www.lapsset.go.ke/projects/oil-pipelines/ (last accessed 19 Mar. 2019); Business Daily "Tullow signs deal to build oil pipeline" (24 Oct. 2017) http://www.businessdailyafrica.com/corporate/companies/Kenya-Sh210-billion-crude-oil-pipeline-deal-Tullow/4003102-4153716-q6f1p2z/index.html.
[401] 2016 ESIA Sura 10, §10.2.
[402] Sera ya Uendelevu (Sustainability Policy), aya. 30.
[403] IFC PS 1, aya. 12, 31; IFC PS 5, aya. 9 (kuhamia makazi mapya bila hiari); IFC PS 7, aya. 15 na 17 (jamii asilia).
[404] 2016 ESIA Sura 8, §8.11.1 katika 85. Hata hivyo, taarifa zingine kutoka ESIA zinasaili kauli hii. Kwa mfano, ESIA Sura 1, §1.5 inaeleza kwamba umeme utakaotokana na Mradi huu tayari umelenga miradi mingine ya viwanda vitakavyotumia nishati nyingi kama vile reli, Konza City Technopolis, miradi ya LAPSSET Lamu, na chuma, ufuaji chuma na sekta ya viwanda. and the steel smelting and manufacturing sector.

RAP au IPP, na suala la ugawaji wa manufaa na watu walioathirika hata hivyo halijashughulikiwa katika ESIA.

Aidha, kwa kuzingatia majadiliano katika mashauriano ya awali ya jamii, haionekani kwamba Amu Power amejitahidi kuhakikisha kuwa jamii za makazi mapya, zilizoathirika kiuchumi, au zilizohatarishwa na mradi huo, zitapata manufaa ya msingi kutokana na mradi. Kama ilivyoelezwa katika maelezo ya ushauriano wa kijamii, kaya nyingi zilizoathirika hazina umeme.[405] Ufikiaji wa umeme mara nyingi hutegemea usambazaji wa umeme, kuliko uzalishaji.[406] Hata hivyo, Amu Power imefanya jitihada ndogo sana ili kuhakikisha kuwa jamii za Lamu zitapokea umeme, wakisema kuwa KPLC ndiyo ina mamlaka hayo.[407] Ingawa Amu Power haina mamlaka ya kuunganisha jamii na umeme, jukumu lake chini ya IFC PS hata hivyo linahitaji jitihada zaidi za "kutoa fursa kwa jamii na watu waliohamishwa ili kupata manufaa ya maendeleo kutokana na mradi."[408] Katika hali hii, ni rahisi kufikiri kwamba Amu Power inaweza kufanya jitihada hizo kutokana na jukumu la Serikali ya Kenya katika kuagiza mradi huu. ESIA haionyeshe kama hatua za wazi zimechukuliwa, mathalan kupanga na KPLC ili kufidia gharama za umeme wa mitaa kupitia bajeti ya mradi.

Fauka ya hayo, tunaelewa kwamba manufaa ya ajira kutokana na mradi imetiwa chumvi, kwa sababu asilimia arobaini (40%) ya kazi zote zimetengewa wafanyakazi wa Kichina.[409]

## VI. Jitihada zetu za kubainisha masuala haya na Amu Power, wawekezaji wake na mamlaka zingine

Tumehudhuria mikutano ya mashauriano ya wadau ambapo tuliuliza maswali kuhusu matatizo yetu. Maswali hayo hayakujibiwa au yalijibiwa kwa kupuuzwa, na habari za kupotosha.[410] Tumejaribu kushiriki katika mikutano ya ziada, lakini tumetengwa na kufanywa kusikia hatuna usalama.[411] Tumewasilisha maoni kwa njia ya maandishi, moja kwa moja kwa Amu Power, wanahisa wake (Gulf Energy na Centum), wawekezaji wake (ikiwa ni pamoja na IFC) na mamlaka za serikali zinazohusika, na kwa njia isiyo ya moja kwa moja ya taratibu rasmi za kushauriana, ikiwa ni pamoja na:

- Barua ya Save Lamu kwa African Development Bank (1 Oktoba 2015) - jibu lililopokelewa 1 Novemba 2015 na lilikuwana nakala ya Amu Power
- Barua ya Save Lamu kwa National Environment and Management Authority (12 Novemba 2015)

[405] 2016 ESIA Kiambatisho 9B, §3.1.18 (Ushirikishaji wa Wadau Log No. 18: Wanawake), kipengee 4.
[406] James Ryan Hogarth & Ilmi Granoff, Overseas Development Institute "Speaking truth to power: why energy distribution, more than generation, is Africa's poverty reduction challenge" (May 2015) https://www.odi.org/publications/9406-truth-power-energy-poverty-ambition-africa. Kwa sababu hii, kwa jumla usambazaji wa vitu vinavyotumiwa mara nyingi hutoa huduma bora kwa watu wasiopata nishati kwa njia rahisi: Lucy Stevens and others, Practical Action Policy and Practice "Poor People's Energy Outlook 2016" (2016). https://policy.practicalaction.org/resources/publications/item/poor-people-s-energy-outlook-2016.
[407] 2016 ESIA, Kiambatisho 9B, Taarifa za Mashauriano ya Jamii katika 157.
[408] IFC PS 5, aya. 9.
[409] 2016 ESIA Sura 4 §4.9.9.
[410] Tazama Taarifa ya shahidi Raya Ahmed, Mohamed Bakar, Mohammed Mbwana katika Mahakama ya Kitaifa ya Mazingira (National Environment Tribunal) iliyoambatwa katika Nyongeza 3; na Sehemu III C hapo juu.
[411] *Tazama Save Lamu Facing Intimidation and Interference*, deCOALonize, Medium (9 May 2017) https://medium.com/@deCOAL/save-lamu-facing-intimidation-and-interference-9007309d166e; na pia katika Sehemu III.C hapo juu.

- Barua ya Save Lamu kwa Bodi ya Usimamizi wa Ardhi ya Kaunti ya Lamu (Novemba 17, 2015) na Amu Power kupewa nakala
- Barua yaSave Lamu kwa African Development Bank (25 Novemba 2015) imechapishwa kwa Amu Power - *jibu lililopokelewa tarehe 18 Disemba 2015 lilikuwa na nakala ya Amu Power*
- Barua ya Save Lamu kwa Amu Power (Machi 13, 2016) - *idhini ya upokeaji kwa barua pepe kutoka kwa Bwana Njogu (Amu Power) (Machi 14, 2016) lakini hakuna jibu lililopokelewa*
- Barua ya Save Lamu kwa International Finance Corporation (8 Aprili 2016) - jibu lililopokelewa 22 Aprili 2016
- Barua ya Save Lamu na Natural Justice kwa Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (*National Environment Management Authority – NEMA*) (Agosti 29, 2016)
- Barua ya Save Lamu na Natural Justice kwa Tume ya Kudhibiti Nishati (Energy Regulatory Commission) (Agosti 29, 2016)
- Barua na maoni ya Save Lamu na Sheria ya Haki kwa Tume ya Udhibiti wa Nishati (Energy Regulatory Commission) (Oktoba 28, 2016)
- Barua ya Save Lamu kwa Viwanda na Commercia Bank of China (21 Desemba 2016) - *hakuna jibu lililopokelewa*
- Barua ya Save Lamu kwa African Development Bank (Novemba 27, 2017) - *hakuna jibu lililopokelewa*
- Barua ya Save Lamu kwa Viwanda na Commercia Bank of China (12 Desemba 2017) - *hakuna jibu lililopokelewa*
- Barua ya Save Lamu kwa Viwanda na Commercial Bank of China (13 Januari 2018 ) - *hakuna jibu lililopokelewa*
- Baruaya Kwasasi Farmers Self-Help Group kwa Wizara ya Usafiri (31 Agosti 2018) - *hakuna jibu lililopokelewa*
- Barua ya Kwasasi Farmers Self-Help Group kwa Mwenyekiti, Tume ya Ardhi ya Kitaifa (National Land Commission) (5 Novemba 2018) - *hakuna jibu lililopokelewa*
- Barua ya Kwasasi Farmers Self-Help Group kwa Mwenyekiti, Tume ya Ardhi ya Kitaifa (National land Commission) (13 Januari 2019) na nakala kupewa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira ya Taifa - *hakuna jibu lililopokelewa kutoka kwa Tume ya Ardhi ya Taifa; idhini ya upokeaji na vitendo*

*vilivyopangwa kutoka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (4 Februari 2019) lakini hakuna jibu la msingi lililopokelewa.*[412]

- Barua ya Save Lamu kwa General Electric (16 Januari 2019) - *jibu lilipokelewa 19 Februari 2019*
- Barua ya Save Lamu kwa Ubalozi wa China (14 Feb. 2019) - *hakuna jibu lililopokelewa*

Ripoti hii inapatikana kwenye Kiambatisho 4. Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, licha ya jitihada hizi nzuri za imani ya kushauriana, hatujawahi kupokea ushirikiano wa kina kuhusu hofu zetu.

## V. Tunahitaji tathmini ya ridhaa kuchunguza masuala yetu

Tunapinga kiwanda cha makaa kwa sababu kinahusishwa na hatari za baadaye katika maisha ya jamii yetu ya Lamu. Kiwanda cha makaa kilichopendekezwa Lamu kitaleta madhara ya kudumu, yasiyorekebishika na kinahatarisha maisha ya vitu muhimu katika riziki zetu, utamaduni wetu na mazingira yetu. Hofu zetu kuhusu hatari hizo zimetiliwa nguvu na ukosefu wa mashauriano na ushirikishaji wa jamii katika usanifu wa mradi. Zaidi ya familia 109 tayari zimeachwa bila mapato au uhakika wa chakula, baada ya kuondolewa kutoka kwenye mashamba yao bila fidia.

Tunaamini kwamba IFC inashiriki katika mradi huu unaoweza kuwa hatari kupitia wateja wawili wa fedha wanaotoa msaada wa kifedha kwa makampuni yanayohusika katika kiwanda cha makaa. Aidha, IFC ina historia ya mahusiano na asasi zingine za kifedha ambazo zimehusishwa na kiwanda cha makaa. Utaratibu huu wa uwekezaji unatufanya tuwe na hofu kwamba uwekezaji wa sasa katika Co-Operative Bank na Kenya Commercial Bank sio - wala hautakuwa - uhusiano wa pekee wa IFC katika kiwanda cha makaa Lamu na hatari na madhara yake makubwa katika jamii yetu. Jambo hili linaibua hofu kubwa kuhusu jinsi IFC inavyojitathmini, inavyosimamia, na inavyofuatilia uwekezaji wake mkubwa katika sekta ya kifedha ya Kenya.

Hatimaye, tuna hofu juu ya ukiukaji wa wazi, maalumu, na unaoendelea wa Mfumo wa Kudumu wa IFC katika maendeleo ya kiwanda cha makaa cha Lamu, ikiwa ni pamoja na Viwango vya Utendaji vya IFC na Mwongozo unaohusika wa EHS . Tunaogopa kwamba ukiukaji huu utakuwa mbaya zaidi kadri mradi utakavyoendelea. Kwa hivyo, malalamishi haya yanahitaji ofisi ya CAO itathmini ridhaa na ichunguze IFC na wateja wake ili kujua kama wamefuata kanuni zinazohusika za mazingira na kijamii, viwango na masharti. Tunatarajia kwamba CAO itapata uhahidi wa kutosha na usiopingika unaoonyesha kwamba IFC na wateja wake wamekiuka viwango hivyo.[413] Kwa hivyo, IFC inapaswa kuchukua hatua za haraka ili kuzuia ushiriki wa wateja wake katika mradi huu hatari na kutathmini kwa kina uwekezaji mpya katika sekta ya kifedha ya Kenya ili kuepuka madhara zaidi.

[Saini ziko baada ya ukurasa huu]

---

[412] Tunazingatia kwamba barua za wakulima kwa asasi mbalimbali za serikali zilikuwa maombi rasmi ili wapewe taarifa, na ukosefu wa majibu kutoka asasi hizi ni ukiukaji wa sheria za Kenya.
[413] *Kinyume na* Sera ya Uendelevu(Sustainability Policy), aya. 22.

**Kwa niaba ya : Save Lamu** **Tarehe:** 27/3/2019

Jina: ABUBAKAR MOHAMED ALI
Saini:

Jina: MOHAMED MBWANA
Saini:

Jina: ADAM LALI KOMBO
Saini:

Jina: KHADIJA ABDILLAH
Saini:

Jina: Afuwa Ahmed
Saini:

Jina: Mohamed Athman
Saini:

Jina: KHADIJA SHEKUWE
Saini:

Jina: WALID AHMED ALI
Saini:

Jina: Ishaq Abubakar
Saini:

Jina: Khadija Ernst
Saini:

Jina: ELBUSAIDY SWALEH
Saini:

Jina: Somo M. Somo
Saini:

Jina: Raya Fumau
Saini:

Jina: Khadija Juma
Saini:

**Kwa niaba ya: Kwasasi Farmers Self Help Group**

**Tarehe:** 8/4/2019

Jina: ALI SALIM

Saini: Aug